**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 20 APRILI, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Spika (*Mhe. Samuel J. Sitta*) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:-**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali juu ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements for the Financial Year ended 30th June, 2009).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):-**

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 *(The General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of the Central Government for the Year ended 30th June, 2009).*

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali Kuu na Bodi nyingine kwa mwaka wa fedha 2008/2009 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and other Bodies for the Financial Year 2008/2009).*

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Utekelezaji wa Taarifa za Ukaguzi kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2010 *(The General Report of the Controller and Auditor General on the Performance Audit (VFM) Reports for the period ended 31st March, 2010).*

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Utekelezaji wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kazi za Barabara, Machi 2010 *(The Performance Audit Report on Road Works on March, 2010).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 64

### Serikali Kujenga Hospitali kubwa katika Tarafa za Rulenge na Murusagamba

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (K.n.y. MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa za Rulenge na Murusagamba zipo mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara ambapo hospitali teule ya Murusagamba na hospotali nyingine kubwa na Nyamiyaga zipo:-

Je, ni lini Serikali itajenga hospitali kubwa katika Tarafa hizo mbili ili wakazi wake wapate huduma bora za afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feetham Filipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Rulenge kwa sasa inacho kituo cha Afya Bukiriro cha Serikali na hospitali ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki Dayosisi ya Rulenge ambavyo kwa pamoja vituo hivi vinatoa huduma kama vituo vya Rufaa na kwa sasa vinatoa huduma inayojitosheleza.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Rulenge hupokea ruzuku kutoka Serikalini kila mwaka kwa ajili ya uendeshaji kwa asilimia 60%. Serikali inaendelea kuimarisha hospitali hiyo ili itoe huduma kwa kiwango cha hali ya juu badala ya kujenga hospitali nyingine. Tarafa ya Murugasamba inacho kituo cha Afya katika Makao Makuu ya Tarafa. Halmashauri ya Wilaya ya Ngara inaendelea kufanya upanuzi wa kituo hicho mwaka hadi mwaka kwa kutumia fedha za ruzuku ya maendeleo hadi hapo kitakapokuwa hospitali. Kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 2006/2007 ulifanyika ukarabati wa wodi ya wazazi na kujenga nyumba 2 za watumishi na vyoo vya wagonjwa;

(ii) Mwaka 2007/2008 ulifanyika ukarabati wa wodi za wanaume na wodi za watoto;

(iii) Mwaka 2008/2009 ujenzi wa maabara mpya;

(iv) Mwaka 2009/2010 ujenzi wa nyumba mbili za watumishi na kuweka mfumo wa maji katika wodi zote; na

(v) Mwaka 2010/2011 yaani huu unaokuja, kutajengwa wodi moja kwa ajili ya wanaume nyingine itakuwa kwa ajili ya wanawake.

Ni matumaini yangu kuwa Halmashauri inapata fedha za MMAM na kutokana na umuhimu wake, ni mategemeo yangu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ngara itaendelea kutenga fedha ili kukifanyia kituo kuwa hospitali.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa inajulikana wazi Halmashauri nyingi hazina fedha za kutosheleza kujenga hospitali ambazo zinahitaji fedha nyingi. Kwa Wilaya ya Ngara anakotoka Profesa Banyikwa, Wilaya haina fedha za kutosha ili kuweza kujenga vizuri hizi hospitali kwa ajili ya wananchi wake.

Je, ni lini Serikali itaongeza fedha za kutosha ili hospitali hizi ziweze kupata kujengwa vizuri pamoja na kuwa na vifaa vyote vya mabaara na madawa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kinachozungumzwa hapa ni suala la Bajeti ambayo tunaipitisha wote sisi hapa Bungeni. Kiasi kinachotengwa hapa ndicho ambacho tunakiona kama ni kipaumbele chetu kama Taifa. Kwa hiyo, hela ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wilaya ya Ngara ni hizo ambazo Wilaya ya Ngara ilionyesha kwamba zinahitajika kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, nakubali kabisa anachozungumza Mheshimiwa Mwananzila kwamba hela ambazo tunazo ni kidogo katika Bajeti yetu sisi ambayo inakuonyesha matumizi na mapato ya Serikali, asilimia 60 ndiyo tunatengeneza hapa ndani na asilimia 40 inatoka nje kwa wahisani. Sasa kama unatumia mfumo wa namna hiyo na kama hujitegemei wewe mwenyewe humu ndani, unafanyaje sasa haya yanayozungumzwa hapa.

Ninatambua kabisa unyeti wa jambo analolizungumza Mheshimiwa Mbunge, lakini mimi nasema hapa ni suala la *priority.* Kama tukiamua kwamba kipaumbele kwetu sisi hapa ni kusaidia katika hizo hospitali, basi tukija kwenye Bajeti hii inayokuja tuelekeze mafungu haya na hii changamoto sasa inakwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Matatizo yaliyoko Ngara ndiyo matatizo yaliyopo katika jimbo la Chalinze hususan Msata, Lugoba na Chalinze. Wagonjwa ambao hupewa rufaa ya kupelekwa Tumbi hulazimika kuchangia gharama za usafiri kwa gari ile ya wagonjwa takriban 70,000 mpaka shilingi laki moja na mafuta yanayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya vituo vya afya hivyo nilivyovitaja Chalinze, Lugoba na Msata ni lita 100 mpaka 150 kwa mwezi.

Je, Serikali haioni sasa wanacheza mchezo wa karata tatu kwa nini hatua za makusudi zisifanywe za kujenga hospitali kubwa eneo la Chalinze kwa kuokoa majeruhi wa ajali za barabarani na wagonjwa wengine hasa akina mama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naona kama maswali ndani yake. La kwanza hili analozungumza la kwamba wakati mwingine wagonjwa na wale ambao wanawahudumia wanalazimika kuingia gharama. Inawezekana kabisa kwamba inatokea hiyo na kwamba anachosema Mbunge ni kweli. Inawezekana Bajeti iliyotengwa pale kwa ajili ya kuweza kuwachukua wagonjwa kutoka hospitali moja au kutoka kijijini kupeleka pale hospitali imekwisha, sasa akawajibika kufanya hivyo. Hili ni changamoto yetu sisi wenyewe kama Halmashauri. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba kiasi kinachotengwa kwa ajili ya kupeleka wagonjwa na kuwasaidia. Unachoweza kukifanya hapa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *ambulance* na tuliwahi kujibu hapa ndani. Tukasema kwamba ukishakuwa na *ambulance* ukawa pia na mfumo wa mawasiliano ambao unaweza ukapiga simu ukamwambia mtu aliyeko mahali fulani njoo basi unaweza ukampeleka mgonjwa yule akapata huduma husika haraka.

Sasa anazungumza pia kuhusu suala la kuanzisha hospitali katika eneo la Chalinze. Ninavyofahamu wazo ni zuri lakini utakumbuka kwamba Chalinze iko karibu na hospitali inayoitwa Tumbi, ambayo ndiyo inayowasaidia watu wengi pale. Lakini kama Mheshimiwa Maneno anaona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo pamoja na kwamba *facility* ya Tumbi iko hapa ambayo tumeiimarisha, basi hili ni wazo zuri, tulilete tuliangalie sisi wote kwa pamoja na Halmashauri ya Bagamoyo sasa ione jinsi ambavyo tutaweza kuliingiza pale. Tulifikiri kwamba ukiimarisha pale Tumbi utakuwa unawasaidia na Mheshimiwa Maneno pale atakuwa amefaidika na watu wake watakuwa wamefaidika pale. Lakini nasema wazo ni zuri kama lipo, njooni tuzungumze ili tuone tutakavyosaidia katika eneo hilo.

Na. 65

**Ujenzi wa Hosteli za Wasichana Mashuleni**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la watoto wa kike kupata mimba shuleni hutokana na mazingira mabaya ya shule hasa ukosefu wa hosteli:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiweke Sheria kuwa, ujenzi wa shule zote za Sekondari za Kata ni lazima uende sanjari na ujenzi wa hosteli za wasichana?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inachangia kuharibu na kuhatarisha maisha ya watoto wa kike kwa kutozingatia ubora wa mazingira ya shule ikiwemo watoto kukodisha vibanda vinavyozunguka shule kwa kuishi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuwepo na hosteli katika shule za Sekondari ni utaratibu mzuri.

Aidha, utaratibu huu unasaidia wanafunzi wakiwemo wasichana kutulia shuleni kusoma vizuri na usalama kwa wanafunzi ili kuweza kuepuka kwa kiasi kikubwa matatizo yanayoweza kujitokeza kama utoro na wasichana kupata mimba zisizo tarajiwa kutokana na mazingira hatarishi yanayozunguka shule.

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari za Kata alizoelezea Mheshimiwa Mbunge, zilijengwa kwa nguvu za wananchi wakisaidiana na Serikali. Kazi kubwa imefanyika ya michango ya fedha, mali na nguvu kazi kutoka kwa wananchi.

Aidha, kwa baadhi ya shule hususan katika maeneo ya wafugaji ambapo familia zinahama hama Serikali imejitahidi kujenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachofanya hivi sasa, inaendelea kushirikiana na jamii husika kuona uwezekano wa kujenga hosteli katika shule kwa ajili ya wanafunzi lakini sio kwa kuweka Sheria.

Ziko baadhi ya shule ambazo umbali wa kufika shuleni ni mfupi, hivyo mahitaji ya hosteli kwao sio makubwa sana. Wazo na mwelekeo wa utekelezaji ni mzuri pamoja na kuwa ipo changamoto ya gharama za ujenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika kipengele (a) juhudi za Serikali kushirikiana na jamii zinaendelea ili kujenga hosteli katika maeneo yenye mahitaji.

Hata hivyo, shule ni zetu na watoto ni wetu kikubwa ni wote tujitahidi kuwasaidia watoto kimaadili ili tatizo hili lisiwe kubwa na kuchukua hatua kali kwa wale wote ambao wanaobainika kwamba wamehusika na vitendo vinavyoathiri masomo ya mwanafunzi kama vile kuwapatia mimba.

Hata hivyo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kujenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike, kwa kuweka kipaumbele katika maeneo yenye mazingira magumuhasa maeneo ya wafugaji. Kwa mfano, Mkoani Manyara Serikali imejenga hosteli katika shule ya sekondari ya Yaeda Chini ili kuziwezesha jamii za Wahadzabe kukaa shuleni muda wote wa masomo.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, sina swali la nyongeza, isipokuwa nashukuru kwa kutokana na majibu mazuri ya Serikali.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi. Umri wa *adorecient* ni umri wa mchecheto watoto wote wa kike na wa kiume wanataka kujijua. Ndiyo umri mbaya. Huwezi kuushikilia kwa sababu ndiyo umbile la binadamu. Bahati mbaya Serikali uwezo wa kujenga hosteli pesa ni kidogo.

Lakini bahati mbaya pia Mungu hajakubaliana naye kusudi wasimamishe hii michecheto katika umri huu. Je, na kwa sababu mtoto wa kike ndiye pekee anayeathirika kwa sababu ya umbile lake la kuwa ana *uterus* kuliko wa kiume.

Je, Mheshimiwa Waziri akubaliane nami ifike hatua sasa itakapotokea bahati mbaya hiyo na mtoto akapata mimba wa kike na akajifungua, tutengeneze shule maalum kwa watoto hawa badala ya kuwaacha na kwa sababu ya *anatomy* Mungu aliwaumba na *phisiology? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, huu umri anaozungumza Mheshimiwa Mbunge Dr. Gama anauita kipindi hiki cha *adorisence* mimi *professionally* ni mwalimu, naifahamu hii habari anayoizungumza hapa.

Huu umri unaitwa *foolish age,* ndiyo umri wenyewe huo, ambao mtu akitumbukia pale, unaweza ukaingiza mambo ya ajabu ajabu pale, hizi tabia za kifataki fataki ndiyo zinajitokeza hapo na mambo mengine yanafika hapo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wabunge wanachosema hapa ni jambo la msingi sana. Usipowakinga watoto wetu hawa kwa maana ya kwamba utawawekea hosteli na kwamba hawatakutana sasa na hali hiyo na kipindi chenyewe kama anavyosema Dr. Gama ndicho hicho ambacho ni hatarishi sana *then* utakuwa na matatizo makubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kimsingi hilo hakuna mtu anayepata tatizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapati tabu kuelewa hilo. Hilo analifahamu kabisa kwamba ni kipindi hicho cha kwanza kilichosisitizwa hapa ni suala la kusimamia maadili.

Sisi kama jamii wote kwa pamoja tunatakiwa tushirikiane kuwasaidia watoto wetu hawa, kujenga maadili ya Kitanzania, kuhakikisha kwamba tunakemea tabia hizi zinazojitokeza, kuhakikisha kwamba watoto wetu wanalelewa katika misingi ya Tanzania na msingi ambao utampata Mtanzania mzuri kesho na kesho kutwa. Hiki ndicho kinachozungumzwa.

Sasa kuna hili analolizungumza hapa la kwamba tujenge na kwamba watoto wamepata ujauzito, wakishamaliza waende. Mheshimiwa kama nilisikiliza vizuri na mimi hapa sisinzii huwa nasikiliza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwantumu alisimama hapa kwa niaba ya Serikali, akaeleza akasema kwamba ni lazima utueleze pia, maana ni mjadala sasa huu mpana, lazima utuambie kwamba mtoto huyu kama mama atarudishwa shuleni kule mtoto atamwangalia nani?

Lazima tuangalie pia kwamba anapokwenda kule shule, unamrudisha shuleni kuendelea na massomo watamnyanyapaa wenzake. Limesemwa hapa, yapo mambo mengi ambayo yanazungumzwa hapa ambayo bado ni mjadala lijadiliwe na majibu yapatikane na kwa kuzingatia kuwa hili ni suala la kisera.

Kwa hiyo nataka niafikiane na Mheshimiwa Dr. Gama anachozungumza ni sahihi. Lakini sasa hayo ni mawazo yake, sasa ndiyo tuanze kufikiri wote kwa pamoja kwamba tunafanya fanyaje. Pia tuangalie suala hili usije ukaweka *precedence* ikafungua sasa mlango mpana zaidi halafu ukapata matatizo makubwa zaidi. Lakini kimsingi tunaiona *point* yake, kwa hiyo tutaitafakari wote kwa pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nalazimika kusitisha kidogo, mtiririko wa kipindi cha maswali. Kwa sababu leo hii kwenye *Gallery* ya Spika tuna mgeni mashuhuri na ameandamana pia na wageni wengine mashuhuri kutoka nchi rafiki sana ya Jamhuri ya Watu wa China na ratiba yao haiwaruhusu kuendelea kusikiliza kipindi hiki cha Bunge kwa muda mrefu.

Kwa hiyo, bora niwatambulishe sasa ili uwepo uwezekano sasa wa anayeongoza shughuli za wageni wetu kuwapeleka kuona sehemu nyingine za Dodoma na sehemu nyingine za nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mbele yetu leo yupo Madam Young Junki, ambaye yeye ni Makamu wa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa *NPC National People's Congress of China.* Sasa hii kwa tafsiri yake *National People's Congress* ndiyo Bunge. Huyu anayeitwa Makamu Mwenyekiti ndiye Naibu Spika. Kwa hiyo, tunafurahi sana. *Please rise up. (Makofi)*

*It is an honor and pleasure for us to be able to receive you in Tanzanian Parliament. We realize that the relationship between the two countries, China and Tanzania, have been cordial and exemplary for many years, but this is a special honor for the Parliament of Tanzania to receive a dignitary of your status here in Dodoma.*

*We are especially pleased because you only arrived yesterday and you had to drive to Dodoma, which is not a very pleasant experience, but you can be sure this afternoon we will take you back to Dar-es-Salaam by plane. (Makofi).*

Pamoja naye, ameandamana na Mheshimiwa Lin Jin Koin, *Miss Lin please!* Huyo ni Makamu wa Rais wa *Chinese Peoples' Association for Peace And Development.* Kamati ya Bunge inayopigania amani hapa duniani. Ni mtu mzito sana huko kwao.

Wengine ni Mheshimiwa Balozi wa China hapa nchini. *Ambassador please!* Tunampenda sana Balozi huyu, anafanya kazi kubwa ya kujenga na kuimarisha mahusiano baina ya China na Tanzania. Waliosalia ni baadhi ya wajumbe wa msafara wa mgeni wetu mashughuri. *On behalf of the Members of the Parliament I am obliged to express our solidarity with you during this time, when you have had natural disasters like earth quakes that have affected your people.*

*We feel for you and we trust that the Chinese People will be able to absorb this disaster and mach forward in development. Thank you very much and we wish you a pleasant stay in our country. Thank you. (Makofi).*

Waheshimiwa, tunaendelea sasa. Tunahamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando.

Na. 66

**Mafunzo kwa Watumishi wa Umma**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi wanahitaji mafunzo stadi na taaluma mbalimbali ili kufanikisha utendaji wao wa kazi:-

(a) Je, ni watumishi wangapi wa umma wamepewa nafasi na mafunzo ndani ya nchi kwa mwaka 2007-2009?

(b) Je, ni watumishi wangapi wa Umma wamepatiwa mafunzo nje ya nchi kwa kipindi hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2007 hadi 2009 Watumishi wa Umma 14,544 walipatiwa mafunzo katika Taasisi mbalimbali ndani ya nchi. Kati ya watumishi hawa 9,865 ni watumishi wa Halmashauri za Wilaya na 4,679 ni watumishi wa Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, watumishi waliopatiwa mafunzo nje ya nchi kwa kipindi cha mwaka 2007 hadi 2009 ni 3,110. Mafunzo haya ni pamoja na Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili na Mafunzo ya Kiutendaji ya muda mfupi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumwuliza swali moja tu la nyongeza. Je, katika majibu ya swali (b), kuna watumishi wowote wanaotoka upande wa Zanzibar, waliofaidika na programu hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, sio rahisi sasa hivi kuweza kumjibu kwamba wapo, lakini nina uhakika wapo ingawa sijui Idadi ni kiasi gani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya, swali la nyongeza. Wahandisi waangalie kuna tatizo pale kwa Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Kabwe Zitto, pale.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapo watumishi wa Umma ambao wanajiendeleza kielimu, wengine wanafadhiliwa na Serikali na wengine wanajifadhili wenyewe kwa nia ya kuongeza ujuzi na maarifa kwenye kazi zao.

Lakini watumishi hawa wanapomaliza elimu yao, hawatambuliwi na Serikali kwa muda mrefu na na wengine wala hawahamishwi vituo vya kazi, kitendo ambacho kinasababisha kukata tama na wengine hata kuacha kazi.

Je, Serikali inasemaje kuhusu watumishi hawa? Na inasemaje kuhusu waraka wake ambao unathamini elimu yao na unasema kuwa wabadilishwe vituo vya kazi na kutahminiwa na Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kuwapatia mafunzo watumishi sio kuwahamisha vituo vyao vya kazi, bali ni kuwajengea uwezo ambao watumudu kufanya majukumu yao ambayo wamepewa. Kwa wale ambao kwa elimu yao inakuwa labda eneo lile waliopo inakuwa hawafiti, huwa tunawafanyia mabadiliko. Lakini lengo kuu la mafunzo, si kuwahamisha kituo cha kazi. *(Makofi)*

Na. 67

**Serikali Kujenga Mahakama Za Wilaya Na Mahakama Za Mwanzo**

**MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inaonekana kuweka mkazo mkubwa katika ujenzi wa Mahakama za ngazi ya juu zikiwemo Mahakama Kuu na Mahakama za Mkoa.

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kujenga Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo ambazo ziko katika hali mbaya?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhanii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama nyingi za Wilaya na zile za Mwanzo zipo katika hali mbaya. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu katika mwaka huu wa fedha inatarajia kujenga Mahakama nne za mwanzo katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Mtwara na Arusha. Aidha kupitia Mpango wa Maboresho ya sekta ya Sheria, jumla ya Mahakama 20 za Mwanzo zitajengwa katika mwaka huu wa fedha katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Pwani, Rukwa, Morogoro, Kilimanjaro, Iringa, Mtwara, Manyara, Iringa, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mara na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kuwa, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haina uwezo wa kujenga na kukarabati Mahakama zote nchini kwa wakati mmoja. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini na wananchi kwa ujumla, kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kujitolea kujenga Mahakama hususani zile za Mwanzo. Nia ikiwa ni kuongeza huduma za Mahakama karibu na wananchi.

**MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo hayana ukweli wa utekelezaji, napenda kumwuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, katika Bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri, aliahidi kwamba Wizara yake itajenga Mahakama 10. Na mpaka hivi sasa hakuna Mahakama hata moja aliyojenga. Aidha bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri, anaahidi kujenga Mahakama 20. Je, Mahakama zote hizi anazotoa ahadi, atazijenga lini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali ilisema ingejenga Mahakama 10 kupitia mradi wa *Legal Sector Reform Programme* na mwaka

huu pia tulisema tutaongeza Mahakama 10, na ndio hizi Mahakama 20 ambazo nimezisema. Tatizo lililopo sasa hivi ni kwamba Mahakama hizi zinajengwa kwa pesa ambazo zinatoka kwenye Benki ya Dunia na machakato wa kuzipata pesa hizi, pamoja na matumizi ya sheria yetu ya ununuzi, na mnaifahamu jinsi ilivyokuwa ngumu, zimechelewesha ujenzi wa Mahakama hizi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba pamoja na changamoto hizo, mwaka huu tuna uhakika wa kuzijenga Mahakama hizi 20 na mchakato umeshaanza, tayari tumepata msimamizi tunamwita *Consultant*, na sasa tunatafuta wakandarasi wa kujenga Mahakama hizi kwa mara moja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kuongeza kasi ya ujenzi wa Mahakama. Je, Serikali ina mpango sasa wa kujenga Mahakama ya Wilaya ya Mpanda ambayo inatumia majengo yaliyokuwa ya Mahakama ya Liwali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama nyingi za Mwanzo sasa hivi zinatumia majengo ambayo sio ya Mahakama. Hili ni suala la kihistoria, huko nyuma Mahakama hizi zilikuwa zinaitwa *Native Courts* na zilikuwa zinahudumiwa na Halmashauri zetu. Na ningependa kutoa wito sasa hivi kwamba Halmashauri zichukue tena jukumu hili la kujenga na kuzi-*maintain* Mahakama hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezekano wa kujenga Mahakama ya Mpanda, naomba nimshauri tu ndugu yangu avute subira tukae, labda katika Bajeti ya mwaka huu unaokuja pengine tutaiweka Mahakama hiyo nayo tuijenge. Nia ni kujaribu kupata majengo bora zaidi ambayo yanaambatana pia na majengo ya Mahakimu katika hizi Mahakama mpya ambazo tunajenga.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna jengo la Mahakama Kuu pale mjini Shinyanga ambalo ujenzi wake unaonekana kuwa umesimama. Je, ni lini ujenzi huo utaendelea tena ili kusudi jengo hilo limalizike mapema na kuweza kuchangia katika kupendezesha mji wa Shinyanga, ingawa nafahamu wananchi wa Shinyanga hawatahukumiwa pale kwa sababu ni wataratibu sana na wanafuata sheria za nchi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Dr. Charles Mlingwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajenga Mahakama Kuu katika Mkoa wa Shinyanga na hii ni katika utaratibu wetu wa kuhakikisha kwamba tunajenga Mahakama Kuu katika kila Mkoa kama tulivyosema katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ya mwaka 2005. Mpaka sasa Mahakama hii imefikia katika hatua nzuri na tunachongoja ni kwenda juu kumalizia. Sasa ninachoweza kusema ni kwamba tutahakikisha Mahakama

hii inamalizwa haraka iwezekanavyo, na itawahukumu watu wote wakiwemo pia watu wa Shinyanga, kama watahusika na kupelekwa katika Mahakama hiyo.

Na. 68

**Uuzaji Wa Shamba la Mkonge la Kumburu Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mchakato wa ubinafsishaji na uuzaji wa shamba la Mkonge la Kumburu Wilayani Muheza, ulikuwa chini ya *PSRC* na sasa chini ya *CHC:-*

(a) Je, shamba hilo limeuzwa lini, kwa kiasi gani na kiasi gani kimelipwa hadi tarehe 31 Disemba, 2009?

(b) Je, Mwekezaji aliyenunua amekabidhiwa Hati Miliki ya kumiliki shamba hilo kwa jina lake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, shamba la Kumburu lililoko Wilaya ya Muheza lilikuwa shamba la Mamlaka ya Mkonge Tanzania. Shamba hilo limeuzwa kwa Kampuni ya *"Silver General Distributors Limited"* inayomilikiwa na Watanzania. Aidha, shamba hilo liko umbali wa kilometa 16 kutoka kiwanda cha *TANCORD* kilichoko Ngomeni, Muheza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shamba la Kumburu liliuzwa tarehe 1Desemba, 1998 kwa bei ya shilingi 108,200,000. Hadi tarehe 31 Desemba, 2009 jumla ya shilingi 89,531,220 zilikuwa zimelipwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Mwekezaji aliyenunua shamba hilo amekwishakabidhiwa Hati Miliki ya shamba hilo kwa jina lake.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimwia Spika, imepita sasa miaka 12 tangu shamba hilo liuzwe na hadi sasa bado zaidi ya shilingi milioni 18.6 zinadaiwa. Lakini Mwekezaji ameshapewa Hati ya kumiliki shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upo mgogoro mkubwa sasa hivi sasa kati ya Mwekezaji na wananchi waliovamia shamba hilo zaidi ya miaka 20 iliyopita. Na kwa sababu fedha bado hazijalipwa. Je, Serikali haioni sasa kwamba hii ni fursa nzuri ya kuweza kukaa chini kati ya Mwekezaji na wananchi ili kuondoa mgogoro uliopo wa ardhi katika eneo hilo na wananchi wanaotafuta ardhi wakapata nafasi badala ya kutaka kudai hela ambazo hazijalipwa kwa zaidi miaka 12 iliyopita?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ikabisa na ninakubaliana na yeye kwamba salio lililobaki ni milioni 18,669,000. Lakini nipende kumhakikishia kwamba Bodi ya Wakurugenzi wa *CHC*, yaani *Consolidated Holding Corporation*, tarehe 26 Machi, 2010 walifika kutembelea shamba hilo na Maofisa wameshatembelea mara nne *assets* zote za katani na za mkonge na hivi ninavyosema ni kwamba tayari shamba hilo linaendelezwa. Na nikuhakikishie kwamba wanaliendeleza kutokana na taratibu zilizopo, kwa sababu mashamba haya ya mkonge unaweza ukaona kwamba halija endelezwa, lakini taratibu za mkonge ni kwamba shamba linalimwa 10% kila mwaka kusudi uache eneo lingine liweze kuiva kwa maana ya kilimo cha *rotation cropping.*

Kwa hiyo, shamba hili linaendelezwa na *CHC* imeshaanza kufuatilia hizo fedha, hivi karibuni zitapatikana. Nadhani suala lilikuwa ni ufuatiliaji wa hizo fedha.

Lakini kama watafikia mahali kwamba wameshindwa kulipa hizi milioni 18 watakuwa wamevunja mkataba wa manunuzi kwa maana ya *Sales Contract. K*wa hiyo, maana yake litarudishwa Serikalini. Lakini sitegemei kwa hatua waliyofikia sasa hivi wameshalipa zaidi ya 75% watashindwa kulipa hizo 18.

Kwa hiyo, suala hilo litakamilika hivi karibuni kwa sababu kama nilivyosema *CHC* ilivyokabidhiwa imeshatembelea pale hata mwezi mmoja haujapita.

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *PSRC* ina utaratibu wa kuuza mashamba na imetokea imeuza eneo la Kijiji kwa wawekezaji kwa kusema kwamba ni eneo liko chini ya *PSRC* bila ya wao kuwa na uthibitisho wa hati yoyote. Wanakijiji wako katika *desperate position* ya kutoishi kwa amani; suala hili limeshafika ngazi mbali mbali.

Je, Serikali ina uamuzi gani kumaliza tatizo hili, ili wanakijiji hawa waishi kwa amani?

**SPIKA:** Ni shamba hilo hilo au jingine?

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, Mashamba haya yako Wilaya hizi tatu, Muheza, Pangani na Handeni.

**SPIKA:** Sasa lako la Pangani, hujalitaja, umesema tu shamba shamba.

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ni shamba la Mivumoni ambalo liko Pangani na Muheza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Rished Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa baada ya kumaliza kipindi cha maswali na majibu nikutane na Mheshimiwa Rished kusudi tuweze kupata undani wa tatizo hili ili tuweze kupata undani wa tatizo hili ili Serikali iweze kulishughulikia kwa sababu sina undani wa tatizo hili.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali tatizo la ubinafsishaji wa mashamba limekuwa ni tatizo kubwa sana hapa nchini. Katika taarifa ya mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma iliyotolewa tarehe 29 Aprili, 2009 tulizungumzia tatizo la shamba la Mahindi la Mbozi na shamba la Mpunga la Kapunga, ambapo Serikali pamoja na kuuza shamba lile liliuzwa mpaka kijiji ambacho wananchi wanaishi na mpaka sasa Serikali haijatoa taarifa ya mapendekezo ya Kamati kuhakikisha kwamba kile kijiji na sehemu ya ardhi yao inarudishwa.

Je, Wizara ya Kilimo na chakula mpaka sasa imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba shamba la Mbozi linagawiwa kwa wananchi na shamba la Kapunga eneo la wananchi la kijiji linarudi kwa wananchi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kama ifuatavyo:-

Shamba la Mbozi la Mahindi lilikuwa linamilikiwa na *NAFCO* limekabidhiwa kwa *agency* ya kuzalisha mbegu na wananchi ambao wanaishi kando kando ya lile shamba wanashauri kufanya mkataba na *agency* ya mbegu kwa ajili ya kuzalisha mbegu na ile *agency* itakuwa itakuwa inanunua mbegu inayozalishwa na wakulima hao hapo shambani yaani *Contract Farming.* Kwa hiyo, sisi hatuna mgogoro wowote na kama upo tunaweza kushirikiana na vyombo vingine vya utawala vilivyoko kule kwa ajili ya kumaliza migogoro ya kiutawala inayoweza kuwa inatokea katika maeneo hayo.

Kuhusu shamba la Kapunga, shamba lile hakuna kijiji kilichouzwa shamba lile lilikuwa linahusisha maeneo mawili, eneo moja tangu zamani wakati linamilikiwa na *NAFCO* kulikuwa na eneo ambalo lilikuwa linalimwa na *NAFCO* na kulikuwa na eneo ambalo lilikuwa linalimwa na wakulima wadogo. Lile eneo ambalo linalolimwa na wakulima wadogo linaendelea kuwa la wakulima wadogo, mimi mwenyewe nimewahi kufika na kuzungumza na mwekezaji na kumshauri kwamba pamoja na kuendeleza ile

sehemu ya shamba lake afikirie vilevile kuwasaidia wale wakulima wadogo kupata maji kwenye mfereji ambao tangu zamani ulikuwa unapeleka maji katika eneo lile kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo.

Kwa kweli sera tunayotekeleza ni kuhakikisha kwamba wakulima wakubwa wanafanya kazi kwa mahusiano mazuri na wakulima wadogo. Kwa hiyo, kama liko tatizo litakuwa ni tatizo la kiutawala ambalo tunaweza kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Uongozi wa Wilaya ya Mbarali katika kulishughulikia. *(Makofi)*

Na. 69

**Mipango ya Kuwawezesha Wananchi Kuboresha Kilimo Vijijini**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wizara ina mipangio mizuri kwa wakulima waishio vijijini katika kuboresha kilimo kwa kuwapatia elimu ya kilimo na nyenzo za kilimo:-

Je, Serikali imewandaa vipi wakulima kwa sasa na imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kuboresha kilimo vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ili kuboresha na kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kiweze kuchangia katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa wakulima na Taifa kwa ujumla na pia kujitosheleza kwa chakula.

Mikakati hiyo inahimiza kukuza tija na uzalishaji katika kilimo, mifugo na uvuvi na hatimaye kumtoa mkulima katika kilimo cha kujikimu na kuwa cha kibiashara na chenye tija.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mipango na mikakati hiyo, ni Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, *Agricultural Sector Development Strategy (ASDS,* unaotekelezwa nchi nzima kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, *Agricultural Sector Development Programme (ASDP).*

Katika ngazi ya kijiji waliko wakulima, *ASDP* inatekelezwa kupitia Mipango ya kuendeleza kilimo katika wilaya yaani *DADPs.* Ili kujenga umiliki, *ownership,* na kuweka misingi imara katika kutekeleza mipango hii. Wakulima wanashiriki katika kuibua miradi ya Maendeleo ya kilimo inayotekelezwa katika maeneo yao, kupitia

Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji, *Village Agricultural Development Programme (VADPS).*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka ili kuboresha kilimo vijijini. Kiasi kilichotengwa kimekuwa kikiongezeka kutoka 2.95% mwaka 2001/2002 hadi 7.6% mwaka 2009/2010.

Fedha hizi zimekuwa zikitumika katika nyanja mbalimbali kama vile kutoa mafunzo kwa wakulima, kupitia utaratibu wa mashamba darasa, kutoa mafunzo kwa Wagani, kuwapatia vitendea kazi wagani, ujenzi wa vituo vya rasilimali kilimo, *Agricultural Resource Centres*, na ununuzi wa zana za kilimo kama matrekta madogo, *power tillers*, kupitia Halmashauri za Wilaya na pia kutoa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa zana mbalimbali za kilimo kupitia Mfuko wa Pembejeo, *Agricultural Inputs trust Fund. (Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tangia kauli mbiu imeanza ya kilimo kwanza na ninaomba kujua ni vijiji vingapi vya mkoa wa Kagera vilivyofaidika na Kilimo Kwanza na zana hizi alizozitamka Mheshimiwa Waziri na kulingana na zana ya MKUKUTA wa kilimo. (*Makofi*)

Hivi jana tulipitisha maamuzi ya soko la pamoja, wakulima wengi hawana zana za kisasa na ndiyo tunaowategemea wapeleke mazao yao kwenye soko la pamoja, ninavyoona wakulima wetu na wananchi wetu walio maskini ndiyo watakuwa wabeba mizigo wa nchi jirani tutakaojumuika nao katika soko la pamoja. Je, Serikali inawasaidiaje wananchi wetu na wenyewe wafaidike na hilo soko la pamoja? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, ameuliza kwamba ni vijiji vingapi ambavyo vimefaidika na kilimo kwanza, ni vijiji vyote vya mkoa wa Kagera vimefaidika na Kilimo Kwanza kwa sababu Kilimo Kwanza kinasisitizwa na Serikali na Halmashauri za Wilaya ambazo vijiji hivi viko chini ya Halmashauri za wilaya hizo na fedha zimekuwa zinatengwa za *DADPs* kwa wilaya zote Tanzania. Kwa hiyo, nina imani kabisa msisitizo wa Serikali katika kilimo kwanza umefika katika vijiji vyote vya mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zana za kilimo kama nilivyosema kwamba *DADPs* ndiyo program ambayo sasa hivi tunaiendeleza hakuna *project* au miradi midogo ambayo inatusaidia katika kilimo ni *DADPs* peke yake. Lakini pamoja na *DADPs* tunayo mifuko, kwa mfano mfuko wa pembejeo ambapo wananchi mbalimbali wanakopa na sasa hivi tumeanzisha hiyo benki ya rasilimali ambapo tumetenga bilioni 22 kwa hiyo, wananchi wanaweza wakaenda wakakopa zana za kilimo ili kuendeleza kilimo kwanza na mikopo mingine ambayo tunaweza tukapata kwa wafanyabiashara binafsi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona kwa kuwa mojawapo ya hatua za kuboresha kilimo zaidi katika Kanda ya Ziwa kwa mara ya kwanza ni kutoa ruzuku kwa pembejeo. Lakini kwa upande wa pamba pamekuwa na matatizo makubwa sana juu ya bei ambayo Serikali imekubali na bei ambayo wakulima walikuwa wanapata na wengine kuchukua vocha na kuzifanyia biashara.

Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba watu wanaofanya mambo hayo wanapelekwa kwenye vyombo vinavyohusika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali yetu inajali wananchi na wakulima wake kama inavyopeleka vocha na pembejeo mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza kilimo katika mazao ya chakula pamoja na mazao ya biashara. Na nakumbuka Mheshimiwa Cheyo anakumbuka kwamba zao la pamba lilipatiwa fedha kwa ajili ya madawa yaani ruzuku ya madawa yaani imesaidia sana katika uongezekaji wa uzalishaji wa zao la pamba.

Lakini nije katika suala la wafanyakazi ama watendaji kusema kweli wanazembea katika kusimamia zoezi hili la kutoa pembejeo nadhani Mheshimiwa Cheyo wewe ni shahidi kwamba juzi juzi hapa Mkuu wa Wilaya mmoja amefukuzwa kazi kwa sababu ya kuzembea usimamizi wa *vocha system.* Kwa hiyo, nikuhakikishie kabisa kwamba Serikali hii kuanzia juu mpaka chini ina wawakilisha wananchi. Aidha inafanya kazi vizuri na ndiyo maana yule *DC* akafahamika kwamba hakusimamia kazi yake vizuri. Kwa hiyo, zoezi hilo linaendelea kwa wazembe wote ambao watakuwa wamezembea kwa hela ya Serikali inayotolewa kwa ajili ya kusaidia ruzuku kwa wakulima ili waweze kuchukuliwa hatua zinazostahili.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. *Power Tiller* ni mashine ndogo sana kwa kilimo, lakini wananchi wetu wengi walikuwa wamezoe maksai.

Je, kwa nini Serikali inajiingiza kwenye ununuzi wa *Power Tillers* badala ya kuhimiza na kushauri wananchi waendelee kutumia maksai ambayo gharama yake ni kumlisha tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inahimiza matumizi yote ya *Power Tillers,* Matrekta makubwa pamoja na maksai. Kwa taarifa yako ni kwamba mpaka sasa ni asilimia 10 tu ndiyo wananchi wanaotumia matrekta. Wakulima wa Tanzania asilimia 20 tu ndiyo wanaotumia maksai na asilimia 70 ndiyo wanaotumia jembe la mkono. Kwa hiyo, Serikali tunahimiza vyote lakini hatuwezi tukasema kwamba tutaachia maksai peke yake, kwa sababu ni ukweli usipingika kwamba mavuno utakayoyapata kutokana na kilimo cha maksai ni machache ukilinganisha na mavuno utakayopata kutokana na kutumia P*ower Tillers*. *(Makofi)*

Na. 70

## Kupotea kwa mapato ya Nchi

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, imethibitika kwamba mapato yetu ya ndani yanavuja mno kupitia mianya mingi sana na hivyo kulipotezea Taifa letu mapato mengi mno yanayosababisha umasikini usio wa lazima:-

(a) Je, serikali inalifahamu tatizo hilo?
(b) Kama Serikali inafahamu tatizo hilo. Je, ni hatua gani inachukua kukabiliana nalo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa inalitambua tatizo la kuwepo kwa mianya ya uvunjaji wa Mapato ya Serikali. Hali hii inatokana na mapungufu yaliyopo katika taratibu za kukusanya na kusimamia Mapato ya Serikali pamoja na uelewa mdogo wa nchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa tatizo hilo lakini kwa kiwango imefanyiwa kazi na utekelezaji wake umeanza kuonekana. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua na itaendelea kuchukua hatua mbalimbali, ambazo kwa sehemu kubwa zitasaidia katika kupunguza uvujaji wa mapato. Miongoni mwa hatua hizo ni:-

(i) Kuzifanyia marekebisho mara kwa mara sheria kanuni za kodi na viwango vya kodi na ada mbalimbali.

(ii) Kuwatembelea walipa kodi ili kutambua kiwango halisi cha kodi anachostahili kulipia na kile alicholipa.

(iii) Kwa kushirikiana na Kamati ya kodi ya wilaya. Tumeendelea kusajili wafanyabiashara ambao wanastahili kusajiliwa kwa mujibu wa sheria na hatimaye kuanza kulipa kodi.

(iv) Kuimarisha usimamizi wa kodi unaozingatia misingi ya viashiria vya uvujaji wa mapato.

(v) Kufanya tathimini mpya ambayo itatusaidia kutambua vyanzo vyote vya mapato yasiyo ya kodi na ukubwa wake.

(vi) Kuanzisha utaratibu wa kulipia kodi kupitia benki.
(vii) Kuimarisha elimu na huduma kwa walipa kodi pamoja na utoaji wa *receipt.*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi na nyingine kwa kiwango kikubwa zimetusaidia sana kuongeza mapato ya Serikali. Ni matarajio yetu kuwa Waheshimiwa Wabunge mtaendelea kuisaidiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba kodi na ada zinalipwa kwa wakati na kwa ukamilifu. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa jinsi anavyotujibu maswali vizuri. Naomba nimpe maswali mawili madogo mepesi mepesi tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimeshukuru kwamba Serikali imekubali lakini katika mwanya mkubwa ambao unalisababishia taifa kupoteza mapato ya ndani ni mahali panapoitwa bandari. Je, Serikali ina mkakati gani usio wa kinadharia wa kuboresha bandari zetu pamoja na utaratibu wa kukusanya mapato yetu kupitia kwenye bandari.

Mheshimiwa Spika, tulipoanzisha uwekezaji, nia yetu ilikuwa ni kwamba mwekezaji apate lakini pia na taifa letu lipate. Lakini kuna utaratibu mmoja wa wawekezaji hasa wa mahoteli makubwa anawekeza katika hoteli ana-*enjoy* miaka mitano ya *Tax Holiday*. Akishamaliza hapo anampatia mwenzie ile Hoteli na mwenzie anaendelea ku-*enjoy* miaka mitano ya *Tax Holiday,* hivyo taifa kupoteza mapato makubwa ya ndani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuirudisha hii sheria ya Uwekezaji *Under Certificate of Agency* ili sisi Bunge tuweze kuuziba huu mwanya mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA FEHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikushukuru sana kwa pongeza zako na nitaendelea kujitahidi kujibu maswali kwa ufasaha kabisa ili Waheshimiwa Wabunge waweze kunifahamu na wananchi wote kwa ujumla.

Kuhusiana na kuboresha bandari ya Dar es Salaam, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Anne Killango Malecela, kwamba juhudi zinafanywa ili mapato ya Serikali yasiweze kupotea kwanza tunaimarisha kitengo cha kutathimini. Tumegundua kwamba baadhi ya mawakala wanaleta mizigo ambayo thamani yao wamaishusha. Kwa hiyo, tunataka kukiimarisha kile kitengo cha kutathimini ili waweze kutathimini uhalali wa bei wa ile mizigo ili kodi halali iweze kutozwa. Lakini la pili tunataka kuimarisha kitengo cha kufuatilia haya makontena ambayo yanakwenda katika *Inland* kontena *terminal* ili

tuhakikishe kwamba kontena hili linakwenda pale kwa dhamira iliyokusudiwa lisiweze kutoka nje hatimaye likiwa linatoka nje basi mzigo ule uweze kulipiwa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunataka kuongeza *scanner* katika bandari ya Dar es Salaam ili mizigo yote tuweze kui-*scan* na kuelewa kilichomo ndani na kodi halali iweze kulipwa na mambo mengineyo ambayo Mheshimiwa Mbunge nitamwomba baadaye tuweze kuonana tuweze kumpa mambo ni mengi.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme kwamba moja ya *tax intensive* ni kuhakikisha kwamba mwekezaji anatakiwa *Tax Holidays* lakini nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hii *Tax Holiday* baadhi ya wawekezaji wanai-*mis use*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitarudi Wizarani nitakaa na wenzangu tuifanyie mapitio tuitazame upya hii sheria na kama basi kutakuwa na ulazima basi tuweze kuileta hapa ifanyiwe marekebisho.

**MHE. JANET ZEBEDAYO MBENE:** Mheshimiwa Spika, samahani inanibidi nisome some kwa sababu sijapata kadi.Ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa sekta isiyo rasmi hususan wazalishaji wadogo wadogo na wazalishaji wa kati ni idadi kubwa sana ya wazalishaji wa nchi hii; na kwa kuwa sio wote ambao mpaka sasa hivi wanatambulika rasmi na Serikali.

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu sasa ya kuwa na mkakati wa kutoa huduma endelevu za kuweza kuwainua uwezo wao ili wapate kusajiliwa rasmi na kuweza kutoa mchango wao moja kwa moja katika kuchangia kodi? Je, kuna mkakati wowote wa kutumia....

**SPIKA:** Swali ni moja tu la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Basi samahani Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Janet Z. Mbene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara ya Fedha ni kuhakikisha kwamba, inapata mapato kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Wazo lako ni zuri na sisi tunalifanyia kazi ili hawa wafanyabiashara wadogowadogo waliopo katika hii *formal sector* tuweze kuwainua hatimaye waweze kujulikana wako wapi na tuweze kuwa-*register* ili waweze kusaidia katika kulipa kodi na lengo hilo tunalifanya kupitia mifuko mbalimbali, nadhani tuna swali ambalo tutalijibu kesho au keshokutwa.

Na. 71

**TRA Kutoza Malimbikizo ya Ushuru**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa madhumuni ya *(Road Licence Fee)* ni pamoja na kutafuta mapato ya Serikali kwa magari yanayotembea na kufanya safari kwenye barabara zetu; na kwa kuwa kawaida magari huharibika na kutelekezwa na wenyewe na hatimaye kuja kuuzwa kwa watumiaji wengine:-

Je, Serikali haioni kuwa kutoza malimbikizo ya ushuru wa barabara (*Road Licence Fee*) kwa magari ambayo yalikuwa mabovu na kufufuliwa baada ya miaka kadhaa ni sawa na unyang'anyi na ni kero kubwa kwa wahusika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Vyombo vya Moto za Mwaka 2001, ada ya umiliki wa vyombo vya moto hutozwa kwenye vyombo vyote vya moto vilivyosajiliwa na kumilikiwa nchini. Ada hii hutozwa kila baada ya miezi kumi na mbili katika kipindi chote cha umiliki. Ada hi hutozwa kwa vyombo vinavyotembea na vile vyenye thamani ya kuwa barabarani lakini havitembei kwa muda.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Vyombo vya Moto inatambua kuwa, chombo kinaweza kuharibika na kisifae tena kwa matumizi ya barabarani. Katika hali hii, mmiliki wa chombo atatakiwa kupata Ripoti ya Polisi kuhusu hali ya chombo chake kutofaa kwa matumizi ya barabarani na kuiwasilisha kwa Kamishna wa Kodi za ndani, ambaye atafuta usajili wa chombo husika na hivyo kutolazimika tena kulipa ada hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inawajali sana wananchi wake na utozaji wa ada za magari au kodi yoyote ile iliyopo kwa mujibu wa Sheria, usichukuliwe kama unyang'anyi bali ni kwa maendeleo yetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mlichukulie suala la kodi kama la kitaifa na Serikali iwaelimishe wananchi wetu.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa swali langu linalenga katika vyombo ambavyo havitembei kwa miaka kadhaa lakini bado vinatengenezeka na kurudi barabarani. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikaweka utaratibu wa kuwawezesha wale wenye vyombo hivyo ambavyo vimekaa bila kutengenezwa kwa miaka kadhaa baadaye vikatengenezwa waka-*report* Polisi na baadaye TRA ili wasilipe huo ushuru wa vyombo ambavyo havikutembea barabarani?

(ii) Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba vyombo ambavyo vimechakaa kabisa vinapaswa kutolewa *report* Polisi na baadaye Polisi watoe *report* TRA ili viondolewe kwenye usajili kabisa. Je, kwa utaratibu huo ni wananchi wangapi

ambao wamesharipoti vyombo vyao ama magari yao yamechakaa kabisa kwa hiyo yafutwe kwenye usajili?

**SPIKA:** Swali la pili la nyongeza linahitaji takwimu ambazo isingekuwa haki kwa muda huu kusema Wizara itakuwa inajua vyombo vingapi vimefanyiwa utaratibu huu; kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu hilo la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro kama ifuatavyo:-

Ninataka nieleze kwamba, nilichokieleza katika jibu langu la msingi ni Sheria ya Usajili wa Vyombo vya Moto na ndivyo Sheria inavyosema na Sheria hiyo imetungwa na Bunge hili Tukufu. Mimi kuniambia kwamba, wakaripoti tu halafu wasilipe, nitakuwa ninakwenda kinyume na Sheria iliyotungwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wataona kwamba hii ni hoja, basi tuishauri Serikali iletwe hapa ifanyiwe marekebisho, lakini kama haijafanyiwa marekebisho kinachosemwa ndani ya Sheria ya Vyombo vya Moto ni kwamba, ukikiweka chombo chako lakini kina thamani ya kutembea barabarani hata kama ukikiweka kwa kipindi cha miaka 10 ukija ukikitembeza barabarani utalazimika kulipa kodi ile ya miaka 10 ambayo hujailipa mpaka Sheria hii ifanyiwe marekebisho.

Na. 72

**Kuhusu Malipo ya Bima za Maisha Zilizoiva**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** aliuliza: -

Kwa kuwa Shirika letu ya Bima la Taifa limeshindwa kulipa Bima mbalimbali zilizoiva na kuleta usumbufu mkubwa wa wateja wake:-

(a) Je, ni kwa nini Shirika halikutekeleza wajibu wake Kikatiba?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za haraka kuhakikisha kuwa wateja wa Shirika hilo wanalipwa madai yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pascal C. Degera, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Shirika la Bima la Taifa *(NIC)*, limechelewesha ulipaji wa madai ya Bima mbalimbali zilizoiva kwa baadhi ya wateja

wake. Hali hii imetokana na kupungua kwa biashara ya Shirika kutokana na ushindani wa soko na hivyo kushindwa kupata mapato ya kutosha ambayo yangemudu gharama za uendeshaji pamoja na kulipia madai ya Bima. Hata hivyo, kwa kutumia mapato yaliyopatikana, Shirika limeweza kulipa madai yenye thamani ya shilingi 51.35 bilioni hadi kufikia Disemba, 2008. Aidha, Shirika linaendelea kudaiwa na wateja madai yenye thamani ya shilingi 28 bilioni.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo zitasaidia kuhakikisha kuwa wateja wa Shirika la Bima wanalipwa kwa haraka. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kulifanyia marekebisho Shirika la Bima ili liweze kujiendesha kwa ufanisi. Marekebisho makubwa yaliyofanywa ni kupunguza idadi ya watumishi kutoka 480 hadi 250.

(ii) Serikali imetathmini majengo ya Shirika ambayo hayaambatani na biashara ya Bima ili yaweze kuuzwa kwa lengo la kupata fedha zitakazosaidia kulipia madai ya wateja.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Mbunge avute subira pamoja na kusaidia kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili. Siyo muda mrefu, hatua za ulipaji wa madai zitachukuliwa.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa ahadi ya kutathmini majengo ya Shirika la Bima ya Taifa ni la muda mrefu; napenda Mheshimiwa Naibu Waziri anihakikishie ni lini tatizo litakwisha ili wahusika waweze kulipwa haki zao?

(ii) Kwa kuwa Watumishi wa Wilaya ya Kondoa na hususan Walimu wa Shule za Msingi walihamasika sana kukata Bima za aina mbalimbali; na kwa kuwa hizo Bima zimeiva kwa muda mrefu sasa na wanasumbuka kila leo kuja kufuatilia malipo yao; je, pindi Shirika litakapouza majengo hayo hawa Watumishi wa Wilaya ya Kondoa watapewa kipaumbele kwenye malipo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Degera, kama ifuatavyo:-

Suala la kutathmini majengo limekwisha na hatua zilizobakia sasa hivi ni kuanza kupata pesa na kulipa; kwa hiyo, hilo halipo tena kwani majengo yote yameshatathminiwa.

Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Degera kwamba, tumechukua muda kwa sababu majengo ya Bima yako mengi na yako katika maeneo mengi na tulitaka kuhakikisha kwamba, tathmini tunayoifanya ni halali na inatuwezesha kulipa madeni yaliyopo.

La pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Degera kwamba, Shirika la Bima linadaiwa shilingi bilioni 28 na tathmini ya majengo yaliyojitokeza ni zaidi ya shilingi bilioni 40; kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, fedha ikipatikana wananchi wote wanaoidai Bima pamoja na wale wa Kondoa, watapatiwa fedha yao.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba, madeni yameanza kulipwa kwa wale ambao Bima zao ziliiva na tukumbuke kwamba, wapo wengine ambao walichukua Bima miaka ya nyuma kuanzia miaka ya 80 na wakati huo thamani ya pesa hiyo ilikuwa ni kubwa.

Je, kwa sasa hivi hao wanaolipwa watalipwa kwa kiwango gani wakati miaka ya nyuma haifanani kiwango chake na thamani yake kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nadhani sisi sote ni mashahidi, Bima ni mkataba baina ya muweka Bima na yule anayeweka Bima, kiwango ambacho watakacholipiwa ni kulingana na mkataba ambao waliwekeana.

Kusema hapa kwamba, mkataba ule utaongezwa sasa hivi kwa sababu walipewa zamani au vipi, nadhani nitakuwa ninawaongopea. Shirika la Bima au Serikali kwa ujumla itaangalia mkataba unasema vipi na basi mkataba huo utaheshimiwa.

Na. 73

**Maji ya Mradi wa Ziwa Victoria Kufikishwa Kwimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa maji ya Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama ni mengi sana; na kwa kuwa Mji wa Ngudu Wilaya ya Kwimba una shida kubwa sana ya maji kwa sababu hauna chanzo cha maji cha kudumu:-

(a) Je, Serikali itaisaidiaje Halmashauri ya Kwimba ili sehemu ya maji hayo yafike katika Mji wa Ngudu?

(b) Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa kukamilisha zoezi la usambazaji wa maji ya Mradi huo katika vijiji sabini vikiwemo vijiji kumi na sita vya Tarafa ya Mwamashimba Wilayani Kwimba?

(c) Je, Serikali bado ina mpango wa kujenga tanki la maji na kuliunganisha na Mradi huo ili kurahisisha usambazaji wa maji na utekelezaji wake umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bujibu P. Sakila, Mbunge wa Kwimba, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria ulianza kujengwa mwaka 2004 na ulikamilika na kuzinduliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 30 Mei, 2009.

Mradi huu ulisanifiwa ili kutoa huduma ya maji katika Miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na vijiji 54 ambavyo viko umbali usiozidi kilomita tano kutoka kwenye bomba kuu katika Wilaya za Misungwi, Shinyanga Vijijini na Kahama. Hadi sasa maji yamefika na kusambazwa katika Miji ya Kahama na Shinyanga na katika vijiji 39 vya Wilaya za Misungwi, Shinyanga na Kahama. Katika Wilaya ya Kwimba, Mradi umefikisha maji kwenye tanki la Mhalo ambapo mfumo wa zamani wa usambazaji maji katika Tarafa ya Mwamashimba umeunganishwa. Halmashauri ya Kwimba, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji ya Miji ya Kahama na Shinyanga (KASHWASA), wanaendelea na ukarabati wa bomba la zamani la kupeleka maji hadi Mji Mdogo wa Mwamashimba. Aidha, KASHWASA imefikisha maji katika Kijiji cha Chasalawi na kujenga gati mbili za kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga ulisanifiwa na kutoa maji mita za ujazo 80,000 kwa siku katika awamu ya kwanza ya kutosha mahitaji ya watu 450,000 katika Miji ya Shinyanga na Kahama pamoja na vijiji 54 katika Wilaya za Misungwi, Shinyanga Vijijini, Kahama na Kwimba hadi mwaka 2016.

Awamu ya pili itahusu upanuzi wa mitambo ya Ihelele katika mwaka huo huo wa 2016 ili iwe na uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 100,000 kwa siku na kuhudumia watu zaidi ya milioni moja katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa haomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu, Mradi haukusanifiwa kufikisha maji katika Mji wa Ngudu, Serikali itachunguza uwezekano wa

kutumia maji hayo au kutafuta chanzo mbadala cha maji kwa Mji wa Ngudu ambapo kazi ya usanifu itafanywa chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji. Usanifu huo utafanywa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mwanza ambapo Mji Mdogo wa Ngudu pamoja na Miji Midogo mingine ya Geita, Misungwi, Sengerema, Magu, Nansio na Ukerewe itahusishwa. MWAUWASA inatarajia kusaini mkataba wa usanifu wa mradi na mtaalamu mwelekezi mwezi huu wa Aprili 2010 na kazi ya usanifu inatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2010.

(b) Serikali imeshaanza mchakato wa kumtafuta mtaalamu mwelekezi ambaye atasanifu mifumo ya usambazaji maji katika vijiji 70. Wakati mchakato huo unaendelea, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa Mamlaka ya Maji ya Kahama (KASHWASA) ili iendelee kuviunganishia maji vijiji ambavyo mfumo wake wa maji hauhitaji usanifu mkubwa. Chini ya utaratibu huu, vijiji 40 ambavyo vina tanki la maji na kichoteo kimoja, vitaongezewa vichoteo vya maji, yaani *Kiosks,* vikiwemo vijiji 16 vya Tarafa ya Mwamashimba alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

(c) Ujenzi wa tanki la maji analoulizia Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya kazi ya usanifu itakayofanywa na mtaalamu mwelekezi kama nilivyosema katika sehemu (a) na (b) ya jibu langu.

Mheshimiwa Spika, katika usanifu wa awali, Wilaya ya Kwimba haikuwemo katika Mradi wa Kahama Shinyanga. Napenda kipekee, kumshukuru Mheshimiwa Bujibu Sakila, Mbunge wa Kwimba, kwa juhudi zake binafsi zilizowezesha Wilaya ya Kwimba kufanywa kuwa sehemu ya mradi mzima. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Awali ya yote, napenda niishukuru sana Serikali kwa Mradi huu na hasa Serikali ya Awamu ya Tatu na ya Nne, kwa kukubali kunisikiliza na kupokea ombi hili katika hatua iliyofikia hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo, naomba sasa niulize maswali mawili.

(i) Wilaya ya Kwimba tumeshafanya maombi mawili; kwanza shilingi milioni mia moja sabini na tatu na laki nne ambayo Wizara ilisema kwamba tusubiri tukaomba milioni 51; kimsingi Serikali imekubali kutupatia milioni 51 kupitia KASHWASA. Je, ile fedha ambayo ingepeleka maji hadi katika Kijiji cha Kawekamo na ikiwezekana pia Mliyungu itapelekwa lini KASHWASA?

(ii) Kama nilivyosema kwenye swali la msingi, maji ya mradi huo ni mengi sana; Ngudu iko kilomita 70 kutoka kwenye tanki la maji ambalo tumelisema katika swali na kilomita 35 kutoka Luneli; kuungaisha Ngudu katika mradi huo wananchi wa Buyogo, Bungumalo, Buneda, Idula na Milama pamoja na Mobogola na Maiga wote watanufaika na mradi huu; kwa nini sasa yule mtaalamu mwelekezi anayesemwa katika jibu asichangiwe atumie nguvu zake nyingi sana kuangalia uwezekano huu badala ya kuangalia uwezekano mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda nipokee shukrani za Mheshimiwa Mbunge, lakini pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha ambazo Wizara iliahidi zitapelekwa, tunachosubiri tu ni fedha kutoka Hazina na ninaamini kabisa fedha zikishapatikana zitapelekwa mara moja; sitaki kumwambia ni wiki hii lakini tukitoka hapa tutajaribu kufuatilia Wizarani na Hazina tujue fedha hizi zitatoka lini. Nina hakika zitakapopatikana fedha hizi tulizoahidiwa zitapelekwa.

La pili, kuhusu Mradi wa Ngudu kutumia maji ya Kahama Shinyanga, naomba niseme tu kwamba, jana wakati Mheshimiwa Waziri akitoa majibu ya nyongeza akielezea maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais alitupa kwa ajili ya kufikisha maji haya katika Mji wa Tabora alisema, Serikali au Wizara inaangalia uwezekano wa maji hayo kufikishwa kule Tabora. Vivyo hivyo hata kwa Ngudu, kwa kuwa mradi huu haukupangwa kupeleka maji Ngudu, tutakachofanya ni kuangalia uwezekano wa hadidu za rejea za Mhandisi anayefanya usanifu huu kuona kama inawezekana kuyafikisha maji haya Ngudu kitaalamu.

Endapo haitawezekana, kazi atakayofanya mtaalamu huyu si tu kuachia hapo, yeye atatafuta chanzo mbadala ambacho kitakidhi kwa hakika mahitaji ya Mji wa Ngudu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, anachokifanya huyu mtaalamu mwelekezi ni kuhakikisha chanzo cha maji ya kukidhi mahitaji ya Ngudu kinapatikana. Kama itakuwa ni Shinyanga basi itakuwa ni hayo.

Na. 74

**Hitaji la Mabomba Mradi wa Maji Mererani**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Mererani una mradi mmoja wa Maji ya Kisima kirefu uliogharamiwa na Shirika la World Vision, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro pamoja na Wananchi na umeanza kutoa huduma lakini unahitaji kuongezewa mtandao wa mabomba ili kutoa huduma bora:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ununuzi wa mabomba hayo ili kufanikisha lengo la mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali inajua tatizo la huduma ya maji isiyokidhi mahitaji katika Mji Mdogo wa Mererani, ambao wakazi wake wengi ni wachimbaji wadogo wa madini. Ili kupunguza

tatizo, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kukarabati mfumo wa maji wa Mji wa Mererani.

Napenda nitumie fursa hii, kuwashukuru wadau wote wanaoshirikiana na Serikali kutoa huduma ya maji katika Mji huo wa Mererani. Kipekee, napenda kulishukuru Shirika la World Vision kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Mji wa Mererani na mahali pengine katika nchi hii ili kutatua tatizo sugu la upatikanaji wa maji katika Mji Mdogo wa Mererani.

Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, kuangalia uwezekano wa kuingiza Mji Mdogo wa Mererani katika *cluster* ya Babati ili Mji huu nao ushughulikiwe kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi yakinifu.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kabla ya hapo na mimi ningechukua nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wa Mererani, kutoa shukrani zetu za pekee kabisa kwa Mashirika yaliyosaidia kuugharamia Mradi huu kwa mtandao wa mabomba yenye urefu wa kilomita 2.4, ambapo wananchi wachache sasa wanapata huduma hii ya maji. Mashirika hayo ni pamoja na World Vision Tanzania na Wizara ya Nishati na Madini, Halmashauri ya Wilaya Simanjiro pamoja na Wananchi wa Mererani.

Kwa kuwa Mradi huu una uwezo wa kutoa maji lita 68,000 kwa saa na pia unaweza kutoa huduma kwa wananchi 51,000; na kwa kuwa ili Mradi huu uweze kukamilika yanahitajika mabomba yenye urefu wa kilomita 12.4 yenye thamani ya shilingi 515 milioni ili Wananchi hawa wa Mererani waweze kupatiwa huduma hii ya maji; je, kutokana na jitihada zote zilizofanyika kwa wananchi hawa Serikali haioni umuhimu wa kusaidia mtandao huu wa mabomba ili Wananchi wa Mererani waweze kunufaika na matunda ya Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi?

**SPIKA:** Swali la nyongeza refu sana, natumaini Mheshimiwa Naibu Waziri utajibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, tunafahamu kuwa Mji wa Mererani umeshatangazwa kuwa Mji Mdogo na ndiyo maana nimethubutu kusema sasa tutauingiza katika Programu yetu ya Mji Midogo ili uweze kuhudumiwa. Naomba tu sasa atambue hilo kwamba, kwa kuwa Mji umekuwa Mji Mdogo na tumeuingiza katika Programu ya Kuhudumia Miji Midogo, Mji huo nao utahudumiwa.

Na. 75

**Changamoto Zinazoikabili Idara ya Polisi**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Polisi inapaswa kutoa huduma kwa haraka na kwa ufasaha:-

(a) Je, ni muda gani hutumika kuandikisha ripoti ya ajali mwananchi anapopata ajali na kutoa taarifa?

(b) Je, ni changamoto zipi zinazoikabili Idara hii ya Polisi hususan upande wa Watumishi wa Polisi, vitendea kazi pamoja na uwezo wa kufanya kazi kitaaluma?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha Idara hii muhimu ya Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida hakuna muda maalum uliotengwa kwa ajili ya kuandikisha ripoti ya ajali mwananchi anapopata ajali na kutoa taarifa Polisi. Taarifa ya ajali inaporipotiwa na mwananchi yeyote kwa kuona au kupiga simu, inatakiwa kushughulikiwa na kufanyiwa kazi mara moja ikiwa ni pamoja na kufungua jalada husika la ajali hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Idara ya Polisi hazina tofauti sana na changamoto zinazozikabili Idara nyingine za Serikali. Changamoto hizi ni pamoja na uchache wa vitendea kazi kama magari ya doria; pikipiki za doria; vipima ulevi; upungufu wa ofisi; na mafunzo kwa Maafisa na Askari.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali bado inajitahidi kukabiliana na changamoto hizi kwa awamu ili hatimaye Askari wetu wa Jeshi la Polisi watekeleze majukumu yao katika kiwango na ufanisi unaotakiwa ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kitaalamu zaidi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango mahususi wa kuboresha Jeshi la Polisi kulingana na uchumi wa nchi unavyokua. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maslahi na vitendea kazi kwa Askari vitaboreka awamu kwa awamu kulingana na kukua kwa uchumi wa Taifa letu.

Na. 76

**Vyeti vya Matokeo ya Mitihani Kuwa na Picha**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya vyeti vya matokeo ya Mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha Nne na Sita kutoka NECTA vinatumiwa na watu wengine wasio watahiniwa kwa ajili ya kutafuta ajira au nafasi za masomo ya juu:-

Je, kwa nini vyeti hivi visiwekwe picha ya mtahiniwa husika kwa kutumia kompyuta ili kuondoa udanganyifu huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu wamebainika kutumia vyeti vya matokeo ya Mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha Nne na Sita visivyokuwa vyao kwa ajili ya kutafuta ajira au nafasi za masomo ya juu, jambo ambalo ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti udanganyifu huu, Baraza la Mitihani la Tanzania limeanza kuweka picha katika vyeti vya matokeo ili kuwawezesha wadau kumtambua mmiliki halali wa cheti. Picha hizo huwekwa kwa kompyuta hivyo haziwezi kuondolewa. Zoezi la kuweka picha katika vyeti litaanza na vyeti vya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2008, ambavyo vitachapwa mwezi Mei, 2010. Aidha, hati za matokeo (*Result Slips*) ya Mitihani ya Kidato cha Nne 2009 zimetolewa zikiwa na picha kwa nakala ambayo nimeileta, hii hapa kama kuna Mbunge atataka kuiona namkaribisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa wananchi wote kuacha mtindo wa kutumia vyeti visivyokuwa vyao, kwani kufanya hivyo, tunawanyima haki wenye vyeti stahili na hivyo ni kutenda kosa la jinai.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya watu ambao siyo waaminifu wanatumia vyeti vya watu wengine kwa makubaliano na wenye vyeti wenyewe. Je, Serikali itachukua hatua gani kwa wenye vyeti hivyo ili kuikomesha kabisa tabia hii ya kuazimana vyeti?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, taarifa za watu wanaouza vyeti vyao ni chache sana na bado hatujapata zenye uthibitisho. Taarifa zilizotolewa kwa wingi ni vyeti kuibwa, vyeti kuuzwa na kesi nyingi tumeshaziwasilisha Polisi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa kusitisha maswali umekwisha, lakini mtakumbuka leo kumekuwa na matangazo; kwanza, hati za kuwasilishwa mezani zilikuwa nyingi, baada ya hapo tukamtangaza mgeni wetu mashuhuri tukachukua muda, kwa hiyo tutayamaliza haya.

Na. 77

## Hospitali ya Mkula Kuwa Hospitali Teule

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Mkula inayomilikiwa na Kanisa la African Inland Church Tanzania (AICT) iliyojengwa miaka 1983/84 inahudumia wananchi wengi wa maeneo ya Mikoa ya Mwanza, Mara na Shinyanga na ndiyo Hospitali pekee iliyo mbali na Makao Makuu ya Wilaya ya Magu licha ya kuwa ina uwezo mkubwa wa kutoa tiba na huduma za afya kwa wananchi:-

Je, isingekuwa busara kwa Serikali kuiteua Hospitali hii iwe Teule *(DHH)* ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na kwa kuzingatia kupata msaada wa Serikali kama ambavyo hospitali za aina hii zinapata?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mwongozo wa utoaji wa huduma ya afya nchini, kila Wilaya inatakiwa kuwa na Hospitali moja tu ya Wilaya. Kwa sasa Wilaya ya Magu tayari ina Hospitali ya Wilaya ya Serikali kama mwongozo unavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwongozo huo na kuzingatia mahitaji ya vituo vya huduma za afya zikiwemo Hospitali za Wilaya katika maeneo mengine nchini, tunaamini haitakuwa vyema kwa wakati huu kuwa na hospitali mbili za Wilaya katika Wilaya moja ya Magu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, hospitali hiyo inatoa huduma kwa wananchi wengi, ningependa kumshauri awasiliane na Halmashauri ya Wilaya yake ili kuona uwezekano wa kuingia makubaliano *(Service Agreement)* na Hospitali ya Mkula ili itoe huduma kwa niaba ya Halmashauri. Hii itawezesha wananchi kupata huduma kwa gharama nafuu katika hospitali hiyo.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kumuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mwongozo umebainisha wazi kwamba akinamama na watoto wanapaswa kupata huduma bure lakini kwa sababu hospitali hii ni ya Taasisi Binafsi na inatoza gharama kwa akinamama na watoto; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba ni vyema sasa angetoa maelekezo juu ya mwongozo ili Halmashauri ya Wilaya ya Magu iweze kuingia makubaliano rasmi na hospitali hii ili iweze kutoa huduma na kuboresha tiba kwa Wananchi wa Wilaya ya Magu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, sera inasema watoto na wajawazito watibiwe bure katika Hospitali za Serikali. Kwa maana kwamba, wanapokwenda kutibiwa katika hospitali ambazo siyo za Serikali inabidi kulipa, kwa hiyo inakuwa ni kinyume na sera yetu ya afya.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Halmashauri husika inatakiwa kukaa na Mwanasheria wake ili iweze kuangalia katika yale maeneo ambayo wanaona wanaweza wakaandikishiana mkataba na Hospitali ya Mishenari au ya Dini. Vile vile hospitali yenyewe inatakiwa iangalie Mkataba wa Huduma ili kuweza kuona eneo ambalo wanaweza kushirikiana kutoa huduma na kubeba gharama. Kwa maana hiyo, ningependa kuchukua nafasi hii kumkumbusha au kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu akae na wataalam wake pamoja na Mwanasheria, wapitishe katika Huduma ya Mkataba ili waweze kuona kwamba wanaangalia upande ule wa huduma za mama na mtoto ambazo zinatolewa na Mwanasheria wa upande wa hospitali ukae na Mwanasheria wake wakubaliane katika eneo hilo ili waweze kutoa hii huduma bure na gharama zile zibebwe na Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

Kwa sababu hiyo hiyo, fedha watakayokuwa wanaipata Hospitali ya Mkula pamoja na fedha ambayo inatolewa na Serikali ya *bed grant* na nyingine katika Mfuko wa *Basket Fund,* wanaweza wakaitumia kuchangia gharama inayotolewa katika Hospitali ya Mkula.

Na. 78

**Hitaji la Mashine za *Oxygen* Hospitali ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou-Toure**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou-Toure ina mashine moja tu ya *oxygen*:-

Je, ni lini Serikali itaongeza mashine hizo ili zikidhi mahitaji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Sekou-Toure ambayo ni ya Mkoa wa Mwanza, ilikuwa na mashine nne za *oxygen.* Kati ya hizo; mbili hazifanyi kazi na hazitengenezeki. Zilizobaki mbili, moja imewekwa katika chumba cha upasuaji na nyingine iko katika chumba cha wagonjwa mahututi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kulingana na mahitaji mashine hizi hazitoshelezi. Jukumu la kuagiza vifaa vya hospitali, ikiwa ni pamoja na mashine za *oxygen* ni la uongozi wa hospitali husika kupitia Bohari ya Madawa.

Mheshimiwa Spika, fedha za dawa, vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali zote za Serikali hupelekwa Bohari ya Dawa kulingana na mgao kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa fedha ni kikwazo kikubwa katika kutosheleza mahitaji na vifaa tiba vinavyohitajika katika kutoa huduma za afya. Kwa kuzingatia umuhimu wa mashine hizi katika kuokoa maisha, Uongozi wa Hospitali hiyo umeelekezwa kutumia mgao wa fedha za vifaa unaopelekwa Bohari ya Dawa kununua mashine moja ya *oxygen* na pia Katibu Tawala wa Mkoa ameagizwa kuangalia uwezekano wa kutumia fedha hizo za matumizi ya kawaida kwa miezi michache iliyobaki ya mwaka wa fedha 2009/2010, kununua mashine nyingine ili kuwezesha hospitali hiyo kuendelea kutoa huduma.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Hospitali hii ya Mkoa wa Mwanza Sekou-Toure ni ya siku nyingi sana na OC anayoisema Mheshimiwa Waziri ni kidogo sana iliyobakia. Je, ni lini sasa Hospitali hii itafanyiwa matengenezo ya kudumu ili iweze kuonekana ni Hospitali ya Mkoa?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba kuna upungufu wa vifaa katika hospitali nyingi za hapa nchini kwetu na miundombinu ni mibaya sana katika hospitali zetu. Je, Serikali haioni umuhimu badala ya kupeleka wagonjwa nchi za nje ikakarabati hospitali zetu zilizoko nchini ili ziweze kuhudumia wananchi wengi wa kipato cha chini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Sekou-Toure kweli ni ya zamani na mimi naifahamu kwa sababu kwanza ilianza kama Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, kwa yeyote anayeifahamu Mwanza, hali ya Sekou-Toure siyo kama ilivyokuwa. Serikali kwa kushirikiana na Serikali Kuu pamoja na Mkoa wa Mwanza, Hospitali ya Sekou-Toure imekuwa ikikarabatiwa siku hadi siku na sasa hivi unakuta majengo mengi yamebadilika na kwamba vitu vingi sana vimebadilika. Kwa hiyo, si kweli kwamba ile Hospsitali haikarabatiwi; inakarabatiwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, kama tulivyosema katika Mpango wetu wa MAM ni kwamba, tunataka tutengeneze hospitali ambayo itakuwa ya rufaa katika kila Mkoa. Kwa hiyo, ni wazi kwamba katika mpango huo, tutahakikisha kwamba, Hospitali ya Mkoa wa Mwanza aidha itajengwa nyingine au tutaendelea kuipanua ili huduma zake ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa vifaa na miundombinu, Mheshimiwa Mbunge naona anaendelea kuzungumzia kuhusu suala la kupeleka wagonjwa nje. Kama tunavyofahamu, tumeboresha maeneo mengi na huduma nyingine za wagonjwa wanaopelekwa nje kwa mfano upasuaji wa moyo sasa hivi zimeanza pale Muhimbili. Vile vile Hospitali ya Mwanza ni mojawapo ya hospitali ambayo tunaifanyia mpango wa kuiboresha ili hata wale wagonjwa ambao wanapata huduma za saratani na ugonjwa wa moyo, waweze kutibiwa kule Mwanza. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba, Mheshimiwa Mbunge avute subira, mipango yetu ni mizuri hatimaye hata operesheni tutazifanyia kule Mwanza, ambapo tutashirikiana na hospitali nyingine kama vile KCMC na nyinginezo ambazo tutaziboresha. Ahsante sana.

Na. 79

**Utumiaji wa *Uranium* Kuzalisha Nishati Nchini**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna uwezekano wa mkubwa kuwepo kwa *Uranium* hapa nchini ambayo ni chanzo cha kisasa cha nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia *Uranium* katika kuzalisha nishati?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni aina ya madini ambayo yakichenjuliwa hutumika katika masuala mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuzalisha umeme, tiba ya mionzi, uchunguzi wa *X-Ray*, kuhifadhi chakula, kuua wadudu waharibifu wa mazao, utafiti viwandani na kutengenezea silaha. Tanzania ina mategemeo ya kuwa na migodi ya *uranium* kuanzia mwaka 2012. Mpaka sasa maeneo ya Kati ya nchi yetu hususan Wilaya za Manyoni na Bahi, pamoja na maeneo ya Kusini ya nchi yetu yakiwemo Namtumbo, Liwale, Tunduru na Songea, yamevutia utafutaji wa madini ya *uranium*.

Makampuni makubwa matatu yanafanya utafutaji wa madini ya *uranium* na yamefikia hatua za juu za utafutaji yakiwa kwenye hatua za upembuzi yakinifu wa awali. Makampuni hayo ni Mantra Tanzania Ltd., Uranex Tanzania Ltd. na Western Metals Tanzania Ltd. Teknolojia ya kuzalisha umeme kutokana na *uranium* kama chanzo cha nishati, imekuwa inatumiwa na nchi nyingi tangu mwaka 1958, ambapo Uingereza imekuwa ni nchi ya kwanza duniani kutumia chanzo hicho kwa ajili ya kuzalishia umeme.

Mheshimiwa Spika, taaluma hii ni teknolojia ya gharama kubwa ya uendeshaji wa matunzo na ukarabati wa vinu vya nyuklia *(Nuclear Reactor)* pamoja na teknolojia ya kurutubisha *uranium (Uranium Enrichment)* ili kuifikisha kwenye kiwango cha

kuwezesha kutumika kuzalisha umeme. Kama ilivyo kwa sayansi na teknolojia zote, kipindi hiki cha miaka 50 tangu mwaka 1958, kimeleta mabadiliko na maendeleo ya teknolojia ambayo yamepunguza gharama za uendeshaji na uzalishaji wa nishati unaotokana na *uranium*. Hivyo basi, mabadiliko hayo yamepanua wigo na pia kuongeza uwezo wa nchi zinazoendelea kama ya kwetu, kufanya uwekezaji wa kuzalisha umeme unaotokana na *uranium*.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo hapo juu, utafiti huu, upembuzi yakinifu na hatua za awali za migodi, zinakwenda sambamba na hatua za kuandaa na kukamilisha taratibu. Punde uchimbaji wa madini hayo utakapoanza na miongozo ya madini haya utakapoanza na miongozo ya matumizi ya madini hayo kukamilika; Serikali itafanya jitihada kuhakikisha madini hayo yanatumika kuzalishia umeme na matumizi mengine kama yalivyoelezwa hapo juu.

Pamoja na hayo, Shirika la Umeme TANESCO, nalo linafuatilia kwa karibu maendeleo ya utafiti wa madini hayo nchini na utekelezaji wa hatua zinazofuata za kuanza kwa miradi hii ili kubaini uwezekano wa utekelezaji wa mpango huu wa uzalishaji umeme unaotokana na *uranium* kwa kiwango, muda na mchakato muafaka ili kuingiza kama sehemu ya mikakati ya Mpango Kabambe wa Sekta ya Umeme *(Power Sector Master Plan).*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli itakuwa neema kama *uranium* itatumika kama njia mbadala ya kuzalisha umeme lakini kelele za Watanzania ni kwamba hawajawahi kufaidi madini ya Tanzania. Njia ambayo nafikiri Serikali ingeitumia kama mwekezaji atakayewekeza kwenye *uranium* atapewa mkataba ambao ataambiwa ajenge vinu vya kuzalisha *uranium* ili watu waone faida ya huo uwekezaji badala ya kulipa fedha za Serikali. Mpango kama huu unatumika kule Congo na wameweza kuleta maendeleo makubwa kujenga barabara na reli badala ya kulipa pesa ambazo hazionekani.

Kwa kuwa *uranium* ni madini yenye hatari kubwa kwa binadamu; kwa nini vinu vya kuzalisha umeme visijengwe pale pale panapopatikana *uranium* ili iweze kudhibitiwa pale inapozalishwa na viwanda vinapojengwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niseme kwamba, *uranium* kama inavyotoka ardhini ni udongo. Sasa kuna *process* zinazofanywa pale ili kuitoa kwenye hatua mbalimbali kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Ndiyo maana kwenye majibu nimesema ukishaitoa pale kuna *process* ambayo inatarajia iishie pale ya kutengeneza kitu kinachoitwa *yellow cake.* Ile *yellow cake* inawekwa kwenye madumu maalum halafu inasafirishwa kwenda kwenye viwanda ambavyo vinafanya *uranium enrichment* kwenda kwenye hatua za awali, ambapo inaweza ikatumia *nuclear fuel* au kwenda kwenye hatua ya zaida, ambako Mheshimiwa Ndesamburo kama unavyojua, kuna migogoro ya kimataifa kuhusu baadhi ya nchi

wanazomiliki hizi *nuclear fuel,* lakini wanakusudia kuzipeleka kwenye ngazi ya juu ambayo inaweza ikatumika kutengenezea silaha.

Hizi ni hatua za *industrial development* ya hii *uranium* yenyewe. Sisi kama Tanzania, wawekezaji wetu wataishia kwenye ngazi ya kutengeneza *yellow cake*. Ndiyo maana nasema kwa sababu *uranium* yenyewe inatoka Tanzania, tunaweza kupata uwekezaji wa makusudi ambao tunatarajia ushirikishe Serikali ya Tanzania ili kuitoa pale sasa kuingia kwenye *nuclear fuel,* matengenezo ya umeme na *nuclear reactors* na kadhalika. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwenye jibu la swali la msingi, hatutofautiani sana na swali la Mzee Ndesamburo, isipokuwa nasema wanaofanya kazi hii sasa hivi ni wale wanaofanya kazi katika *level* ya hatua ya madini yale kuwa madini. Sasa inapotoka pale kwenda kuwa nishati, hiyo ni hatua nyingine ya maendeleo ya madini hayo.

Hili la pili ni kwamba, *uranium* kama ilivyo, inapotoka pale chini kwenye ardhi ni madini ambayo unayashika kwa mkono unanawa kwa sabuni unaendelea na shughuli zako. Ni pale yanapopelekwa kwenye hatua ile ya *enriched* ndiyo sasa yanapokuwa madini hatari. Kusema kweli katika hatua hiyo hutarajii kwamba, mtu yeyote atayashika.

Kwa hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa hivi tunaendelea na utaratibu wa kutengeneza taratibu na miongozo kwa kushirikiana na Wakala wa Atomic ambao wako Arusha ili kutengeneza taratibu na miongozo hapo tutakapofikia hatua ya kuwa na *uranium* yenyewe mwaka 2012 tuwe na miongozo na kushika na kumiliki madini haya kwa hatua hiyo yakishachenjuliwa kwa njia zilizo salama kwa watumiaji wote.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali ulikwishapita na maswali yamekwisha. Matangazo; tunaanza na wageni. Kwenye *Speaker's Gallery* tunaye Naibu Balozi wa Uingereza hapa nchini, Mheshimiwa Susie Kitchens, nadhani yule pale. *It is a pleasure to receive you here in Dodoma. We have excellent relations and in fact that you are here, is another attestation of that fact. Please, convey our best regards to Her Excellency The High Commissioner. (Makofi)*

Mgeni wa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe; Ndugu Kassim Abdallah Mweka Hazina wa CCM Wilaya ya Nachingwea; yule pale karibu sana.

Mheshimiwa Mdhibiti na MKaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Ludovick Utouh, amefuatana na Maofisa Waandamizi wa Ofisi yake na kutoka Hazina. Kwenye ujumbe huo pia yupo Mwakilishi wa SIDA (Sweden), Ndugu Viveca Ho. Naomba wasimame.

Wapo wageni wa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya ni wawekezaji wa Sekta ya Mifugo Dar es Salaam. Kampuni inaitwa Twiga Feed Ltd. wanaongozwa na Dr. Herman Moshi na Ndugu Gren Moshi; karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Sevelina Mwijage kama ifuatavyo: Mheshimiwa Pilly Kabusinzi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake na Diwani wa Viti Maalum Geita; Elias Mtoni, Mkurugenzi wa Siasa CUF Wilaya ya Geita; Ndugu Saidi Zuberi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Kata ya Nkome; Ndugu Bertha Elias, Katibu wa Jumuiya ya Wanawake Kata ya Nkome; Ndugu Anna Peter, Mjumbe wa Serikali ya Kijiji Ihumula wa Chama cha CUF. Wale pale; karibuni sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Savelina Mwijage, ambao ni wanae Gervazi na Edison. Wale pale; ahsante sana.

Wageni wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini ni Wawakilishi waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda cha Mutex Musoma, ambao ni Ndugu Pundo Josephat, Maengera Mashana na Sospeter Mtesigwa. Wale pale; ahsanteni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ni Mheshimiwa Yuster Kinyaga, Diwani wa Viti Maalum Iringa; yule pale karibu sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Manju Msambya, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Kaparamsenga, Ndugu Frank Lawi Erasto; yule pale karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Herbert Mntangi, ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake kutoka Kata za Masuguru, Kigombe, Mtindiro na Kilulu, Jimbo la Muheza; wale pale karibuni sana.

Kama kawaida huwa nawakumbusha watu wa Muheza; sijui mmekuja na machungwa au mmekuja hivi hivi?

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Cap. John Komba ni mlezi wa Kikundi cha Utamaduni cha CCM kiitwacho Mapambano kutoka Maili Moja Kibaha, wanaongozwa na Sebastian Maganga, Kiongozi wa Kikundi; yule pale; Ndugu Katherine Makungwa ni mwenyeji; Ndugu Leah Kasiga, Kiongozi wa Nidhamu. Hawa wamejipanga vizuri kweli; karibuni sana kutoka Kibaha.

Mgeni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila ni Ndugu Samson Kisinza, ambaye ni shemeji yake; yule pale.

Wageni wa Mheshimiwa Felix Kijiko ni wafuatao: Ndugu Evans Sultan, Ndugu Joram Mtema, Ndugu Daudi Mungura na Ndugu Dismas Luhwanya; ahsanteni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ni Makatibu wa UWT Kata ya Sanuka na Kalinzi kutoka Kigoma Vijijini, ambao ni Ndugu Felsta Thomas na Ndugu Beatrice Kibi. Wale pale karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro ambaye ni mwanae anaitwa Allen Aloyce Kimaro; yule pale karibu sana kutoka Vunjo nadhani.

Wageni wa Mheshimiwa Kidawa Salehe, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Hadija Ngozi na Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni ni Ndugu Miza Ali Kombo, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja; Ndugu Mtumwa Peya Yusuf, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM; na Ndugu Subira Mohamed Ameir, Katibu Mwenezi wa CCM Jimbo la Bumbwini; wale pale. Karibuni sana, huwa ni furaha kwetu kuwaona ndugu zetu kutoka Zanzibar.

Wageni wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ambao ni Madiwani wanne wakiongozwa na Mheshimiwa Masoud Kimondo Diwani wa Kata ya Maseme. Ahsante sana karibuni sana.

Wageni wa Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa wanaongozwa na Ndugu Hadija Maufi, Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Sumbawanga Mjini; Ndugu Adolfina Kanongo; Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji UWT Mkoa; Ndugu Scolastika Malocha, Mwenyekiti wa UWT Sumbawanga Vijijini; Ndugu Hidaya Rubeba, Mjumbe wa Baraza UWT Taifa; Mheshimiwa Rose Komba, Diwani wa Viti Maalum Halmashauri ya Mpanda; Ndugu Camilla Selukingi, Katibu UWT Wilaya ya Sumbawanga Mjini; Ndugu Mariam Sangu Selemani, Mjumbe wa Baraza la UWT Mkoa; Ndugu Teddy Mgawe, Mjumbe wa Baraza la UWT Mkoa na Ndugu Stella Paulo, Mjumbe wa Baraza la UWT Mkoa wa Rukwa. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Rukwa.

Ndugu Lilian Meena kutoka Kampuni Kickstart ya Dar es Salaam yupo Bungeni kuonesha pampu za kilimo cha umwagiliaji ambazo hazitumii mafuta wala umeme. Maonesho hayo yapo kwenye eneo letu la tafrija, Jengo la Utawala. Waheshimiwa Wabunge, nendeni mkaangalie hizi pampu ili muone uwezekano wa kuweza kuzifikisha katika majimbo yetu zisaidie kilimo cha umwagiliaji. Basi mtaona pale kwenye eneo la tafrija.

Mwisho, wapo wanafuzi 30 kutoka Chuo cha Biashara hapa Dodoma, ambao wamekuja kushuhudia shughuli za Bunge. Naomba msimame tuwatambue. Ahsanteni sana wataalam wetu, tunawatakia mafanikio katika mafunzo ili muweze kuja kulitumikia Taifa kwa ufanisi.

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaitisha Mkutano wa Kamati ya Nishati na Madini, saa saba mchana, Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutane leo saa saba mchana, Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutane saa saba mchana leo katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa saba mchana, Ukumbi Namba 231; umeshachukuliwa, utaratibu wa utawala utafanyika pale ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa George Simbachawene, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Sheria Ndogo, mkutane saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement*.

Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, nimetoa ridhaa wao wakutane saa tano kuzingatia Muswada wa Famasia ulioletwa hapa kwa Hati ya Dharura, Ukumbi wa Pius Msekwa. Natumaini watakaoanza saa tano wataweza kufika mahala pazuri tu.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, anahitaji Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wakutane saa saba mchana, Ukumbi wa *Basement B;* kuna na A na B.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo. Kwa kuendeleza shughuli zinazofuata na kwa kuzingatia inabidi nikakutane na wageni wetu kutoka China, namwita Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ili aendeleze shughuli zinazofuata.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2010)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji nilionao kwenye meza ni watatu na naomba niwataje. Kwanza kabisa, atachangia Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga na Mheshimiwa John Paul Lwanji ajiandae. Mheshimiwa Kabwe tafadhali.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali kama ambavyo iliwasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapo jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kutambua uamuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kurekebisha kifungu namba12 kwa ajili ya wao kuweza kufanya mashauriano zaidi Serikalini ili kuhakikisha kwamba, tunalinda haki za watu na wakati huo huo tunaimarisha uchumi wa Taifa letu.

Kwa hiyo, uamuzi ambao ulichukuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni wa kiungwana na naamini kabisa kwamba, baada ya mashauriano huko Serikalini, wataweza kuja na mabadiliko ambayo yatakidhi haja siyo ya sekta moja tu ya mawasiliano, bali yatakidhi haja ya sekta zote za kiuchumi nchini, kwa sababu tunatarajia kesho kuanza kujadili Muswada wa Sheria ya Madini, ambao pia nao una maudhui kama hayo ambayo Muswada wa mwanzo ulikuwa umezingatia kuyaleta mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia eneo moja tu; eneo la mabadiliko ya Sheria ya Msajili wa Hazina pamoja na kumpa nguvu zaidi na kuiimarisha zaidi Ofisi ya Msajili wa Hazina. Mwaka jana kwenye Taarifa yetu Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma na kufuatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na pia Taarifa za Kamati nyingine za Bunge …

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia kuna kelele kidogo, kwa hiyo, naomba u-*bring order* tuendelee kuzungumza.

**MWENYEKITI:** *Order, order,* tafadhali Waheshimiwa Wabunge, taratibu! Tuendelee Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kamati za Bunge za *Oversight* zilitoa mapendekezo kwa ajili ya kuiimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina. Tutakumbuka kwamba, wakati tukiwa ni nchi inayoongozwa na *command economy*, kwamba kila kitu kilikuwa kinapangwa na Serikali; tulikuwa na mashirika mengi sana ya umma ambayo yalikuwa na chombo ambacho kinasimamia *(SCOPO)*.

Mara baada ya kufanya ubinafsishaji, tulivunja chombo kile na kwa muda mrefu sana toka *SCOPO* ilipovunjwa katikati ya miaka ya 1990 mpaka hivi sasa, hakuna chombo maalum ambacho kinasimamia mashirika ya umma kwa ujumla wake. Kutokana na hali hiyo na mara baada ya Bunge kuunda Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ikaonekana kwamba kuna haja sasa ya kuwa na chombo cha Serikali, ambacho kitasimamia mashirika ya umma kama jinsi ambavyo nchi nyingine zinafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, South Africa wana Ofisi ya *Public Enterprises* na mpaka wana Waziri wa *Public Enterprises* kwa ajili ya kusimamia mashirika yote ya umma. Waziri huyo anaitwa Barbara Hoogan. Tanzania hakuna chombo maalum ambacho kilikuwa kinasimamia hili.

Mabadiliko ya sheria ya sasa yanachukua majukumu ambayo *SCOPO* ilikuwa inayafanya na inayaleta kuyaweka chini ya Msajili wa Hazina na hivyo kumpa Msajili wa Hazina mamlaka ya kuweza kusimamia mashirika yetu ya umma. Kwa hiyo, hii ni hatua nzuri sana na inaonesha jinsi gani ambavyo mmeweza kutekeleza majukumu ambayo Kamati ya Bunge iliyapendekeza, lakini zaidi ya hapo, Kambi ya Upinzani Bungeni toka tumeanza Bunge hili la Tisa mwaka 2006, imekuwa …

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Zitto! Waheshimiwa Wabunge, tafadhalini kidogo, kuna mchangiaji anachangia hapa, halafu sauti zenu zinaingilia

michango ya Mheshimiwa Zitto na yeye tu ndiye niliyemruhusu achangie. Mheshimiwa Zitto, tafadhali!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kambi ya Upinzani Bungeni toka Bunge hili la Tisa limeanza mwaka 2006, imekuwa ikipigia kelele *management* za mashirika ya umma. Haidhuru kwamba, imechukua miaka minne Serikali kusikia hilo na leo imeleta mabadiliko hayo ya sheria. Kwa hiyo, tunadhani kwamba ni hatua nzuri, ingawa tumechelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchumi wa Tanzania kwa takwimu za mwaka 2009 ni takriban trilioni 21, fedha za Tanzania. Mashirika ya Umma yote ya Tanzania, mitaji ambayo imewekezwa katika mashirika ya umma, ina jumla ya shilingi trilioni 6.1. Kwa hiyo, kuna fedha za umma au mitaji ya umma mingi sana ambayo ni zaidi au takriban asilimia 30 ya GDP ya nchi na hili eneo lilikuwa halisimamiwi hata kidogo. Kwa hiyo, hatua hii ambayo tumechukua ya kuweza kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma ni nzuri na tunaelekea pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Msajili wa Hazina inarekebisha pia Sheria ya *Public Corporations Act* ya Mwaka 1992. Sheria hii inamwondoa kwa sasa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha katika Bodi za Mashirika ya Umma. Katika hali ya kawaida, tungetarajia kwamba, Sheria hii ingewaondoa moja kwa moja Makatibu Wakuu wote, kwa sababu mashirika ya umma yamesambaa kwenye Wizara mbalimbali.

Kumekuwa na tatizo kubwa sana la Makatibu Wakuu wa Wizara, ambao wao ni wasimamizi wa sera, wanatoa maelekezo kwa ajili ya mashirika, wakati huo huo wanakwenda kukaa kwenye Bodi kuamua juu ya maelekezo ambayo wao wenyewe wameyatoa.

Katika Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, ambayo ilikaa pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo, tulipendekeza kwamba, pawepo na mabadiliko katika Muswada huu katika *Public Corporations Act*, kuhakikisha kwamba, sasa Makatibu Wakuu wote wa Wizara zote wanaondoka kukaa kwenye Bodi ya Mashirika ya Umma. Tayari maelekezo hayo kutoka Serikalini yameshatoka na hapakuwa na sababu ya kufanya marekebisho haya kidogo kidogo. Kwa hiyo, namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aangalie ushauri ambao tulikuwa tumeshautoa kwenye Kamati na akawa ameukubali, lakini hatujauona kwenye *Schedule of Amendment* hapa. Ninaomba *Schedule* hiyo ije ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunafanya mabadiliko hayo kwa pamoja na kutenganisha majukumu hayo kama jinsi ambavyo Kamati na Wabunge waliokuwa kwenye Kamati walivyokuwa wameshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ametoa tena Taarifa ya Mwaka inayoishia Juni, 2009. Kwa miaka miwili iliyopita, Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zimekuwa zikizungumzia umuhimu wa kuondoa *conflict of interest* kwa Wabunge ambao ni watunga sheria, ambao ni wasimamizi wa Serikali na vyombo vyake, kuendelea kuwemo kwenye Bodi za

Wakurugenzi za Mashirika ya Umma. Taarifa ya mwaka huu pia imeeleza suala hilo na imesema kwamba, hiyo ni moja ya hoja ambayo mpaka sasa haijajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi kwamba, Kambi ya Upinzani Bungeni toka mwaka 2006 imekuwa ikilielezea suala hili na madhara yake na la msingi zaidi, inawezekana kuna Kambi moja ya Wabunge wakadhani kwamba, tunapoleta hoja hizi tunawa-*target* wao, hapana! Ukiangalia Wajumbe wa Bodi na mimi ndiyo ninayasimamia mashirika ya umma yote kwa niaba ya Bunge, orodha ya Wabunge waliomo kwenye Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma wako 35 tu.

Bunge lina Wabunge 322 hivi sasa na hao 35 wanazunguka, wanahama kutoka shirika moja kwenda shirika lingine; ni wale wale. Mawaziri wanatumia fursa ya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi kuteua marafiki zao, kuteua watu ambao wana nasaba moja ya kisiasa. Njia pekee ya kuondokana na hiyo *temptation* katika hali ya kawaida sisi binadamu ni watu wenye tama; utakuwa Waziri utataka uweke watu ambao watakutetea na matokeo yake Bodi za Wakurugenzi zimekuwa na makundi mno. Ndani ya Bodi moja utakuta kuna kundi la Waziri ambaye ameikuta ile Bodi na Waziri ambaye aliondoka. Kwa hiyo, unakuta mashirika hayaendi na kuna mifano mingi sana ya Bodi nyingi sana ambazo maamuzi hayafanyiki kwa sababu ya uteuzi wa kisiasa ambao umefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, Mawaziri wanateua Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi bila kushauriana na mwenye mali na mwenye mali kwa mujibu wa sheria ni Msajili wa Hazina. Msajili wa Hazina anaamka asubuhi anasoma kwenye magazeti, Waziri fulani amemteua Zubeir Ali Maulid kuwa Mjumbe wa Bodi ya TANESCO! Msajili wa Hazina hana *CV* ya Zubeir Ali Maulid, hajui ametoka wapi, labda atakuwa ni Diwani, maana kuna wengine wanateua mpaka Madiwani kwenye majimbo yao kuingia kwenye Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumelisema sana, sasa naomba lifikie mwisho. Mwanasheria Mkuu, umepewa jukumu la kuhakikisha kwamba, nchi yetu inakwenda kwa *rule of law* na yetu inazingatia *governance*. Hakuna sababu tena, kama tatizo ni malipo, maana labda inawezekana Wabunge wanateuliwa ili ku-*complement* kutokuwa na mapato, kutokuwa na fedha na kadhalika; ni bora mrekebishe jinsi gani ambavyo Wabunge wanalipwa kuliko ku-*compromise governance*.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika hili pia tuhakikishe kwamba, sasa tunakwenda mbele, tunatekeleza maagizo na maamuzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Wabunge ambao wanadhani kwamba, wanaweza wakaitumikia nchi yetu vizuri kwa kuwa kwenye Bodi za mashirika ya umma, wapishe siasa waende kwenye hizo Bodi wafanye kazi, tulitumikie Taifa vizuri; ni suala tu la mgawanyo wa madaraka.

Mwaka kesho nchi yetu itakuwa na miaka 50 baada ya Uhuru kwa upande wa Tanzania Bara, miaka takriban 46 baada ya Mapinduzi na baada ya Uhuru wa Zanzibar na miaka takriban 46 baada ya Muungano. Tumeshakua sana, kwa hiyo, tunao watu ambao wanaweza wakaingia kwenye mashirika na wakaweza kushughulikia mashirika

haya bila haja ya kuchanganya na kuondoa hizo *power* kutoka kwa Mawaziri kuteua Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala tu la kiutendaji, kumekuwa na matatizo sana. Wenyeviti wa Bodi za Mashirika ya Umma wanateuliwa na Rais, Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanateuliwa na Rais pia. Kwa hiyo, kumekuwa na kutokuwa na maelewano kwa sababu *appointing authority* ni moja kati ya Mwenyekiti wa Bodi na yule Mtendaji Mkuu wa Bodi.

*Public Corporations Act* ya Mwaka 1992 imesema wazi kwamba, Bodi za Wakurugenzi ndizo zitakazokuwa zinateua Watendaji Wakuu wa Mashirika, lakini hilo halifanyiki, bado Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaendelea kuteua Wakurugenzi Wakuu na Mashirika mengine Mawaziri wanateua Wakurugenzi Wakuu. Ninaomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuimarishe kidogo ile sehemu ya *Public Corporations Act* ili iwe wazi kabisa kwamba Watendaji Wakuu wanateuliwa na Bodi na kupewa mikataba maalum ya kufanya kazi ili Bodi hizo nazo ziweze kuingia mikataba maalum na Msajili wa Hazina kwa ajili ya utendaji wa mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na maombi hayo ya kuletwa kwa mabadiliko ambayo tulikuwa tumekubaliana, lile la Makatibu Wakuu wa Wizara zote kama tulivyokubaliana kwenye Kamati na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hili la Wabunge kuondoka kwenye mashirika ya umma kwa kufanya marekebisho kwenye *Public Corporations Act* kwamba, hakuna mwanasiasa atakayeteuliwa kuingia kwenye Bodi za Mashirika ya Umma, yaweze kuzingatiwa ili tuweze kupitisha sheria hii na kuboresha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuweza kudhibiti mali zetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutuletea hoja hii vizuri, maelezo yake jana yalikuwa mazuri.

Ukweli ni kwamba, toka ndugu yetu huyu ameingia hapa na kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amefanya kazi nzuri, anaendelea kufanya kazi nzuri na ametushauri mambo mengi kwa muda mfupi. Kwa hiyo, namtakia kila la heri na tumpe ushirikiano unaostahili ili aweze kutufanyia kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na *Public Service Retirements Benefits Act*, ukurasa wa 14 mpaka 15, kifungu cha 12(2), naomba nisome ile *sub-section* (*2)* anasema: *"Subject to sub-section (3) and (4) and paragraph "e" of section 16, an officer who attain the age of 55 and does not opt to retire voluntarily shall continue to be in service until he attain the age of 60 which is the age of compulsory retirement."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki nakiona kwanza, kinamfunga mtumishi ambaye ameshafika miaka 55 na zaidi. Ninachotaka kuelewa ni kwamba, ukishafika miaka 55 usipostaafu, basi huwezi kustaafu katikati mpaka uende miaka 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikotoka wakati *retirement age* ya hiari ilikuwa miaka 50 na ila ya lazima ilikuwa miaka 55, mimi nakumbuka kwamba ukishafika miaka 50 unaweza ukastaafu kwa hiari.

Vile vile kati ya miaka 50 na 55, ukiona kwamba mambo yanakwenda vigumu, wakati mwingine afya unaona umechoka choka hivi na kadhalika, basi ilimradi umefikia ile *qualification* ya kuwa na miaka 50, unaomba kustaafu na una-*qualify* kupata haki zako zote za kustaafu baada ya kufikia umri huo.

Sasa hapa ilivyoandikwa kwamba lazima ufike 60 kama hukuwahi pale 55, kwa kweli ninaona kama inataka kuwanyima haki baadhi ya watumishi kwani inawezekana miaka 55 ulijiona bado una nguvu, lakini ulipofika miaka 57, miaka 58, ukaona nguvu zako zimepungua pungua na ili usije kufukuzwa kazi kwa sababu ya uzembe au jambo lingine, unaamua kuandika barua ya kustaafu.

Mimi ningelishauri sana Serikali iliangalie hili. Sijui ni vigezo gani vimetumika katika kumlazimisha mtu lazima afike miaka 60 baada ya kufikisha miaka 55. Ninamwomba Mwanasheria Mkuu na Serikali kwa ujumla waliangalie hili, ilimradi mtu ame-*qualify* kufika miaka 55, nadhani akifika 57, 58 naye aruhusiwe kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nakumbuka sawa sawa, zamani watumishi wanawake walipewa kaupendeleo hivi; unajua akina mama hawa wanafanya kazi nyingi sana za maofisini, viwandani, halafu wakifika nyumbani tena wanafanya kazi za nyumbani na kazi kubwa ile ya kibaiolojia. Sasa, wanaweza kufika miaka hiyo wakawa wamechoka, kulikuwa na upendeleo maalum wakishatimiza miaka 50 wanaweza kustaafu tu.

Sasa kwa kuliweka hivi, kwa ujumla hata ile huruma ambayo ilikuwa imetolewa kwenye sheria za awali ya kumhurumia huyu mwanamama ambaye anaweza akawa amefika mahali amechoka kwa sababu ya mizigo mikubwa ambayo mtumishi mwanamke siku zote anayo, nayo itakuwa imeondoka. Nilitaka kushauri liangaliwe hilo, ikiwa ni kutazama hawa akinamama ambao wanafanya kazi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukija kwenye Sheria nyingine inatoa mwanya, sijui ni kipengele gani kile, kinatoa mwanya kwamba siyo lazima ufikishe miaka 60, sasa naona hapo kama kuna *contradiction* kidogo. Ukurasa wa 40 nafikiri kifungu namba 98, kama niko sawasawa, lakini kwenye Sheria ya *NSSF* hii niliyosoma ya kwanza ni ya Serikali, lakini kwenye Sheria ile ya *NSSF* tafsiri yake ukiisoma pale unakuta kuwa mtu akishafikisha miaka 55 na zaidi anaweza akastaafu bila matatizo yoyote. Sasa kwa nini kuwe na tofauti kubwa kiasi hicho, hawa huku waseme kuwa inaruhusiwa lakini ile Sheria nyingine inasema hairuhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianzisha *Regulatory Authority* ya mambo haya ya Hifadhi ya Jamii. Nilidhani moja ya kazi ku-*standardise*, kuangalia mambo muhimu haya ili yawe sawasawa *whether* uko kwenye *Public, PPF* au *NSSF,* haya mambo ya msingi nadhani ni vizuri yakaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye ukurasa wa 40, pale napambana na tafsiri ya neno *informal sector,* nadhani hii ni katika Sheria inayohusu *National Social Security Fund,* inasema: "*Informal Sector means The sector which include workers who working formally and who do not work in terms of an employment contract or any other contract".* Hapa nataka nijihusishe na suala la wakulima katika siku za nyuma tulisema jamani Serikali ni vizuri ikaangalia vilevile uwezekano wa kuanzisha hizi *scheme* za Hifadhi kwa wakulima kwa sababu ukweli ni kwamba wakulima wanapozeeka na kama bahati mbaya kama hana mtoto au watoto aliona nao hawamsaidii sana basi anakuwa hoi kiasi kwamba hata maisha yake yanaweza kupotea kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumeshauri kwamba ni afadhali kwa mfano, kama wanaweza kuwa wanachama wa NSSF ukatafutwa utaratibu wa kuwawezesha kuingia kwenye *NSSF*. Wataalam wataangalia utaratibu wa namna gani mkulima ataingia kule na kulipa zile *due* zinazohusika ili aweze ku- *qualify* kuwa mwanachama na afikiriwe kupata maslahi ambayo yatamsaidia mkulima huyo. Mara kadhaa katika vikao vyangu au mikutano yangu ya hadhara wakulima wameniuliza ninyi wafanyakazi mna *pension,* mki-staafu maisha yenu yanaendelea kuwa mazuri, sisi wakulima ambao ndiyo tunahangaika maisha yetu yanazidi kuwa duni kwa sababu hakuna *scheme* yoyote mliyotuwekea, hivi mna mpango gani wa kutusaidia sisi wakulima angalau na sisi tuwe na afueni baada ya kustaafu kwa maana ya kwamba akifika miaka hiyo ya 60/70 hawezi kuwa *active* katika kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa tafsiri hii hapa ambayo nasema habari ya *informal sector,* kama inaweza ikamhusisha na mkulima ili wakulima nao wafikiriwe kuingia kwenye *scheme* hizi hasa ya *NSSF* ili baadaye wakishazeeka mzee wa watu au Mama wa watu na yeye aweze kufaidika na jambo hili, tutakuwa tumewafikiria na kuwaondolea matatizo yanayowakabili wakulima wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lipo kwenye ukurasa wa 43, kifungu namba 15A(1).Hapa anasema: "*Where the Director General is satisfied that there is evidence of non remittance of contribution to the fund by an employer as required under this Act, he shall report such a default to the Authority".* Hili ni tatizo sugu, wapo waajiri wengi ambao hawataki au hawapendi kupeleka michango ya wafanyakazi wao katika hii Mifuko ya Hifadhi wanakata mishahara ya wafanyakazi, sasa kama wanakata mishahara ya wafanyazi hizi pesa wanazipeleka wapi na kule *NSSF* au *PPF* hawazipeleki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wanalelewa hawa na kwa nini wanaonewa aibu kwa kutokushughulikiwa? Kwa sababu hili ni kosa, kukata mchango wa mtu badala ya kuupeleka kule *NSSF* au *PPF* hupeleki, matokeo yake unakaa nao na wengine wanatumia kwa mambo yao mengine au gharama zingine za uendeshaji na kadhalika badala ya kupeleka kule kunakohusika hivi ni kwa nini hawa wanaonewa aibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili siyo jambo la kulitazama kwa makusudi tu. Kwa mfano, hivi majuzi wafanyakazi wa *Air* Tanzania karibu mia moja na hamsini na kitu walistaafishwa kutokana na hali ya *Air* Tanzania kwamba ndege zimepungua na idadi ilikuwa ni kubwa. Kwa hiyo, ikabidi wapunguzwe, sasa wale waliopunguzwa walipokwenda kufuatilia mafao yao kule wamekuta kwamba michango yao haijafika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, tumia *microphone* ya mbele, hiyo ya kawaida.

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafuatilia hoja ya Mheshimiwa Missanga lakini sielewi anachangia Muswada gani. Pamoja na michango mizuri inayonivutia lakini sielewi anachangia Muswada gani, Muswada anaochangia nadhani ni tofauti siyo huu ambao nimeuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Missanga tafadhali washa *microphone,* halafu fafanua hili.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichogawiwa ni hii *miscellaneous Ammendment* ya *Financil Law* au ni tofauti na hiyo ambayo..

**MWENYEKITI:** Siyo, ni tofauti.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi niombe radhi.

**MWENYEKITI:** Umesamehewa Mheshimiwa.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Lakini nadhani yale niliyosema yamezingatiwa.

**MWENYEKITI:** Kama ulikuwa nalo la kuchangia kwenye hili uendelee au vinginevyo iwe basi tena.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Kwa sababu nillikuwa namalizia, nilikuwa nimebakiza suala moja tu, basi nadhani niishie hapo lakini Serikali imesikia yale ambayo nimeyasema. Ahsante sana.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na nimeshiriki pia katika kupitia Muswada huu. Sitakuwa na

mengi ya kuchangia isipokuwa nitajikita kwenye eneo moja dogo na eneo hilo ni ile sehemu ya tisa ya Muswada, natambua kwangu hakuna bahari, kwangu kuna mbuga tu, lakini watu pia wanashiriki katika Ujenzi wa Taifa katika maeneo hayo, wanashiriki pia kwenye shughuli hizo za ubaharia na kwenda maeneo mbalimbali hapa Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu na nachukua nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa umahiri alionao katika kuleta Miswada yake hapa Bungeni na kwa kweli nadhani tumepata mtu mahiri wa kuweza kutusaidia tunaporekebisha Sheria zetu, basi hizi Sheria zitusaidie na ziendane na hali halisi ya mazingira yetu kwa sababu kitu kikubwa hapa tunaangalia usalama wa raia wetu pamoja na rasilimali zetu. Sasa hiki kifungu cha 9 naelewa kabisa kuna mjadala ambao umekuwa ukiendelea kuhusu adhabu ya kifo, watu wanafikiria kwamba pengine tuifute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haijaletwa hapa Bungeni lakini jinsi ilivyoletwa inaonekana kama kwamba inataka kuwapendelea wageni ambao wanachukua rasilimali zetu bila sisi wenyewe kuwaruhusu. Mfano mmojawapo ni hii meli ya juzi juzi iliyokuja kukamatwa hapo ikivua samaki, huo ni uharamia na watu hawa sijui kama bado wako gerezani au wapi lakini nimeambiwa kuwa bado wapo na kuna kesi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya uharamia ukiangalia kamusi zinasema hivi *"Pirate"*yaani haramia ni jambazi anayeiba baharini kwa kutumia nguvu yaani *shifter*, mnyang'anyi au gaidi". Pia katika tafsiri ya Kiingereza katika *Dictionary* ya *Oxford* inasema: "*Is the one who robs at sea or plunded as the land from sea without a commission of a sovereign state"*. Sasa ukiangalia unajua hasa ni nini adhabu ya huyu mtu, inatakiwa sasa ukiua adhabu yake iwe ni kifo, sasa huyu anaye *plunder* na kuua, maana huyu jambazi yeye kazi yake ni kunyang'anya na akizuiwa kunyang'anya ni lazima aue, sasa tunamtangulizia adhabu ambayo ni chini tunasema kwamba afungwe maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufungwa maisha huko kuna wengine wanaweza kujitetea pale akafungwa miaka saba, miaka ishirini, miaka mitano au miaka miwili akaondoka zake. Sasa apewe hiyo adhabu *maximum sentence,* sitaki watu wauwawe, hapana, iletwe Sheria hapa kama tunafuta adhabu ya kifo basi ifutwe, sasa kwa nini haya majambazi yawe ya baharini, yawe ya nchi kavu, yanapora mali zetu na nini, wao wapewe adhabu ambayo ni chini ya hiyo, tatizo letu tunapenda sana kuwahusudu watu wa Mataifa ya nje kuliko sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa *maximum sentence* hapa ni *capital punishment* kwa kosa kama la kuua na kufanya nini sasa ingetamkwa pale kwamba badala ya kusema *life imprisonment* isomekane kwamba ni *death sentence,* sasa waji-*extricate* kutoka hapo. Wao wajikwamue kutoka hapo kwa nini asife, sidhani kama kuna usalama wowote jambazi anapokuingilia. Jambazi kazi yake ni kuua na kupora. Kwa hiyo, naomba sana tusianze kutanguliza hisia kwanza kwamba Muswada utakuja

ukakubalika kwamba *death sentence* tutaiondoa, hapana uletwe Muswada hapa ukubalike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tufanane na *civilized states* na sisi *of course* labda tuna *marks* za kufika huko lakini sisi ni maskini. Ni lazima tulinde mali zetu kwa hali na mali. Leo hapa tulikuwa na Naibu Spika wa China wenzetu hawaangalii wewe ni nani inapofika kwenye rasilimali zao pamoja na watu wao wamenyongwa juzi hapa na Wajapani kwa kosa la kuuza madawa ya kulevya, walikamatwa watu na madawa ya kulevya walikuwa sijui watatu au sijui wangapi wakanyongwa, kwa sababu wanalinda watu wao na hawana ajizi kwenye suala hili *they are very serious* na hatuigi masuala mabaya, tunaiga masuala mazuri tu, basi tutakwenda kule tutaiga yale mazuri, lakini yale machungu ya kuturekebisha hatutaki tunafanya mambo kama sisi ni Marekani, Uingereza lakini ni maskini, hatuwezi kuendelea na Sheria zetu ndiyo zimeiga mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi zitakwenda kwa mfano za Benki Kuu za wapi zitakwenda na mwisho wale watu wataachiwa na huku *plundering of our resources* inaendelea tu, magogo yatakwenda, samaki wetu watakwenda, Benki zitaibiwa yaani *we are not serious, I am not a prophet of doom* Sheria zetu tuzirekebishe ili ziendane na hali yetu naomba sana kifungu hiki kiangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *pirates* ni biashara nchi jirani hapo ya Somalia, sasa hivi ndiyo kazi, utakuta mwaka 2008 kwa kazi hiyo walilipwa malipo ya rehani dola milioni 55/=, sasa dola milioni 55/= ni shilingi billioni ngapi za Kitanzania ni pesa nyingi sana. Mwaka 2009 ikapanda ikawa dola milioni 60/= na mwaka huu inaongezeka zaidi na vijana wa kule sasa hawataki kazi nyingine zaidi ni kazi hiyo ya uharamia. Lile sijui ni Taifa, sijui ni nini, Somalia ilishasambaratika siyo Taifa, ni nchi tu ipo ya Ukoo na nini na kazi yao ndiyo hii sasa kama ikiwa *lucrative* na mambo yetu ndiyo hayo na magereza yetu hayo tunayoyaboresha watu kule wanasoma magazeti, wanakula ubwabwa, wanafanya nini, basi watu wataamua wata- *opt* kwenda kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akikamatwa anakwenda, *he spend the rest of his life* na kwa kweli sidhani kama kweli itafikia hatua atamaliza *life sentence* itakuwa baada ya miaka fulani anaachiwa anaendelea na shughuli zake. Sasa hivi tunavyofahamu hata hiyo *death sentence* hapa nchini sijui kama inatekelezwa na ndiyo unakuta sasa uhalifu ndiyo unazidi nchini hapa mfano juzi hapa ukiangalia vitu kama vya Tukuyu vinasikitisha sana watoto wadogo wanauawa, kwasababu Sheria zetu hatukazii sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, kama hatuwezi basi tuwaachie nchi zilizoendelea, tunapomkamata tukishamhukumu badala ya kuja mtu anakaa muda wote anakula vitu vyetu ndani humo, *resources* zetu, hizo pesa zingeweza kutumika kwa shughuli nyingine badala ya kuwalisha wao, tungesomesha watoto wetu na kadhalika. Kwa hiyo, tuwaambie Wamarekani bwana njoo uchukue hawa watu, kawahukumu wewe kwa sababu hatuna njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba iangaliwe hii kwamba badala ya *imprisonment for life* iwe *death sentence for life for those people* wanaojishirikisha kwenye uharamia, majambazi na wengineo. Hii ni juu yao sasa wao wenyewe watajikwamua vipi na tusiwe na huruma, sijui huyu Mchina, huyu Mmarekani, huyu Msomali, *death sentence should be native for those people* wanaoji- *involve* kwenye haya mambo ili ijulikane kabisa Tanzania siyo nchi ya kuchezea tunapokwenda pale ni hatari. Hii meli iliyokamatwa kama nilivyosema mwanzo tukaja kuambiwa kulikuwa na meli nyingi zilikuwa zinavua pale na meli nyingi zinapita zinabea magogo. Sasa kweli sisi tunaendelea kuwa maskini, mtu anakosa hata shilingi 200/= ya kuishi kwa siku na mali zetu zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu tukiwakamata ndiyo wanaingizwa katika magereza yaliyo mazuri wanapumzika lakini watu wetu wanaendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipoteze muda lakini naomba sana hiki kifungu kiangaliwe, hii *death sentence* kama inafutwa basi ijulikane kwamba ni *life sentence*, siyo tuna sheria ya *death sentence* kwa watu wetu halafu upande mwingine kuna sheria inayowasamehe wengine kupata adhabu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo na naunga mkono Muswada huu.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa John Paul Lwanji, sasa nitamwita Mheshimiwa John Momose Cheyo na atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, kwanza nataka kutumia nafasi hii kuwaeleza wale wapiga kura wangu walikuwa wananipigia simu niko wapi, naomba kuwataarifu kuwa nilikuwa Afrika ya Kusini kwa ajili ya Bunge la Afrika, Bunge ambalo tunajivunia Balozi Mongela kwa kulianzisha lakini linahitaji msaada wa sisi sote ili liwe Bunge kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka zaidi kujielekeza katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza ambayo ni rahisi ni kipengele Na. 40 ambacho Mwanasheria Mkuu wa Serikali amefuta kipengele cha saba katika *Electoral Laws Expenses Act*. Jambo hili ni zuri na napenda kumsifu sana kwa kuwa msikivu kwa sababu kweli ilikuwa inaleta shida kwamba wewe unagombea halafu upeleke timu yako ya kampeni kwa Afisa wa Kata na sitaki kuleta ugomvi katika Bunge hili lakini baadhi ya Maofisa hawa wanajulikana kabisa kwamba wanatumikia chama kimoja. Kwa hiyo, ni jambo jema sana ambalo limefanyika na nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ambayo nataka kujielekeza ni kuhusu jambo muhimu la *Treasury Register* yaani mtu ambaye anasimamia mali ya Serikali. Kusema kweli tangu tuanze mambo ya ubinafsishaji, sehemu hii ni kama vile tulikuwa tumeacha mali zote za Serikali hazina mwenyewe, na mali hizi ni nyingi. Serikali mpaka

tarehe 30 Juni 2008 ilikuwa imewekeza takriban trilioni sita, trilioni sita ni karibia bajeti ya Serikali nzima ya mwaka ambao tunaumaliza sasa hivi. Sasa hizi fedha bila kuwa na mwenyewe ni kweli tunapoteza fedha nyingi sana na hazina wafuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka nilipokuwa katika Kamisheni ya Mheshimiwa Bomani ya kuangalia mambo ya Madini, tulipomwita *Treasury Register* hebu tupe orodha ya *share* za Serikali katika Mashirika mbalimbali ambayo yalikuwa yanahusika na madini, tulishangaa mahali ambapo tulikuwa tunafikiri tuna-*share, Treasury Register* hakuwa na habari. Hali ya namna hii kusema kweli Serikali inaendesha mali bila kuwa na mwenyewe. Kwa hiyo, hatua hii ni hatua ambayo sisi Wabunge wote lazima tuisifu na tusiishie kusifu tu bali tusisitize iwe ni ofisi ambayo inajitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi katika vipengele hapa kwamba fedha zake zitaletwa hapa Bungeni na Bunge hili litaidhinisha fedha kwa ajili ya Ofisi hii, jambo hili ni jema na ofisi hii iimarishwe ili iweze ikaangalia mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC),* unajua wazi kwamba juzi tu tulipokuwa tunaangalia hesabu za Serikali tumegundua hata kuna sehemu zingine ambapo Serikali imetoa *guarantee* kwa ajili ya Mashirika mbalimbali lakini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amegundua fedha hizo wala hauwezi ukazipata mahali popote kama vile zimeandikishwa ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kulikuwa na takribani bilioni 26 ambazo Kagera *Sugar* imepewa bilioni 7, Kiwira *Coal* imepewa bilioni 15.5, Dar es Salaam *Cement Company* imepewa bilioni 7.7 na zote hizi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hakuweza kuona *register* yoyote ambayo inaonesha *guarantee* ya Serikali katika sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali yetu ina dhana mbaya kuhusu mambo ya dhamana. Wanafikiri kwamba unapodhamini basi unamwezesha tu, ni kitu ambacho unaweza ukakiweka kwenye droo au kwenye kikapu na siyo tatizo la kwao kama Serikali. Lakini ukweli ni kwamba unapotoa *guarantee* maana yake ni kwamba kama yule mtu atashindwa kulipa itakuwa ni mzigo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa mwaka ambao umeishia tarehe 30 Agosti, takribani bilioni mia tano na sitini na tisa, hizi ni fedha nyingi sana kwa Serikali, lakini Ofisi ya *Treasury Register* hata hizi pesa wakati mwingine hawazifahamu. Kwa hiyo, ni vizuri kuhakikisha kwamba Serikali inaangalia *guarantees* zake. Ningependekeza ni afadhali tujue kila mwaka Serikali ina *commitment* ya namna gani kwa watu mbalimbali na ziwe mojawapo ya kipengele katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaletewa bajeti ya Serikali lakini hatujui Serikali imetoa *guarantees* sehemu ngapi na ina deni kiasi gani, ndiyo maana tunaona kila wakati deni la ndani zaidi linakua kwa takriban asilimia ambazo hazikubaliki. Kwa hiyo, ni lazima tufike mahali ambapo Serikali tunaweza kuiambia huwezi ukatoa

dhamana ya zaidi ya kiwango hiki cha bajeti, kwa sababu tumetoka katika sehemu ambapo tulikuwa na madeni mengi, sasa tumepunguza madeni mengi sana ya nje kwa sababu watu wametusaidia, tusiingie tena katika utaratibu ambao tunaanza tena kukopa na kutoa *guarantees* ambayo tunapoteza fedha kwa sababu hatuwezi kulipa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika vipengele vilivyowekwa hapa ingeeleweka mojawapo ya kazi ya *Treasury Guarantee* iwe pia kudhibiti hizi dhamana ambazo tunatoa kwa ajili ya *NSSF*, *PPF* na kila wakati tunasema bajeti yetu ya Serikali inaendeshwa sana na Mashirika haya, Serikali ikishindwa kutoa fedha za kunusuru madeni haya, ndiyo kusema kwamba *NSSF* haitakuwa na fedha ya kulipa wafanyakazi, *PPF* itaanguka na Mashirika mengine pia. Kwa hiyo, tunahitaji *Controller* au mtu ambaye atahakikisha kwamba Serikali inafikia wapi katika kutoa hizi dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua hata kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali kwamba hata Deni la Taifa, kwa maoni yetu tungependa kuona kwamba hili Deni la Taifa pia iwe mojawapo ya jukumu la *Treasurer Register* ili tuweze hata kufuatilia, pawepo na ofisi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Benki Kuu inaangalia Deni la Taifa, *Accountant General* anaangalia Deni la Taifa, Wizara ya Fedha ina kitengo cha Deni la Taifa, tumegundua hata mara nyingine Benki ya Tanzania inaweza ikalipa deni na baadaye ikatokea kwamba deni lile lilishalipwa au deni lile lina bakaa iliyo ndogo zaidi. Hali hii ndiyo imetufikisha mahali ambapo tuna matatizo, tuna-*scandals* kama zile za *EPA* na kadhalika kwa sababu Deni ya Taifa halina mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wangu na natumaini tutauweka pia katika ushauri wa Kamati kwamba *Treasury Register* apewe majukumu zaidi na asiwe mtu ambaye anaongozwa na Katibu Mkuu wa Fedha kwamba nenda hivi ama pesa yako tunaikata hivi, tufike mahali ambapo *Treasury Register* awe na *independence* iliyo karibu kidogo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali. Tukifika hapo basi mali za Serikali zitaangaliwa na ushauri mzuri utaweza kutolewa kwa Serikali kwamba, tusifike mahali ambapo tunakuwa na dhamana kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na haya ndiyo nilitaka kuyasema. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa John Momose Cheyo. Sasa namwita Mheshimiwa mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Estherina Kilasi.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya mabadiliko mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ambayo ameanza sasa na tunampongeza sana kwa sababu mabadiliko yanaenda na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeza hizi sheria muhimu kwa wakati muafaka, mimi nina jambo moja au mawili ya kuchangia. Kilichonigusa hasa nichangie ni kwa upande wa sehemu hii inayohusu Msajili. Hoja hii imekuwa ni ya muda mrefu kwa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sisi sote Wabunge na hasa wale ambao tupo kwenye Kamati hizi muhimu tunazoziita (*Oversight Committee*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hii siyo hoja ya Wabunge labda wa Upinzani ni ya Wabunge wote wa CCM na Wapinzani kwa sababu wote tulikuwa tunaona ofisi hii angalau haifanyi kazi yake ipasavyo. Utakumbuka wakati tunatoa Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, tuliongea kwa sauti kubwa sana na wenzetu Wabunge wakatuunga mkono kwamba hii ofisi inahitaji kujitegemea sambamba na tulivyopigia kelele kwenye sheria ya *CAG* kwamba huyu Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inabidi awe na ofisi yake na bajeti yake ili kusudi aonyeshe ile *independence*. Naomba nipongeze sana uamuzi huu hasa kwa Wizara ya Fedha kwa kushiriki kikamilifu kuhakikisha kwamba wanaiachia Msajili iwe ni Ofisi ya kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyetiki, angalizo langu ambalo nataka kulisema katika ofisi hii, tulizungumza wakati ule kwamba ofisi hii ilikuwa haijawa imara, haina wafanyakazi, haina watalaam wa kutosha kuweza kuhimili majukumu ya idara hii ya Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, kwa sasa pamoja na sheria hii na vifungu vyote vilivyooneshwa ambavyo naviunga mkono kwa asilimia mia moja ni kwamba sasa kinachotakiwa ni kuhakikisha katika yale majukumu aliyopewa anapewa wataalam wa kutosha sana ili kazi hizi ziende vizuri kwa sababu kuna mapungufu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunapitia Mashirika ya Umma, unaweza ukakuta unamuuliza Msajili au ofisi ile kwamba hebu tupe orodha ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa inawezekana hesabu haipo, ni kiasi gani cha hisa zimeuzwa au ulizobaki, nazo hana. Ni pesa kiasi gani zipo kwenye mfuko wa ubinafsishaji ambazo zingefaa aidha ku-*invest* au kuwalipa hata wale ambao wamepunguzwa kazini, unakuta hiyo hesabu haipo na unavyomuuliza unaona kama unamwonea hiki kitu hakipo. Kwa hiyo, ilikuwa haijulikani nani mwenye majukumu, Katibu Mkuu au Msajili. Kwa hiyo, nafikiri kwa sasa tutakwenda vizuri. Ndiyo maana nasisitiza hapa kwamba hii ofisi iimarishwe vizuri kila kitengo, kama kutakuwa na kitengo kinachoshughulikia mambo ya ubinafsishaji tu na usajili wote wa ubinafsishaji uwe pale. Lakini vilevile kufuatilia madeni ambayo tunayo kwenye mashirika tuliyouza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumetembelea Kilombero *Sugar*, unaona aibu unapokuta wafanyakazi wanalalamika kulipwa malipo yao ya wakati ule walipoacha mkataba wa Serikali na kuingia mkataba mpya. Mwekezaji anakwambia sisi tumeshalipa sehemu yetu lakini bado Serikali inadaiwa, ukimuuliza Afisa Msajili labda vipi hawa watu kwa nini hawajalipwa, anakwambia tunatafuta pesa. Ukimuuliza ni kiasi gani, inawezekana hata ile orodha hawana, kwa hiyo hilo nilifikiri sana lisimamiwe na kuifanya hii ofisi iwe imara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije labda kwa upande mmoja, limenigusa na nikasema nizungumze. Lakini nawapongeza Mawaziri hasa kwenye upande wa Bodi. Kwa upande

wa Bodi zinazoteuliwa kwenye Mashirika ya Umma, Msajili ndiye anayewajibika kwa kila Shirika la Umma na ndiye anayepitisha majina na kutangaza. Nawapongeza Mawaziri wamekuwa wakifuata utaratibu mzuri tu wa kuteua hawa Wakurugenzi wa Bodi. Unapoteua Mkurugenzi wa Bodi ni lazima uhakikishe kwamba anakwenda kusaidia nini kwenye lile shirika bila kujali ni nani. Kwa sababu utaratibu ulioanzishwa sasa ni wa kutangaza nafasi hizi za bodi, kwa hiyo watu wanaomba wenyewe wanafanya *interview* na hatimaye wanateuliwa, mtu wa kuwajulisha aidha anakuwa ni Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusianze kuiga kila kitu kwa sababu inaonekana wenzetu wa upande mwingine wanasema, labda tuanze kubadili sera yetu, tutakapofikia kwamba Mbunge asiwe Waziri basi na Mbunge asiwe tena Mjumbe wa Bodi. Lakini kwa hali iliyopo siyo rahisi ukatenganisha vitu hivi, kwa sababu kama mtu una uwezo ninavyoona kwa uzoefu wangu, nimekuwa Mjumbe wa Bodi, nakumbuka Bodi ya kwanza niliteuliwa na Mheshimiwa Basil Mramba kuwa Mjumbe wa Bodi ya *TRA*, lakini nikaambiwa nipeleke *CV*, nikapeleka *CV* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha msingi nafikiri unasaidia sana kama una *profession* yako, lakini la pili kama ni Mbunge, kwa sababu unapokuwa pale kuna vitu vingine ambavyo vinahitaji tafsiri ya sheria mbalimbali na wewe umezipitia hapa, unasaidia kuelimisha wenzako. Kwa hiyo, kinachotakiwa pale ni *competence* siyo *politics*. Kwa hiyo, nafikiri tujenge hoja tu tusiseme kwamba kuna upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limenigusa, Mwenyekiti wangu ninachoungana naye ni kimoja, kwamba wale wanaoteuliwa waangaliwe kama wanafaa katika kusimamia shughuli zile za shirika, lakini tusiangalie kwamba huyu ni Mbunge au ni nani kwa sababu ameteuliwa kabla hajawa Mbunge na kazi zake anazifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaamini kwamba Mawaziri wameshateua Wajumbe wa Bodi kwa kuangalia urafiki au undugu. Mimi nilipoteuliwa nilikuwa simjui hata Waziri mmoja, lakini niliteuliwa kwa kuangaliwa tu, najisemea kwa sababu kidogo inaonyesha kama Mawaziri wanateua ndugu hivi, lakini naomba nipongeze kwamba wamekuwa wakisimamia kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Uenyekiti wa Bodi, tumeguswa na vitu vingi sana huko tunapokutana navyo, sasa naamini Msajili atakuwa msimamizi wa kuangalia hata malipo ya Wajumbe wa Bodi mbalimbali. Kwa sababu kuna tofauti kubwa sana na mara nyingi ukimuuliza Msajili anasema hizi wanapanga kwa kuangalia uwezo wa Shirika, lakini ni vizuri kukawa na *uniform payment* kwa mashirika yote ili kusionekane kuna matumizi makubwa kati ya Bodi moja na Bodi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ilikuwa kwamba baada ya kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuna sheria zingine bado zinahitaji marekebisho ambazo ni muhimu sana na zingetakiwa zifanyiwe kazi. Kwa mfano, nilikuwa namdokeza *PM*

hapa kwamba kuna sheria ambazo zimetungwa na hazijawahi kufanya kazi mpaka sasa. Kwa mfano, sheria hizi za kupandisha Hifadhi za Taifa. Mwaka 2008 tulipitisha sheria ya kupandisha hadhi ya Hifadhi ya Taifa ya Usangu Ruaha. Eneo lile tukawa tumepitisha kwa makosa, sheria ilipitisha kwamba lazima vijiji 14 vihame, lakini kilichokuwa kinazungumzwa hapa ni vijiji saba tu, tunafikiri hii sheria mpaka sasa haijafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza *TANAPA* hawajaanza kufanya kazi kule ndani kwa sababu mipaka inaonekana ina-*conflict of interest* kwamba vijiji vinaingia ndani ya hifadhi, vijiji 14 vinaingia ndani ya hifadhi, kwa hiyo ningeomba Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri ambayo ameianza sasa ajaribu kuipitia na hii sheria aone inaweza ikarekebishwa kwa wakati gani, iwe kwa njia ya Azimio kwa haraka iwezekanavyo ili kusudi *TANAPA* nao waweze kufanya kazi yao. Lakini vile vile na wananchi hao wanaoizunguka hii hifadhi waweze kuendelea na shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia mchango wangu vile vile napenda niwashauri wananchi wa Mbarali wanaozunguka hifadhi ile kwamba, wale ambao wameshaweka kesi au pingamizi waziondoe haraka ili kusudi Serikali waweze kufanya kazi yao, ili tuweze kurekebisha mipaka iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Kilasi umekuwa ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho. Kwa heshima zote naomba nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aanze kutoa maelezo ya kujumuisha mijadala ya Waheshimiwa Wabunge.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia Muswada huu, kwa kuongea, kuandika, kwa kushangilia na kupiga makofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pia kwa jinsi ambavyo umeongoza mjadala huu asubuhi hii. Tumekuwa na wachangiaji sita ambao wamechangia kwa maandishi. Mchangiaji wa kwanza alikuwa ni Daktari wa Falsafa ya Sheria Mheshimiwa Harrison Mwakyemba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mhandisi Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Ndugu yangu Ismail J. Ladhu, Jimbo lake Dar es Salaam. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuongea nawatambua kama ifuatavyo: Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani; mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Alhaji Mohammed Missanga, Mheshimiwa Paul Lwanji Mbunge wa Manyoni Magharibi; Mheshimiwa John M. Cheyo na mwisho Mheshimiwa Estherina J. Kilasi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na waliochangia kwa maandishi. Mheshimiwa Daktari wa Falsafa ya Sheria Mheshimiwa Harrison Mwakyembe

anakubaliana kabisa na sisi kwamba Muswada huu ni vizuri uwasilishwe. Lakini ametahadharisha kwamba baadhi ya madhumuni na sababu za Muswada hayaendani na marekebisho tuliyoleta. Tunakubaliana na wazo na tumesahihisha makosa hayo.

Eneo moja ni kwenye adhabu ya *Piracy* au uharamia wa bahari na tukasema kwamba ni kifungo cha maisha gerezani. Labda nilieleze hili kwa sababu Mheshimiwa Lwanji amelizungumzia labda elimu tu. Adhabu ya kifo ambayo inatamka kwamba utanyongwa mpaka kufa inatumika tu kwa makosa ya kuua kwa kukusudia. Kosa la uharamia siyo moja ya makosa yanatoa adhabu hiyo. Lakini kama huyu haramia ataua mtu wakati akifanya kitendo kile kosa lake halitakuwa uharamia, kosa lake litakuwa ni kosa kubwa la kuua kwa kukusudia, adhabu yake ni kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba wapo Watanzania wenzetu wanaofikiria kwamba adhabu ya kifo si adhabu na irekebishwe. Lakini vile vile wapo Watanzania wenzetu ambao kwa nia nzuri kabisa wanafikiri adhabu hii ni adhabu nzuri na iendelee. Utaona wakati Watanzania wetu walemavu wa ngozi walipokuwa wanauawa ovyo ovyo *reaction* ya Watanzania inaeleweka.

Kwa hiyo, hili jambo la mchakato ni jambo la majadiliano na si suala la Serikali kukimbilia kuleta Muswada hapa kusudi kuibadilisha adhabu hiyo. Waacheni Watanzania ndio watakaoamua hatma ya adhabu hiyo. Katika adhabu ambazo nilikuwa natoa machozi nilipokuwa Jaji ni adhabu ya kifo ya kumhukumu mtu afe. Lakini nimefungwa mikono na sheria. Kwa sababu siwezi kueleza hisia zangu, naeleza hisia za Watunga Sheria ambao ni Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Mwakyemba na wengine wamesema kwamba tufikirie kumuondoa Katibu Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye ile sheria ya Msajili, ni wazo zuri, lakini tutashauriana na wenzetu wa Zanzibar kwa sababu wao wanafikiria kwamba Katibu Mkuu wa Hazina wa Zanzibar atalinda maslahi vizuri zaidi akiwa Mjumbe wa bodi hiyo. Kwa hiyo, tutazungumza nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Sheria ya Magazeti, Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewe dhana tu kwa sababu sidhani kama tunapishana. Wale waliochangia kwa maandishi, akiwemo ndugu yangu Mbunge mwenzangu kutoka Jimbo la Ikulu na pia Mheshimiwa Fatma Maghimbi. Tunachofanya hapa hili suala la washauri, Mahakamani zinapokuja kesi za kwenye Magazeti tunachofanya ni kwamba sheria haifanyi kuwa ni lazima wakae lakini Mahakama yenyewe ikiona kama kuna ulazima washauri hao kuwepo basi itaagiza wakae. Au kama watu ambao wamepeleka mashauri hayo mahakamani wakiona wanawahitaji washauri wa mahakama watasema hivyo na mahakama itaridhia. Kwa hiyo, hili suala si la kuondoa au kuvibana vyombo vya habari kama ni hatua ya Serikali kuvibana vyombo vya habari na mengine ambayo mmeniandikia. Hatubani vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Washauri wa Mahakama wataendelea kuwepo katika Mahakama za Mwanzo na ambao ushauri wao unambana hakimu. Watanzania kukaa na Majaji katika kesi za mauaji na pia Watanzania kukaa katika kesi katika Mahakama ya Biashara kwa kesi zile ambazo zinawahitaji ambazo Jaji au Mawakili wanafikiria kwamba ni bora washauri hao wawepo. Hatuwaondoi kwa sababu tunajua ni njia mojawapo ya kuwashirikisha Watanzania wenzetu katika utoaji wa haki. Kwa hiyo, ni suala la sera.

Tunachofanya hapa ni kuipa tu Mahakama uamuzi. Kama ukihitaji suala hili linahitaji kushauri ruhusa. Mawakili na wateja wao wakiona kwamba shauri hili linahitaji Mshauri wa Baraza wataiambia Mahakama na Mahakama haitakuwa na uwezo wa kusema hapana. Kwa hiyo, tunachokataza hapa ni kwamba ni lazima wakae. Kwa sababu wakikaa wanakaa watatu. Kama mmoja hayupo shauri haliendelei. Inawezekana umesikiliza ushauri amebaki shahidi mmoja, huyo mmoja labda haji inabidi uahirishe. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba ni vizuri haki pia itendeke kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha naye amezungumzia juu ya ile sheria ya adhabu kuhusiana na uharamia katika Bahari Kuu. Anasema kwa sababu ya ujanja wa maharamia hawa ni vizuri na sisi pia tukawa wakali. Ninachosema ni kwamba ni hatua kubwa tuliyofikia, kwanza kwenda kwenye *issue* ya *extra teritorial* kwenda nje ya mipaka ya nchi, si suala dogo, ni suala kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwadini Jecha pia amezungumza kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba ofisi ya Msajili ipewe mamlaka kamili ya utendaji ili asimamie vema na ipasavyo usimamizi wa ubinafshaji na ofisi hiyo ipewe fedha za kutosha. Nafikiri Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha kwa kweli ushauri wako ni ushauri mzuri sana na tunaupokea. Nafikiri Waziri naye yupo hapa anasikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mhandisi Stella M. Manyanya nakushukuru sana kwa kunipongeza lakini pia naomba ushiriki katika ibada ile ya asubuhi ambayo kila siku Spika anaizungumzia hapa Dua la Kuliombea Bunge. Kwa sababu nafikiri ndiyo tunaanzia hapo na tumtangulize Mungu katika mambo yote. Ni kweli kwamba nitaendelea kumsaidia Rais Bungeni kwa kadri ya uwezo wangu. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Manyanya anazungumzia juu ya hii Sheria ya Mabenki. Anatambua utendaji mzuri wa Mabenki katika baadhi ya maeneo, lakini anakerwa sana na misongamano ya Benki. Anasema Mabenki yanajilimbikizia faida bila kuboresha miundombinu na hivyo kusababisha misongamano kwenye mabenki na watu badala ya kufanya shughuli zao wanatumia muda mwingi huko benki. Mapendekezo yake ni kwamba mabenki yabanwe kwa kuongeza kifungu cha adhabu ya faini kama hawajafikia kiwango fulani cha huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kila tatizo linatatuliwa na sheria kwa sababu wewe na benki yako umeingia mkataba na kama unaona benki haitekelezi upande wake ruksa ziko sheria nyingine ambazo zinaweza kusababisha ukadai haki yako hiyo Mahakamani. Lakini labda ni vizuri nitumie nafasi hii pia kuwaomba wenzetu wa mabenki wafanye jitihada za kuwafanya Watanzania wenzetu wasitumie muda mwingine sana benki kwa sababu ambazo wanaweza kuzitatua wenyewe. Lakini pia kuwaomba Watanzania wenzetu watumie *ATM*, mashine za kuchukulia fedha badala ya kwenda kukaa kwenye mistari. Nasikia kwamba hazifanyi kazi, kwa hiyo, mabenki msikie kwamba hazifanyi kazi, mchukue hatua za kuzirekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo amechangia Mheshimiwa Manyanya ni kuhusu huduma za jamii. Anauliza kama Vyama vya Siasa navyo vinahusika kwenye kifungu cha 7 cha Sheria ya Uchaguzi kuhusu vikundi vile. Jibu ni rahisi ni kwamba ndiyo, weka gharama za vikundi hivyo na usipoweza sheria ya gharama za uchaguzi iko wazi utaenguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia pia suala la kanuni nafikiri siyo suala la Muswada huu. Lakini namshauri ashiriki kwenye kuzirekebisha hizo kanuni ili aweze kufahamu jinsi zinavyofanyakazi. Ushauri wake tunaupokea kuhusiana na kanuni. Lakini pia namwomba ashiriki kuziboresha si sehemu ya marekebisho tunayofanya.

Halafu Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga anazungumzia marekebisho kwenye Benki Kuu anakubaliana na sisi, nakushukuru sana. Lakini kama walivyo Wabunge wengine anashauri kwamba Waheshimiwa Wabunge waondolewe kwenye Bodi kama ilivyo kwa Makatibu Wakuu. Sababu anazotoa ni kwamba Waheshimiwa Wabunge mnawanyima watumishi ufanisi wa kuchangia mawazo kwenye vikao na pia kuchanganya utendaji na utungaji wa sheria. Nafikiri suala hili pia Mheshimiwa Kabwe Zitto amelizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu yako wazi lakini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria Mkuu mwenyewe si kambare, tunafuata utaratibu na haya masuala ya ugawaji wa mamlaka kwa kweli nilishasema kwamba ni vigumu sana kufanya *a complete separation of powers,* labda kuna mambo mengine ambayo Wabunge wakiwemo kwenye mashirika hayo inasaidia. Lakini labda kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri kwamba wakati wanapofanya uteuzi wa wajumbe katika bodi hizo waangalie uelewa wa Wabunge wote na wasipendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga nakushukuru pia kuhusiana na mchango wako kuhusu Sheria ya Magazeti. Lakini nitofautiane na wewe kwamba lengo letu si kuhatarisha uhuru wa vyombo vya habari, kutoa habari na uhuru wa wananchi kupata habari. Unauliza swali kwamba vyombo vya habari vinapotendewa uovu kwa mfano, kuvunjiwa vyombo vyao kwa mfano kamera ni hatua gani zinazochukuliwa? Labda nitumie nafasi hii kuwaomba wote wanaohusika katika utekelezaji wa sheria. Kama mwandishi wa habari anafanya kitu ambacho kinaonekana kama ni jinai tutumie utaratibu mzuri wa kumdhibiti badala ya kumvunjia vyombo vyake anavyotumia. Kama ukifanya

vinginevyo basi sheria itachukua mkondo wake. Lakini nawaomba watendaji wawe wavumilivu pia wa kujizuia katika utekelezaji wa kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa Ali Khamis Seif naye anashauri, Wabunge nao waondolewe kwenye bodi. Lakini ana suala la Kikatiba kwamba je, wale maharamia watakaokamatwa huko Zanzibar itakuwaje, wataletwa bara kwa ajili ya kushughulikiwa? Tunachozungumzia hapa ni uharamia katika Bahari Kuu, Bahari Kuu haina mwenyewe kwa mujibu wa sheria za Kimataifa. Sasa mtu anayefanya uhalifu pale ndiyo huyo tunayemlenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaofanya kwenye *territorial waters* nafikiri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Serikali ya Muungano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar wanaweza kukubaliana namna ya kuishughulikia *issue* hiyo. Sidhani kama kutakuwa na mgongano kwa sababu tunazungumzia maharamia wa Kisomali. Sasa nitashangaa kama wenzetu Tanzania Bara, Zanzibar itakuwa na uwezo wa kuwa-*prosecute,* ninyi muwang'ang'anie au Zanzibar kuwang'ang'ania hao na *vice verse*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mwingine wa Mheshimiwa Ali Khamis Seif ni kwamba huyu Msajili wa Hazina anapokuwa na mamlaka ya kuamua mishahara ya watumishi wa Mashirika ya Umma basi asiwe anawabana sana. Nafikiri ni mchango mzuri tutauzingatia.

Halafu Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu unapendekeza kwamba sheria ya *Freedom of Information Act* iletwe hapa Bungeni badala ya marekebisho haya ya kuondoa washauri wa Baraza. Kama nilivyosema Serikali haina sababu wala nia ya kuvibana vyombo vya habari kwa kuwaondoa hawa Washauri wa Baraza katika kesi za magazeti.

Kuhusiana na sheria hii ya *Freedom of Information Act* mchakato unaendelea na *Inshallah* mwaka kesho kwenye Bunge lijalo la miaka mitano tutaangalia uwezekano wa kulileta hapa Bungeni. Kwenye jambo hili nafikiri Mheshimiwa Ladhu na Serikali mko pamoja kwamba iko haki ya wananchi kupata habari na sisi kama ni Serikali na Serikali hii ambaye mwanasheria wake ambaye ni Serikali ya CCM ndiyo lengo lake kuwafanya wananchi wapate habari kwa sababu ni haki ya msingi. Mimi si mwana CCM lakini Serikali hii ya CCM ambayo mimi ni Mwanasheria wake ninaifahamu italeta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Mheshimiwa Lubeleje kwamba tumefanya masahihisho makubwa katika uchapaji na tumezingatia pia ushauri wa Kamati. Lakini ni rahisi kusema tumezingatia, naomba kutumia nafasi hii kuwashawishi waandishi wa Sheria kuhakiki hati zao kabla hazijaletwa mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua nafasi hii kuwaomba watumishi wote wa umma popote pale walipo, kuhakiki barua na hati nyingine za Serikali kabla hazijasambazwa kwani tabia na umahiri wa mtumishi unaweza kufahamika kwa makosa yaliyoko kwenye hati au barua, tunaomba tuondoe haya makosa madogo ya uandishi

ambayo hatutegemei kuyafanya. Mheshimiwa Lubeleje nakushukuru sana kwa maoni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatuma Maghimbi alizungumzia kuhusiana na Wazee wa Baraza, nimeshajibu na pia nimetoa angalizo hili kwamba Serikali haina nia ya kubana habari na kama nilivyosema Washauri wa Mahakama wataendelea kukaa katika Mahakama nyingine kama ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kwamba, Sheria ya Habari bado ipo jikoni, mchakato unaendelea. Ushauri wako kwamba Msajili wa Hazina afanyiwe upekuzi mkali, *vetting* ili kuhakikisha hana sura ya ufisadi, ni ushauri mzuri tumeupokea, lakini sura ya ufisadi siifahamu ikoje, lakini imeeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mabadiliko ambayo umesema kwamba kazi ya kutunga Sheria ni ya Bunge na Serikali isiingize tafsiri tofauti na maamuzi ya Bunge. Ni kweli, nimesikia, hiyo ni sauti ya mama na mimi naipokea lakini niseme kwamba jambo hili limefanyika na Maafisa wa Bunge na Maafisa wa Ofisi yangu, nimechukua msalaba na nimekiri kwamba hili limefanyika lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu nilishatoa maelezo kwake na akakubaliana na sisi, ni kwa nia njema kabisa wala hatukuwa na hila. Nakushukuru sana mama. Najua ulinilea wakati nikiwa pale *University* na unaelewa kwamba mpaka sasa nina adabu ile ile niliyokuwa nayo pale mwanzo. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Zitto Kabwe nakushukuru sana kwa mchango wako mzuri ndugu yangu na naona kuna wazee wanakuvutia lakini nakushauri, Kigoma ni kwema kwa sababu titi la mama ni tamu hata kama la mbwa. Umeshauri kwamba Makatibu Wakuu wote watoke ni kweli ndio sera na tulichosema hapa ni kwamba Sheria inayohusika sasa hivi hapa, ni Sheria inayomhusu Katibu Mkuu, Hazina. Wengine wale Sheria zao zitakapokuja zitashughulikiwa lakini tulishawatoa kwenye yale mashirika mengine ya Serikali kwa mfano, *agencies* hawapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Wabunge kwa kweli jamani, eleweni kwamba hili suala la *separation of powers*, msome vizuri, *separation of powers*, mimi ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hali ya kawaida ningetakiwa kuwasikiliza sana wenzenu wa CCM, lakini mnajua ninavyofanya. Ku-*balance* hili ni vigumu sana. Namshukuru dada Estherina Kilasi, enhee, huyo huyo, kwa ushauri wake ule alioutoa kwamba uwezo ni muhimu zaidi kuliko chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hilo ni sawa sawa kaka yangu umeniomba niwe mwangalifu kwenye haya, ni kweli lakini narudia kwamba mimi sio kambare, nafuata Kanuni na Sheria. Mheshimiwa Alhaji Missanga nakushukuru sana kwa yale

mambo mengine uliyosema, lakini kwa sababu hayahusiki na Muswada huu nafikiri utakapofika tutachangia. Ni wazo zuri la akiba kwamba ni vizuri kuangalia mbele ya safari hasa haki za wazee, leo uko kijana, kesho utazeeka ni lazima kuwe na utaratibu wa namna gani ya kuhifadhi wazee. Kwa sababu nakumbuka wote hapa mlikuwa vijana na wengine tulikuwa *national service* kule tunavaa bukta, tunakimbia sana, siku hizi naona wengine hawawezi. Ni wazo zuri lakini wakati wake ukifika tutalizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paulo Lwanji namshukuru sana amezungumzia kwamba Sheria ziendane na wakati na sisi tutajitahidi kuleta hizi Sheria. Tunapata ugumu wa kutengeneza *Legislative programme* kwa sababu ya mambo mengine ambayo huwezi kuyafahamu katikati ya njia, lakini tutatengeneza *Legislative programme* kusudi tujue ni Sheria ngapi tunaweza kuzifanyia nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amezungumzia adhabu ya kifo na mimi nazungumza kwamba, tuwe makini sana jamani kwenye hili, tusiwe na haraka sana kusema tufute adhabu ya kifo. Ni vizuri kusikia mijadala ya Watanzania wenzetu na *issue* ya uharamia, hii ya Samaki sio ya uharamia, kwa jinsi ya Sheria hii tafsiri ya uharamia yaani *piracy* imetajwa kwenye Sheria ya Kanuni ya Adhabu na inahusu wale ambao wanashambulia meli kwa ajili ya kupata faida. Ni watu kwenye meli binafsi au meli ambazo ni za Serikali, lakini kama waliomo kwenye meli hizo za Serikali wameihasi hiyo Serikali, hao wanaweza kuwa ni *piracy* pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu ya kifo inayopendekezwa kwenye Sheria hii nashauri kwamba kwa sasa tufanye adhabu ya kifungu cha maisha tu, kwa sababu haya sio makosa ambayo tunaweza kusema watu wanyongwe. Lakini vile vile kwa sababu makosa haya yanafanyika kwenye Bahari kuu ni vizuri pia tuzingatie Sheria za Kimataifa ambazo nyingi zinasema adhabu ya kifo hii isitolewe, lakini sisi kwetu pamoja na hayo, akiua mtu huko, akifika hapa habari sio *piracy* tena, habari ni kuua kwa kukusudia na ikidhibiti basi adhabu yake ni kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cheyo namshukuru, mimi ni msikivu kwa sababu mimi pia ni mtoto wa mkulima na mchungaji. Hili suala la dhamana na deni la Serikali kwamba lifanyiwe kazi na Msajili wa Hazina, pendekezo ni zuri lakini ipo Sheria, ile Sheria ya Madeni na Mikopo ya mwaka 1974 iliyotungwa na Bunge ambayo inasimamia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu msajili kazi yake tunaomba tumwelekeze kwenye *issue* hii ya mashirika ya Umma. Kwa sababu ukimrundikia tena yeye kufuatilia madeni na ile *formula*, atakuwa anafanya hiyo tu na itam-*hog down,* ile nyingine tuiachie mamlaka ile inayohusika isimamie ile Sheria ya madeni na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi amesema kwamba, Msajili wa Hazina awe *independent*, ni sauti yake mama, ni sauti ya busara na pia ametoa angalizo kwamba msajili aangalie zile posho za Wajumbe wa Bodi, ni kweli baadhi ya

Bodi posho zao ni kubwa sana na wengine posho ndogo ingawa msingi wa kufanya hizo posho ni mapato ya Bodi lakini *at least* kuwe na *equity*. Nachukua ushauri wake kwamba tuangalie Sheria ambazo zinahitaji marekebisho, kwa mfano, ile Sheria iliyotajwa ya Hifadhi za Taifa, na naomba kumwarifu kwamba nitafanya hivyo na kama tutaona umuhimu hatutasita kuleta marekebisho hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio kwa wastani mambo ambayo nimeyasikia, lakini kuna moja ambalo pengine ni vizuri tukalirekebisha na alilizungumzia Mheshimiwa Zitto Kabwe, tumeondoa ile iliyokuwa sehemu ya 17 kwenye Muswada ambao ilikuwa na Ibara za 41 na 42 na badala yake tukaweka mpya na Ibara zinazoingizwa hapo zinastahili kuwa hapo ni 41 na 42 na sio 43 na 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ullisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya**
**Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010**
**[*The Written Laws Miscellaneous Amendment)***
***(No. 2) Bill, 2010]***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati Mwanasheria Mkuu anajibu juu ya mojawapo ya kazi ya Msajili wa Mali ya Serikali, alisema kwamba tusimuhusishe na *guarantees* au dhamana za Serikali.

Lakini kwenye Ibara hii, *investment* mahali popote pale pamoja na Serikali ni pamoja na *guarantees* au dhamana inayoweka kwenye shirika hilo. Sasa ananiambia kwamba tuyaachie mamlaka zingine, ni mamlaka gani katika Serikali pamoja na ile sheria iliyopo ya *guarantees* na nini hakuna mamlaka iliyotajwa inayohusika kuangalia *investment* ya namna hii ambayo ni *guarantees* na nilimwambia kwamba ni kubwa mpaka inakwenda karibu bilioni 569, zote hizi hazina mwangalizi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba katika Ibara hii mojawapo ya kazi au *investment* ingepaswa kuwa na *broad term definition* iki-*include guarantees* za Serikali katika mashirika mbalimbali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kwa sababu ukiangalia majukumu kwa mfano haya ya kama shirika linakopa na linapata *guarantee, definetly* nilichokuwa nazungumzia ni ile *guarantee* ambayo pengine ni *foreign* au *local*, lakini ina-*guarantee* na Hazina, lakini kwenye sheria kama mashirika haya yanafanya hivyo *definetly* itakuwa ni kazi yake. Nashukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 39(a)
Ibara ya 40
Ibara ya 40(a)

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

Ibara ya 42

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010 [*The Written Laws Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2010]***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa mabadiliko ya Sheria Mbalimbali No. 2 wa mwaka 2010[*The Written Laws Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2010]* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali No. 2 wa Mwaka 2010 [*The Written Laws Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2010]* kama ulivyorekebishwa sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu, hoja imetolewa na imeungwa mkono**.** Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii sasa naomba niwahoji, wale wote ambao wanakubaliana na Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010 [*The Written Laws Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2010]* wasme ndio, wale wote ambao hawakubaliani waseme sio. Asante sana wote wamekubaliana kwa hiyo, Muswada umepitishwa rasmi na kwa hiyo, utaenda kwenye hatua yake nyingine ambayo ni ya kutiwa saini na Mheshimiwa Rais. Katibu.

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, sasa nadhani hatua zote zitakuwa zimeshakamilika, sasa labda kwa sababu hapo awali nilizungumzana Mheshimiwa Waziri

ambaye Muswada wake unafuata kama muda tulionao yeye utamtosha kwa ajili ya kuwasilisha, sasa kabla sijamwita Katibu kwa ajili ya hatua hiyo, labda nimsikie Mheshimiwa Magufuli kama muda tulionao utamtosha ili tuweze kuendelea.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa muda uliobaki ni mdogo na watu tuna njaa, nafikiri tukale kwanza halafu tuje kwenye kipindi kingine. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

Kumradhi kwa ombi hilo, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anayefuata kwa muda uliobaki hatoweza kuwasilisha hoja yake, nachukua nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili ambapo Mheshimiwa Waziri atakuja kuwasilisha hoja yake.

*(Saa 6.40 Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010**
***(The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010)***

**Muswada wa Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo wa Mwaka 2010 *(The Grazing Land and Animal Feed Resources Bill, 2010)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tulipofika mwisho wa wiki iliyopita, Mheshimiwa Waziri mtoa hoja aliomba Miswada hii irejee katika Kamati ili iweze kufanyiwa kazi tena na nimearifiwa kwamba kazi hiyo imefanyika. Kwa hiyo, wajibu wangu sasa ni kumwita Mwenyekiti wa Kamati aweze kutupa taarifa ya kazi iliyofanyika kwenye Kamati na baada ya hapo ndiyo tutamwita mtoa hoja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO – MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, ili niweze kuwasilisha taarifa fupi ya Kamati yangu kuhusu mchakato wa Miswada ya Mifugo iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Aprili, 2010, wakati wa majadiliano Bungeni juu ya Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo na Muswada wa Sheria Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Mifugo, Serikali iliomba kwamba Miswada hiyo irejeshwe kwenye Kamati ili kujadili mambo kadhaa ambayo yaliibuka

wakati wa majadiliano. Bunge lilikubali maombi ya Serikali na Kamati yangu ilikutana tarehe 18 Aprili, 2010, kutafakari masuala yaliyohitajika kufanyiwa kazi. Baada ya kazi hiyo kukamilika, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 87(6), napenda kutoa taarifa ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja zifuatazo ambazo zilikuwa zinahojiwa. Kwanza, ni usajili wa mifugo. Hoja ya kwanza, ilihusu kuondoa masharti yote yanayohitaji mfugaji kusajili mifugo yake. Katika majadiliano, Kamati imeridhika kwamba mfumo unaopendekezwa wa kuanzishwa kwa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo, hauwezi kufanya kazi bila kuwepo kwa utaratibu wa kusajili mifugo. Hata hivyo, Kamati imeridhika kwamba muda wa kutosha wa maandalizi ya utekelezaji unahitajika. Kamati pia imeridhika kwamba kipindi cha mpito cha miaka mitatu kilichopendekezwa na Serikali kinatosha kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa uhamishaji wa mifugo iliyozidi uwezo wa eneo la malisho. Hoja hii ilikuwa kuondoa kifungu kinachoweka amri ya kuondoa mifugo iliyozidi kwenye eneo kama ilivyokuwa awali kwenye Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali na Vyakula vya Mifugo. Kamati imeridhia marekebisho ya Kifungu cha 20 yenye kumpunguzia madaraka Mkaguzi kwa kutoa *notice* ya miaka mitatu ili mfugaji aweze kufuga kulingana na uwezo wa ardhi. Endapo mfugaji atakuwa hajakamilisha zoezi katika kipindi hicho, atapewa nyongeza ya miaka mitatu zaidi. Kanuni zitakazoandaliwa chini ya Kifungu hiki, zitaelekeza taratibu za kuweka mifugo kulingana na uwezo wa ardhi ya malisho.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, ilikuwa ni muda wa maandalizi na utekelezaji. Hoja hii ilihusu muda wa utekelezaji wa Sheria hizo na kwamba muda zaidi unahitajika ili Serikali itoe elimu ya kutosha kwa jamii ya wafugaji na wananchi kwa ujumla. Aidha, ilielezwa kuwa Serikali pia inahitaji muda wa kutosha ili kuandaa miundombinu kwa ajili ya matumizi ya mifugo. Kutokana na umuhimu wa kuwepo muda wa kutosha, Kamati imekubaliana kwamba muda wa miaka mitatu wa maandalizi, unatosha. Katika muda huo, masharti yanayohusu usajili wa mifugo yatatekelezwa lakini hayatahojiwa na Mkaguzi wala Mahakama. Vile vile muda huo utawezesha Serikali na Mabaraza ya Vijiji kutenga maeneo ya malisho ya mifugo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 yaani *The Land Use Plan Act, 2007.* Muda wa mpito umewekwa katika Muswada kupitia Jedwali la Nyongeza Na. 2 la Marekebisho ambalo Waheshimiwa Wabunge watakuwa wamekwishagawiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne, ilihusu tafsiri ya baadhi ya maneno na Waheshimiwa Wabunge walipendekeza kuongeza tafsiri ya baadhi ya maneno kama *traceability bridge* na *traceability depth* yenye kuelezea ubora wa mfumo wa *traceability.* Kamati imeridhia kuingizwa maneno haya katika Kifungu kinachompa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni Ndogo kama yalivyoingizwa kwenye Jedwali la Nyongeza Na.2 la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano, ilikuwa ni mapendekezo ambayo yalikuwa yameshawasilishwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwenye Jedwali la

Marekebisho na Mapendekezo hayo yalipokelewa na kimsingi Kamati imekubaliana kwamba mambo mengi yaliyojitokeza katika majadiliano hapa Bungeni yamefanyiwa kazi na Serikali kupitia Majedwali ya Marekebisho matatu ambayo yamekwishawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya, Kamati yangu inashauri kwamba Bunge lako Tukufu liendelee kukamilisha hatua zilizobaki na kuupitisha Miswada yote miwili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri kuweza kutoa maelezo kuhusu Muswada huu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, utakumba kwamba tarehe 15 Aprili, 2010 wakati wa majadiliano hapa Bungeni juu ya Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Mifugo. Serikali iliomba Miswada hiyo irejeshwe kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ili kujadili baadhi ya mambo ambayo yaliibuka wakati wa majadiliano na Bunge lako Tukufu lilikubali maombi ya Serikali. Kamati ilikutana tarehe 18 Aprili, 2010 kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafakari masuala yaliyohitajika kufanyiwa uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje kwa kupokea na kujali hoja, kupokea maoni na ushauri wa wadau kuhusu Miswada hii. Aidha, mapendekezo, ushauri na maoni yamezingatiwa na kufanyiwa marekebisho katika baadhi ya vifungu vilivyozua mjadala.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbusha kwamba mchakato wa kuboresha sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera ya Mifugo, ulianza muda mrefu. Napenda tu nitoe taarifa kwa haraka haraka kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia 54 nimeshawatambua kabla sijaiondoa Miswada hii na baadhi ya hoja za jumla jumla nilizizungumzia.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nieleze tu kwamba nchi yetu ina changamoto kubwa sana katika sekta ya mifugo hasa kwa kuzingatia kwamba ukubwa wa eneo letu la Tanzania ni hekta *949,000 square kilometre* lakini hadi sasa hivi eneo ambalo limeshatengwa kwa ajili ya wafugaji ni hekta 1,000,000.3 pamoja na ukweli kwamba hekta zinazofaa kwa ajili ya mifugo ni zaidi ya hekta milioni 50.

Mheshimiwa Spika, lakini ieleweke pia kwamba tangu tupate uhuru, idadi ya mifugo ilikuwa kama milioni nane wakati idadi ya binadamu ilikuwa milioni tisa. Kwa sasa hivi, idadi ya watu ni milioni 40 na katika mifugo pamekuwa na ongezeko kubwa.

Kwa takwimu tulizonazo kwa sasa hivi tuna ng'ombe zaidi ya milioni 19.1, mbuzi zaidi ya milioni 13.6, kondoo zaidi ya milioni 3.6, nguruwe milioni 1.6, kuku milioni 57, mbwa milioni nne, mbali ya wanyama wengine kama pundamilia, bata mzinga, sungura, na kadhalika. Eneo tulilonalo wakati tukipata uhuru liko vile vile wakati idadi ya matumizi ya ardhi inaongezeka ndiyo maana sekta ya mifugo, sekta ya kilimo na sekta zingine, zina changamoto kubwa katika kuleta mabadiliko ya kweli katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba nchi yetu imekuwa na mifugo mingi na ni ukweli kwamba katika Afrika, nchi yetu ni ya tatu baada ya Ethiopia, Misri pamoja na Sudan lakini ukweli ni kwamba sekta hii ya mifugo katika *contribution* ya kukua kwa uchumi kwenye *GDP* imekuwa ikichangia kwa asilimia 4.7 tu kwa zaidi ya miaka mine ukilinganisha na nchi nyingine kama Botswana ambayo yenyewe ina mifugo milioni 1.8 lakini sekta ya mifugo imekuwa ikichangia kwa asilimia 30. Nchi ya Namibia ambayo ina mifugo milioni 2.2, sekta ya mifugo imekuwa ikichangia kwa asilimia nane. Hata nchi kama Ethiopia ambayo ndiyo wanaongoza, wana mifugo karibu milioni 38, sekta ya mifugo imekuwa ikichangia kwa asilimia 18.8. Nchi kama Sudan ambayo yenyewe ina mifugo karibu milioni 35, sekta ya mifugo imekuwa ikichangia kwa asilimia 20. Hata majirani zetu Kenya ambao wao wana ng'ombe milioni 11.5, sekta ya mifugo imekuwa ikichangia kwa asilimia 12. Hata Uganda ambao wana ng'ombe milioni 6.2, sekta ya mifugo imekuwa ikichangia kwa asilimia 5.2, sisi asilimia 4.7 kwa miaka zaidi ya mitano. Kwa hiyo, hii ndiyo *challenge* na ni suala kubwa ambalo sisi kama Serikali, sisi kama wadau wa mifugo, sisi kama Watanzania, tunatakiwa tuliangalie, ni kwa namna gani sekta hii ya mifugo, pamoja na kwamba tuna mifugo mingi, imekuwa haichangii katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na hatua mbalimbali za Serikali katika kufikia haya malengo ambayo leo yamenifanya niwasilishe Miswada hii, kwa sababu tatizo kubwa limekuwa kutokuwa na Sheria ambazo zingeweza kutusaidia kufika hapa tulipo. Kwa sababu ya Sheria zetu hata wawekezaji imekuwa vigumu kuja kufungua viwanda vyao kwa sababu hawezi akaja akaanzisha kiwanda hapa wakati atakapoanza kuchinja nyama, nyama zake hazitapata katika soko la dunia. Hawezi kuanzisha kiwanda cha maziwa, wakati maziwa ya Tanzania huwezi ukayauza nje ya nchi kwa sababu ya Sheria zetu. Huwezi ukaanzisha hata kiwanda cha kuku au cha mayai wakati mayai yale huwezi ukayauza nje kwa sababu ya Sheria zetu. Hii imekuwa ni kero kubwa kwa Watanzania katika kuchangia kwenye pato la Taifa ndiyo maana utaona pamoja na kwamba tumekuwa na mifugo mingi, sisi tumeendelea kuwa masoko ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya ngozi ambapo kwa mfano mwaka jana tuliuza ngozi zaidi ya milioni 5.6 zilituingizia karibu shilingi bilioni 30 hadi 32 hivi lakini asilimia 80 ya ngozi zote tuliziuza kama *raw material* na nyingi zimepitia Kenya. Katika nchi yetu, pamoja na kwamba tuna ng'ombe wengi, huwezi ukauza maziwa, hata vile viwanda vilivyokuwepo ambavyo wamejaribu kuanzisha, vimeshindwa kuuza maziwa nje nchi kwa sababu ya Sheria zetu. Kwenye nyama yenyewe ndiyo usiombe, huwezi ukauza nyama kwa sababu ya Sheria zetu na ndiyo maana tunasema kwamba pamekuwa na michakato mingi katika kuhakikisha kwamba tunafikia hatua ambayo itatuwezesha kuondoka mahali tulipokuwa ili twende mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye mwaka 2001, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Awamu ya Tatu, aliitisha mkutano wa wadau wote wa sekta ya mifugo mjini Arusha, wakiwemo Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na kadhalika. Ule mkutano ulikuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mkapa kwa siku tatu kujadili masuala ya mifugo. Katika michango mbalimbali iliyochangiwa na Waheshimiwa waliohudhuria katika kikao hicho, kuna masuala mengi ambayo yalipendekezwa na katika mapendekezo hayo ndiyo mwaka 2006 pakaanzishwa Sera ya Mifugo ya mwaka 2006. Baada ya Sera ya Mifugo kupitishwa, pamefanyika mikutano mbalimbali ambayo iliwahusisha viongozi wa Kitaifa mpaka na wadau wa chini kabisa katika kuzungumzia ni kwa namna gani tunaweza tukaondokana na tatizo la kuwa na mifugo mingi lakini ambayo haichangii kwenye pato la Taifa bali kuongeza migogoro.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na *TIRDO* pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, ilifanya mkutano wa wadau pale *Saint Gasper*, *Dodoma* na mkutano huo ulihusisha pia *NGO* pamoja na wadau wengine katika kujadili suala la mifugo. Mkutano mwingine ulifanyika mwaka 2008 kule *Land Mark Hotel* kupitia Rasimu ya Mapendekezo ya Sheria. Mkutano mwingine, Wizara kwa kushirikiana na *ICC* ulikuwa *Impala* Arusha, ulihusisha Madiwani, wafugaji wa Mikoa ya Mara, Arusha, Manyara na *NGO* kuzungumzia suala la mifugo Tanzania. Lakini pia palifanyika mkutano kule Bagamoyo ambao ulihusisha Wizara ya Mambo ya Ndani na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Katiba na Sheria wakishirikiana kwa pamoja katika kuzungumzia masuala ya *cattle lasting, Article 5,* masuala mengi ya jumla yalizungumzwa na katika maazimio ya pale walisema *livestock identification and traceability* inaweza ikawa *solution* ya kutoka kwenye matatizo yaliyokuwa yanaikabili nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini Wakuu wa Mikoa wote, ma-*DC*, Wakurugenzi na kadhalika mwaka jana chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda hapa Dodoma, ulifanyika mkutano kuzungumzia masuala ya mifugo tu, palikuwa na mapendekezo mengi na *resolutions* nyingi zilifanyika, wadau wengi walipendekeza kwamba pawepo na Sheria ambazo zinaweza zikatusaidia kuondokana mahali tulipo. Lakini pia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwenye mwaka 2007 kule Arusha alifungua mkutano na Maafisa Mifugo wote, lakini mwaka uliofuatia ulifunguliwa mkutano na Makamu wa Rais ambapo masuala ya mifugo yalikuwa yakizungumziwa. Lakini katika kila mwaka sisi tumekuwa tukifanya mikutano kuzungumzia masuala ya mifugo. Hata mimi mwenyewe tumefanya mikutano kule Sumbawanga, ulikuwa wa wadau wa maziwa, tumefanya mikutano na wadau wa nyama kule Morogoro. Hapa Dodoma mwaka jana tumefanya mkutano na wadau wa maziwa na kadhalika ambapo lengo kubwa ni kuona ni kwa namna gani tunaweza tukaondokana na matatizo haya yanayohusu mifugo.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu haya yote yasingewezekana bila kutungwa kwa Sheria na napenda kwa ruhusa yako ninukuu baadhi ya maneno na maelekezo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, ambayo yako ukurasa wa 29. Katika maazimio na katika maelezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambapo sisi wote tumezunguka na kunadi yanasema, pamoja na kwamba Tanzania ina mifugo mingi sana mchango wa

mifugo kwenye uchumi wa Taifa ni mdogo. Kwa lengo la kuendeleza sekta ya mifugo ili ichangie zaidi ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuongeza kipato cha wafugaji, Serikali ya CCM itaendeleza kwa msisitizo zaidi lengo la kuzingatia zaidi ubora, kuliko wingi pekee katika ufugaji ili kufikia lengo hilo, hatua zifuatazo zitachukuliwa katika kipindi cha mwaka 2005 na 2010. Kwanza, ni kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika viwanda na kuongezea thamani mazao ya mifugo, kama vile ukataji wa nyama, usindikaji wa maziwa na kadhalika. Pia, kuwashawishi Watanzania wale nyama na mayai na kunywa maziwa kwa wingi zaidi. Lakini ni ukweli usiopingika hata ulaji wa nyama na unywaji wa maziwa kwa Watanzania bado uko chini na hii ni kwa sababu hata utengenezaji wa vyakula vyetu una matatizo na ndio maana pia tumeleta hapa sheria ya kudhibiti mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi unaweza ukaenda ukanunua kuku, lakini utakapomchinja yule kuku atakuwa ananuka dagaa tu. Unaweza ukaenda ukanunua maziwa lakini ukakuta asilimia kubwa watu wameongeza maji na badala ya maziwa yale kukusaidia, baadaye unaanza kuharisha na ndio maana udhibiti wa vyakula ni moja ya Muswada ambao tumeuleta hapa na kwa sababu hiyo, hata ulaji wa maziwa kwa sasa hivi, kuanzia mwaka jana tumetoka kunywa lita 40 hadi lita 41 kwa kila Mtanzania kwa mwaka wakati *WHO* wanataka tunywe lita 200 kwa kila mtu anayeishi katika dunia hii kwa mwaka. Ulaji wa nyama katika nchi yetu bado uko chini, tumetoka kwenye kilo 10 kwa kila Mtanzania kwa mwaka hadi kilo 11 kwa kila Mtanzania kwa mwaka wakati *WHO* wanataka tule kilo 50 kwa kila mtu anayeishi duniani kwa mwaka. Ulaji wa mayai nao bado uko chini, ni mayai 69 kwa kila Mtanzania kwa mwaka, wakati tunatakiwa kila mtu ale mayai 300 kwa mwaka, sasa hizi zote ni changamoto. Inawezekana watu wameshindwa kula vyakula hivi kutokana na utengenezaji wa vyakula vya mifugo ulivyo hapa nchini ndio maana tumeleta Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Ilani ya Uchaguzi, inasema pia kufufua na kujenga mabwawa na majosho mapya kwa ajili ya mifugo, kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa kuuza sehemu ya mifugo yao ili wajipatie mapato; kuwahimiza wafugaji kutekeleza Kanuni za ufugaji bora na kwa ujumla kuwawezesha kuingia katika ufugaji wa kisasa, haya hayawezekani bila kuleta Sheria; kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia ufugaji endelevu usioharibu mazingira, haya pia yanahitaji Sheria; kuendelea, kukuza na kuelekeza masoko ya ndani ya mifugo na ya nje ya mazao ya mifugo yetu; kuendeleza mikakati ya kukuza sekta ya mifugo kupitia ugani, tiba, kinga na kadhalika; kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe; kuendeleza na kutenga maeneo ya wafugaji kwa lengo la kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji na kuendelea kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika kwa wafugaji. Haya ndiyo maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005/2010. Sasa kwa kuzingatia maelekezo haya, sisi Wizara na Serikali tulijua kuwa hatuwezi kuyatekeleza haya bila ya kuwa na Sheria na ndio maana tulileta Sheria ili kusudi tuondoke mahali tulipo twende mahali ambapo panastahili kwa maendeleo ya watu wote.

Mheshimiwa Spika, Sheria inapotungwa, ni lazima iwanufaishe Watanzania wote, wafugaji, wakulima, wafanyabiashara, wafanyakazi na kadhalika. Lakini pia tunafahamu

changamoto kubwa zinazotupata katika kutunga Sheria na hasa unapotunga Sheria inayohusu binadamu. Lakini hizi zote ni changamoto na mimi ninaamini kwamba sheria hizi zikipitishwa, tunaweza tukaleta mabadiliko makubwa sana katika sekta ya mifugo na kufanya sekta hii kuchangia kwenye pato la Taifa kama wenzetu ambavyo sekta hiyo imekuwa ikichangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutokuwa na Sheria hizi, idadi ya mifugo iliyouzwa kwenye minada hapa Tanzania katika kipindi cha miaka miwili ya 2008/2009 ilitoka kwenye mifugo 779,260 hadi 781,230 tu, mbuzi waliouzwa walifikia 623,732 tu, kondoo waliouzwa walifikia 114,564 tu na hivyo kufanya uzalishaji wa nyama kukua kutoka tani 410,706 hadi 422,330 tu ongezeko la 2.8%. Lakini pia tumeuza ng'ombe 3,264 tu, tumeuza kondoo na mbuzi 1,834 tu kwa nchi za Komoro, Kenya, Burundi na Malawi kidogo, nyama zetu hatuwezi tukaziuza katika nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumeuza tani 139.8 tu za nyama ya ng'ombe na tani 35 za nyama ya kondoo na tani 46.7 za nyama ya mbuzi wakati mahitaji, Egypt kwa mfano, inahitaji tani 149,000 za nyama ya ng'ombe, Falme za Kiarabu zinahitaji tani 172,560 za nyama hata Kongo *DRC* hapa jirani wanahitaji tani 23,000 na kadhalika, ukiachia soko lingine la Japan, Europe na kadhalika. Tumeshindwa kufanya haya yote kwa sababu ya Sheria zetu. Sheria zetu haziruhusu kuuza bidhaa hizi kwenye soko hilo na ndio maana siku zote *contribution* ya sekta ya mifugo imekuwa ni chini ambayo ni 4.7% ukilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tulipobadilisha Sheria ya Uvuvi, Na.22 ya mwaka 2005, ilitufanya tuanze kuwauza samaki wetu katika Soko la Ulaya na ndio maana kwa mwaka jana tu, Ziwa Viktoria tu lilituingizia Serikali zaidi ya shilingi bilioni 224 kutokana na samaki tuliowauza nje ya nchi. Lakini pia kutokana na kurekebisha Sheria zetu, imefanya tuwe na viwanda zaidi ya 35 ndani ya *East Africa Community*, Kenya, Uganda na Tanzania, vinavyohusu samaki lakini vimewafanya wakazi wa Mwanza wawe na *circulation* ya shilingi milioni 600 kila siku kwa ajili ya biashara ya samaki. Lakini kwenye upande wa mifugo, sisi tumeendelea kuwa wasindikizaji, Botswana wana ng'ombe 1.8 *contribution* kwenye *GDP* ni 30%, sisi tuna ng'ombe milioni 19.1 *contribution* ya kwenye *GDP* ni 4.7% kwa hiyo, Miswada hii ni muhimu sana katika kuwasaidia wafugaji, wakulima, wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla katika kujenga uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, kupitishwa kwa Sheria hizi pia kutawasaidia sana wafugaji kwa sababu kwa sasa hivi kuna mchakato wa kuanzishwa Benki ya Wakulima na hasa baada ya msisitizo mkubwa unaofanywa na Serikali juu ya Kilimo Kwanza. Hawa wafugaji bila kuwa na Sheria ya Usajili, hawezi akaenda akakopa benki, kwa sababu hata mashamba ya kilimo yanasajiliwa, hata mitumbwi ya kuvulia samaki yanasajiwa. Kwa hiyo, bila ya kuwa na Sheria hii, wafugaji wataendelea kubaki nyuma. Kwa hiyo, hizi ni juhudi za Serikali katika kuwasaidia wafugaji ili twende pamoja katika maendeleo ya nchi, ndio maana tumeleta Muswada huu muhimu kwa faida ya wafugaji na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Miswada hii pia linaendana na Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji, Na.5 ya mwaka 1999, lakini pia na Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi, Na.6 ya mwaka 2007 na ndio maana utaona Sheria hii imeendana sana na Sheria hiyo. Lakini mapendekezo ya Miswada hii pia yanaendana na Sheria ambazo tayari sasa zipo, kwa mfano, Sheria Na.17 ya mwaka 2003 ya Magonjwa ya Mifugo, Sheria Na.16 ya *Veterinary* ya mwaka 2003, Sheria ya Nyama, Na.10 ya mwaka 2004, Sheria ya Maziwa, Na.8 ya mwaka 2004, Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Na.19 ya mwaka 2008, Sheria ya Ngozi, Na.18 ya mwaka 2008. Kwa hiyo, kupatikana kwa Sheria hii ndipo kutakuwa na maendeleo ya kweli na mimi ninaamini kabisa mambo mazuri yanaweza yakafanyika na yakatekelezwa kwa mujibu wa sheria na wananchi wetu kwa pamoja wakaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini ieleweke kwamba katika kipindi chote cha miaka hii yote, pametengwa maeneo ya wafugaji ambayo ni hekta milioni 1.3 tu. Kwa kupitia Sheria hii, Miswada hii ikishapitishwa, tuna uhakika sasa maeneo ya ufugaji yataanza kutengwa ili kusudi kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Ninaamini Miswada hii ni muhimu sana kwa manufaa ya Watanzania wote na ndio maana ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, waipitishe kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, wakati nilipouleta hapa, uliungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi sana lakini pia kulikuwepo na Wabunge wachache ambao walishauri kwamba tuuboreshe zaidi. Kwa sababu Sheria inapotungwa huwa ni Sheria kwa ajili ya watu na ndio maana nilikubali irudi kwenye Kamati ili kusudi tuweze kuyafanyia kazi yale yote ambayo yangeweza kuuboresha Muswada huu. Kwa bahati nzuri, yote ambayo yalikuwa yamejitokeza, tumeyajadili na kukubaliana nayo na kwa bahati nzuri hata kwa taarifa ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na yeye ameeleza.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ambayo yalijitokeza ni pamoja na hoja ya uhamishaji wa mifugo iliyozidi uwezo wa eneo la malisho. Hoja ya kwanza ilikuwa ni ya usajili wa mifugo; Serikali inashauri kwamba mfumo uliopendekezwa kuanzishwa wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo, hauwezi kufanya kazi bila kuwepo kwa utaratibu wa kusajili mifugo. Hata hivyo, Serikali imekubali ushauri wa wadau kwamba pawepo na muda wa kutosha wa maadalizi na hivyo Serikali imependekeza kipindi cha mpito cha miaka mitatu kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa ni uhamishaji wa mifugo iliyozidi uwezo wa eneo la malisho. Tumeleta *schedule of amendment* ya Kifungu Na.20, ambacho sasa kinapunguza hata madaraka ya Mkaguzi kwa kutoa *notice* na kwa sasa hivi atatoa *notice* ya miaka mitatu, halafu ikishapita ile miaka mitatu atatoa tena *notice* nyingine ya miaka mitatu, kwa hiyo, ni miaka sita. Katika miaka sita, sisi wote tutakuwa tumeshachaguliwa, tukarudi, tukachaguliwa tena, ile *notice* itakuwa bado imesimama. Kwa hiyo, hii ni *flexibility* ya Serikali na katika kipindi hicho chote Serikali itakuwa imejipanga vizuri na kujiandaa.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tatau ni muda wa maandalizi ya utekelezaji, Serikali imekubali ushauri wa kuweka muda wa miaka mitatu wa maandalizi. Katika muda huo, masharti yanayohusu usajili wa mifugo yatatekelezwa, lakini hayatahojiwa na Mkaguzi wala Mahakama. Vilevile muda huo utaiwezesha Serekali na Mabaraza ya Vijiji kutenga maeneo ya malisho na kuwekeza katika miundombinu, kwa mfano malambo, mabwawa, majosho, minada na hasa ya kupima kwa mizani, vibanio, masoko na njia za mifugo. Aidha, muda huo utaiwezesha Serikali na Maabara ya Vijiji kutenga maeneo ya malisho ya mifugo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Sheria ya Matumizi ya Ardhi, Na.6 ya mwaka 2007 lakini ndio maana tumeweka ile Nyongeza ya Marekebisho, Na.2 ambayo imetolewa kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ni ilihusu kutolewa tafsiri kwa baadhi ya maneno kama *traceability bridge* na *traceability depth* yenye kuuelezea ubora wa mfumo wa ufuatiliaji, Serikali imekubali ushauri huo na kuuingiza katika kifungu kinachompa Waziri Mamlaka ya kutunga Kanuni, maeneo haya yameingizwa katika Jedwali la Nyongeza la Mapendekezo, Na. 2.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tano ya mapendekezo yaliyomo kwenye jedwali imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, kupitia majedwali ya marekebisho. Kutokana na maelezo hayo yaliyotolewa hapo awali kuhusu hoja hizo, Serikali imeyafanyia kazi na majedwali matatu ya marekebisho yameshagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, napenda kusisitiza kwamba, sheria hizi ni muhimu sana kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji, kuwasaidia wakulima na kuwasaidia Watanzania wote. Nimeeleza changamoto tulizonazo na sisi Tanzania tumekuwa siku zote ni kama wasindikizaji katika maendeleo pamoja na kwamba tuna mifugo mingi katika Afrika na ni watatu lakini tumeona kabisa kwamba *contribution* ya sekta ya mifugo katika nchi yetu, bado iko chini. Ninaamini kwa kupitisha Sheria hizi, tutaweza kwenda mbele na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuondoa migogoro na kujenga uchumi wa Watanzania wote kupitia sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi kuelezea kwa uchache na Sheria hii iko wazi na ni kwa manufaa ya Watanzania wote. Ninapenda kupitia Bunge hili, kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote na ninavyowaona wanatabasamu sasa, nyuso zao ni nzuri, wanafurahi, wapitishe Miswada hii miwili ambayo ni muhimu sana kwa Watanzania. Si vyema sisi Watanzania bidhaa zetu tukashindwa kuziuza nje, tukiuza nje ndipo tuta-*create employment*, tutajenga viwanda, kwa sasa wawekezaji wameshindwa kuja kujenga viwanda hapa nchini kwa sababu wanajua wakijenga kiwanda cha nyama, nyama ya Tanzania haiwezi ikauzwa nje. Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa pamoja kabisa, nikishamaliza kutoa hoja hapa, wote tuupitishe moja kwa moja Muswada huu ili uweze kuleta mafanikio kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Miswada ya Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameshatoa hoja ingawa inahusu Miswada miwili, lakini kwa utaratibu huwa tunapitisha Muswada mmoja baada ya mwingine. Kwa hiyo, nitamuomba sasa Katibu, atamke hatua inayofuata na hiyo itatusadia kuzingatia Muswada wa kwanza wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 *[The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010]'*.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010**
***[The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010]***

**MWENYEKITI:** Kama nilivyotangaza awali, kwenye Kamati ya Bunge zima, tunauzingatia Muswada mmoja kwanza halafu ndio tunakwenda Muswada mwngine baada ya kuupitisha huo. Sasa nitamwita Katibu ili atupitishe kwenye Muswada wa *The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010.*

Ibara ya 1

**MWENYEKITI:** Ibara ya kwanza ina marekebisho na yalikwishawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86, nampa dakika zisizozidi tano ili aweze kutoa hoja yake ya kujenga, kuhusu mabadiliko hayo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Niliwasilisha marekebisho yanayohusu Kifungu 5 na 6 lakini niseme wazi kwamba baada ya kukutana na Kamati na kwa kuzingatia marekebisho ambayo Waziri ameyafanya, kimsingi ninaelekea kuondoa hoja zangu hizo ambazo nilikuwa nimekusudia kufanya marekebisho hayo na hasa baada ya kuona kwamba, katika Miswada hii ambayo inakwenda sambamba kuna eneo ambalo lilikuwa linalazimisha masuala fulani mazito, lakini Waziri ameelezea na yameweza kuondolewa na kuwekwa kwenye lugha fulani ambayo baadaye tutakutana huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, bado ninaomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo kidogo kwamba katika mchakato mzima huu wa kusajili mifugo na suala zima la *identification registration and traceability* kuna eneo ambalo wamebainisha usajili wa makazi na kwa kuwa wafugaji wetu tunaowazungumza ni wachungaji wa mifugo ambao wanahama wakati wa masika kubadilisha makazi yao kufuata malisho, wakati masika wanakuwa hapa, wakati wa kiangazi wanakuwa pale, sasa ukisema unasajili makazi: Je, utaratibu huu Mheshimiwa Waziri atauweka katika kanuni, utaratibu ambao hautakuwa na usumbufu kwa wafugaji hasa wanapofuata malisho katika eneo moja, lakini wakati huo huo kutambua kwamba hali ya hewa inapobadilika wafugaji

wanalazimika pia kutoka sehemu moja kufuata malisho hata nje ya maeneo yale ambayo walikuwa wamejisajili? Waziri atakubaliana nami kwamba wataweka utaratibu mzuri kwenye kanuni atakazozitunga ili kuhakikisha kwamba wafugaji hawatafungwa na mifugo yao na hatimaye kupoteza mifugo katika eneo moja ambalo halitakuwa limepata mvua.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii kwa mujibu wa kanuni ya 38 Mheshimiwea Ole-Sendeka ameondoa hoja yake ya kuleta mabadiliko ila anataka sasa ufafanuzi ikiwa kwenye kanuni suala la usajili makazi ya wafugaji litakaakaaje ili lisiwe na ubumufu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa kukubaliana na Serikali? Nataka kumthibitishia kwamba wakati tutakapokuwa tunaandaa kanuni za Muswada huu tutazingatia hayo ili kusudi sheria hii isije ikawa kero kwa wafugaji na wakulima kwa pamoja.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibaraya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nataka tu kuuliza kwenye Ibara ya 4(2) ambapo kutakuwa na utaratibu wa kuweza kutambua pamoja na kuandikisha mifugo: Je, gharama itakuwaje? Ni nani ambaye ataweza kuchukua gharama ya kufanya shughuli zote hizi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVIVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara hii, Muswada huu gharama zimewekwa kwa watu, kwa maana nyingine kuna maeneo ambapo Serikali itagharamika, kuna maeneo ambapo Halmashauri husika zitagharamika na kuna maeneo ambapo mfugaji kwa kweli lazima agharamamike. Hii ndiyo hali halisi na ndiyo maana sheria hii inaendana vizuri na sheria Na. 6 ya mwaka 2007 ya matumizi bora ya ardhi. Lakini gharama kubwa zitabebwa na Serikali, lakini pia na wadau nao kwa njia moja au nyingine watabeba gharama zao. Ni katika kuzingatia kama hali halisi unapotaka kusajili shamba lako, kwa vyovyote kuna maeneo ambapo lazima utagharamika, unaposajili mtumbwi wako kuna maeneo ambapo lazima kuna kugharamika. Hata kwa sasa hivi kuna usajili wa kimila ambao ng’ombe wanaweka

alama, labda anabandikwa kwenye tumbo hapa anaandikwa Magufuli au anaandikwa Sitta, ile ya kulitengeneza lile la kuchoma moto ni gharama. Kwa hiyo, kuna gharama za aina fulani ndogo ndogo ambayo wahusika watahusika lakini ukweli hili pia linaweza likatekelezwa kupitia kwenye miradi ya *DADPs* ambayo inashughulikiwa kwenye Halmashauri husika.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, ulileta mezani mabadiliko kuhusu ibara ya tisa sijui bado unayo hayo au una...

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ibara ya tisa, mabadiliko yangu yako pale pale. Napendekeza mabadiliko. Niliwasilisha mabadiliko haya kwa kuzingatia kwamba kwenye *section nine sub section three* ilikuwa inaweka adhabu isiyozidi shilingi milioni mbili kwa makosa hayo yaliyotajwa hapo juu, lakini wakati huo huo inasema au kifungo kisichozidi mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona ni vizuri nilete mabadiliko yote mawili kwa upande wa adhabu kwamba milioni mbili ni fedha nyingi sana na hasa unapozungumzia wafugaji ambao makosa mengine yanaweza kuwa ya mbuzi mmoja hujamsajili au ya ng’ombe mmoja, au kondoo mmoja halafu adhabu unayokuja kupewa inakuwa ni uamuzi wa Hakimu. Inaweza ikawa shilingi milioni mbili au isiyozidi milioni mbili. Nikaomba isizidi shilingi laki mbili kwa sababu ya kuzingatia kwamba kosa lenyewe linaweza pia kuwa dogo na kifungo kisichozidi miezi sita kwa sababu nia ni kuanza mambo haya na inahusu ng’ombe, mbuzi na watoto wa mbuzi waliozaliwa. Kwa hiyo, niliona nipendekeze masahihisho hayo kama Mheshimiwa Waziri hatakuwa na pingamizi nitashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kupunguza adhabu zilizopangwa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili ombi la Mheshimiwa Ole-Sendeka, sisi tuliliangalia kwa upana zaidi na ndiyo maana kiwango cha faini kinaanzia zero hadi shilingi milioni mbili. Mahakimu wetu na Mahakama zetu zinazingatia busara sana, hawezi mtu akawa na tatizo la mbuzi akatolewa shilingi milioni mbili.

Lakini tuliangalia pia kwamba mtu anaweza akawa na ng'ombe hata 100 na thamani ya ng'ombe mmoja kwa sasa hivi wanafika mpaka shlingi milioni moja. Sasa ng'ombe mia moja maana yake ni shilingi milioni 100. Sasa kutozwa faini ya shilingi milioni mbili kwanza watakuwa wamemsaidia sana. Lakini tulilizingatia ombi la Mheshimiwa Ole-Sendeka, tukasema katika kanuni tutapokuwa tunaziandaa tutaendelea kuelezea kama ni mbuzi au kondoo faini iwe kiasi gani ili kuweza ku-*accomodate* maombi yake aliyoyatoa Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, nadhani kwa maelezo hayo maana yake sheria inataja kiwango cha juu, sio kwamba inazuia Hakimu kutumia hekima yake kutoza faini ya kiwango cha chini zaidi kulingana na mazingira.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwomba Waziri auone ukweli uliopo kwamba kiwango hicho cha juu alichoweka bado ni kikubwa kulingana na mazingira aliyoyataja na ukizingatia ya kwamba tunazungumza wafugaji bado hatujawawezesha kupata makazi kwa maana ya kuwekeza kwa maana ya kuwa na uhakika na maji katika sehemu inayohusika kuwa na uhakika na malisho.

Lakini inahusu mpaka Mwenyekiti, hata suala kuchinja tu pale ukifanya makosa inahusu hiyo. Kwa hiyo, nilifikiri Mheshimiwa Waziri kama hatakubaliana na kiwango changu hicho ameona kama nimeshuka sana na yeye angeangalia uwezekano wa kutoka hapo alipo maana bado viwango ni vikubwa sana na adhabu hii bado maandalizi hayajafanyika na sheria ni sheria. Kwa hiyo, bado haitamzuia Hakimu hata kwa kosa la huyu mbuzi mmoja au kondoo mmoja maana sijui kanuni zipi zitaandaliwa za kumwambia kosa likiwa la mtoto wa mbuzi, basi faini ishuke kidogo ikiwa ya ng'ombe kumi, basi ipande. Nilifikiri kwamba sijui kama Waziri angeweza kutumia busara za kushuka kwa adhabu hizo kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka tatizo ni kwamba yamo makosa madogo na yapo pia makubwa kidogo. Sasa hata ukishuka zaidi yale makosa makubwa utakuwa umeyawekea adhabu nyepesi, ndiyo maana amejaribu kuyaachia Mahakama labda ifanye itumie hekima zake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwona Mheshimiwa Ole-Sendeka amekubali na nilitaka kusimama kusema hayo hayo kwamba nafikiri *spirit* yetu iwe kuwahimiza wananchi wa Tanzania wenzetu kuheshimu na kutii sheria kwa sababu kama wametii sheria, hilo haliwezi kutokea lakini wasipotii sheria basi sheria ina meno na inauma kote kote.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI**: Umekwishasimama mara mbili.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Basi, kwa hiyo imetosha?

**MWENYEKITI:** Huna nafasi nyingine tena. Kwa hiyo, ningependa kweli tuamue kwa kura sasa kwa sababu kanuni ya 88 inanihitaji nifike mahali tupige kura tu kama badiliko lipite au lisipite.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunatunga sheria. Sheria ikiwa *soft* tu kila mahali hapatakuwa na sheria na patakuwa hakuna sababu ya kutunga sheria. Tunatunga sheria ili mtu aliyehusika na ng'ombe hata 200 hii sheria imguse. Lakini kwa heshima kubwa sana ya Mheshimiwa Ole-Sendeka, nimeeleza kwamba katika kanuni tutatoa ufafanuzi. Kwa hiyo, sheria hii sisi kama Serikali tumeshindwa kuondoa, hivyo inabaki pale pale kuanzia *zero* hadi shilingi milioni mbili au vifungo. Lakini katika kanuni tutaangalia hayo ambayo yatakuwa yanawahusisha kwa ajili ya mbuzi na kondoo na kadhalika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani halistahili kupigiwa kura, hili sio jambo kubwa sana, tuachie Mahakama nayo muhimili ule mwingine uweze kufanya kazi yake kiwango cha mwisho kilichowekwa sio lazima kitumike hicho hicho kwa sababu sheria imeweka kiwango cha juu, lakini ni kuanzia chini kwenda juu.

Jambo moja tu Mheshimiwa Waziri nilikuwa nataka kuwa na uhakika tu wa sarufi. Hivi mtoto wa mbuzi au ndama wa mbuzi? Au kwenye mbuzi hakuna ndama? Nataka kuelewa tu maana yake. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishamaliza huu Muswada, ukishapitishwa nitaangalia kwenye Kamusi ili nijue vizuri kwa sababu na mimi sijui, lakini nafikiri ni mtoto wa mbuzi na wa ng'ombe naye ni ndama. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Basi wakati wa Kamati tutayatumia yote mawili halafu baadaye tutajua.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Mzindakaya umewasilisha mapendekezo ya mabadiliko katika ibara ya 21, nakupa muda usiozidi dakika tano ili uweze kuyaelezea mapendekezo yako.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuleta haya mabadiliko. Kwanza ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba kabla sijaandaa mabadiliko haya nilishamweleza shabaha yangu na naona kama tulikuwa tunakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze tu kwa kifupi ni kuwa sisi tuna ugonjwa wa kutokuhangaika na kuongeza thamani ya mazao yetu. Ukienda Namibia, Waziri Mkuu ni shahidi hawaruhusu kuuza ng’ombe nje, Botswana, Swaziland, *South Africa* jirani zetu wa Kenya hawaruhusu kuuza ng’ombe *live* nje. Ndiyo maana nimeleta mabadiliko hapa ili na sisi tufanane na wenzetu. Hii itahimiza Serikali kujenga viwanda vya kutosha ili tuongeze thamani ya mazao yetu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya hayo napendekeza kwamba kile kifungu cha *clause* 21 isomeke kama ifuatavyo; kwa kusema:-

(a) B*y deleting sub clause (1), and substituting it with the following new sub clause:*

*" (1) Livestock imported into Mainland Tanzania shall be registered and its particulars be submitted to Director".*

(b) *By deleting the words "or export" appearing in the first line of sub-clause (2) between the words "import" and "of".*

(c) Na hivyo hivyo, ule upande wa pembeni, b*y deleting the words "and export" appearing in the marginal note of that clause*. Kwa hiyo, kwa msingi huo na kule mwanzo kabisa tunapozungumza *paragraph four* maneno yatakayosomeka yatakuwa *traceability of imports of livestock and not export.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Kwenye mabadiliko muwe mnatoa hoja sio kuwasilisha.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni hoja ambayo imeletwa mbele yetu, tunayo ruhusa kama Wabunge kutoa maoni yetu?

**MWENYEKITI:** Mna ruhusa, mmepewa muda ila mkumbuke kwamba huwezi kutumia zaidi ya dakika tatu. Kwa hiyo, ukiwa na dibaji ndefu sana, kengele italia halafu basi, hoja itakuwa imepotea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa angalizo lako. Ni juzi tu Waziri Mkuu alikuwa anajibu swali kuhusu watu wanaolima na kwamba Serikali inawakataza kupeleka mazao yao nje. Wakati ambapo bado hatuna viwanda vya kutosha nchini kuna kiwanda cha Mheshimiwa Mzindakaya, sawa; lakini baada ya hapo hakuna kiwanda kingine. Tuna machinjio ya kisasa ya ng'ombe ndiyo inajengwa sasa Ruvu, kuna machinjio ndogo hapa Dodoma, hakuna nyingine. Itakuwa ni hatari kubwa kama sheria hii itakaza *export* ya watu ambao wanataka wana mifugo iliyo mingi wanapeleka Kenya, wanapeleka sehemu nyingine tufike pale ambapo tuna uwezo wa kuweza kutumia wanyama wetu wote ndiyo tuweke angalizo kama hilo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cheyo amenisadia sana. Unajua tunapotunga sheria ni lazima tuangalie

mazingira ya hali halisi. Serikali ni hvi karibu baada ya kupitisha sera ya mifugo tuliamua kufungua minada kwenye mipaka, na ukienda Musoma na wenzetu kutoka Arusha kwa sababu ya soko zuri lilivyokuwa kule Kenya wameweza kuuza mifugo yao kupeleka Kenya na nimeeleza hapa katika maelezo yangu kwamba asilimia 80 ya ngozi zetu tumeziuza kama *raw material*. Tungekuwa tumebana hizo sheria, maana yake hata zile shilingi bilioni 36 tusingeweza kuzipata, lakini mbali ya hivyo hii sheria ndiyo wala bado haijapita na tumeiweka kwenye *grace period* ya miaka mitatu, watu wa kuja kujenga viwanda bado, na kwa sasa hivi watu walikuwa wanaogopa kuja kujenga viwanda kwa sababu walikuwa hawawezi wakauza nyama zao nje hata kwenye makampuni ya madini yanaagiza nyama kutoka nje.

Lakini mbali ya hivyo viwanda vilivyopo, baada ya Tanganyika *Parkers* kutoweka, ni vichache sana na *production* yao ni ndogo sana. Kwa hiyo, mimi ningefikiri katika ile *spirit* ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitoa ya kuwaruhusu wananchi wa Rukwa kuuza mazao mpaka nchi za jirani Malawi na kadhalika tuendelee na *spirit* hii.

Lakini kwa baadaye kama hali halisi itaturuhusu kuwa na viwanda vingi vya nyama, viwanda vingi ya vyakula, tunaweza tukatengeneza hata katika *regulations* ili kusudi tuka-*accommodate* suala la Mheshimiwa Mzindakaya. Ningemwomba Mheshimiwa Mzindakaya akubaliane na yale mapendekezo yaliyoko kwenye Muswada wa mwanzo kwamba watu kwa wakati huu waendelee pia kuuza bidhaa zao kama wanavyoweza kufanya hizo *process* na tumekuwa tukifanya hivyo hivyo hata minofu ya samaki *otherwise* tungekuwa tunazi-*park* kwanza minofu ya samaki tunai-*process* ndipo inakwenda. Lakini tunapeleka hata samaki wanakwenda kutengeneza wao kule, ili angalau tukipate hicho kidogo badala ya kukikosa kabisa.

**MWENYEKITI:** Kama ninakumbuka vizuri nadhani kuna masoko ya nje yanahitaji wanyama wa kafara, sasa wa kafara huwezi ukamchinjia kabisa anataka achinje mwenyewe, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya labda tuachie kwa sasa kwani ni suala la muda tu ikifika wakati tunaona tumekaa vizuri basi!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri sina tatizo la kuelewa labda ni namna ya kukubaliana na Waziri hata mawazo aliyotoa Mheshimiwa Cheyo isipokuwa nilichotaka kusema kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri mimi nadhani ingekuwa vizuri katika kipindi hiki cha miaka mitatu waweze kutazama jiografia ya nchi ilivyo na hali halisi ilivyo ili ikiwezekana itakapobidi zitengenezwe *regulations* kwa sababu vilevile tabia hii ya kupenda sana kuuza *raw materials* zetu ni ugonjwa wa nchi zaidi.

Mimi naomba nalo hilo tujifunze kama shule kwa sababu gani? Ukiona juhudi inayofanyika ya kuongeza ujenzi wa viwanda ni ndogo sana na sababu nyingine ambayo nataka nieleze na ushahidi ninao ni kwamba Tanzania hatujaanza kujenga *incentives* kwa *processors*, ni vibaya kujisemea lakini nchi hii wanakataa kutoa *subsidies* huwezi kuuza mazao ya vyakula kama hutoi *subsidies* katika nchi, ndiyo maana watu hawaji kujenga viwanda wala havitajengwa kwa Sheria hii ya *traceability* na *registration*, itajengwa kama tukiweka *incentives* za *export* na mojawapo ni *subsidies* katika mazao ya chakula. Naomba ujumbe huu uifikie Serikali ni ndogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 25

*(Ibara mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010**
***(The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo yaani *The Livestock Identification, Registration and Traceability Act of 2010* kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo yaani *The Livestock Identification, Registration and Traceability Act of 2010* kama ulivyorekebishwa na Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki!

*(Hoja ilitolewa iIamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu hapa ni ya kukubali kuupitisha Muswada wa Sheria inayohusu Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa mwaka 2010 yaani *The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010.* Hoja hiyo ilitolewa na imeungwa mkono lakini ni wafugaji wawili tu ndiyo wamepinga na kwa hiyo, Muswada huu umeshapata kibali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu Kanuni ya 91 Muswada ukishasomwa mara ya tatu maana yake Bunge limeupitisha. Ninafurahi kutangaza rasmi kwamba sasa Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili, na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 umepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Waziri tunakutakia heri, ni changamoto kubwa lakini mkitunga kanuni vizuri na pia kusimamia jambo hili vizuri tunaweza kuondoka hapa kwenye ujima tukaenda kwenye utaratibu wa kisasa zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Namuomba Katibu aweze kusoma hatua inayofuata.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Malisho ya Vyakula vya Mifugo wa mwaka 2010 *(The Grazing Land and Animal Feed Resources Bill, 2010)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 3

*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilziotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 16

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16 inataka pawepo na sehemu ya kuchunga au kulisha mifugo. Kwanza, ninachotaka kuelewa ni utekelezaji wake kwanza kwa upande wa Serikali, mimi nimeshtushwa sana na alipokuwa anachangia Mheshimiwa Waziri kusema kwamba ardhi inayofaa kwa malisho ni takribani hekta milioni 50, iliyotengwa sasa ni milioni 1.3. Sasa ninachotaka kujua ni utaratibu gani utakaofuatwa yeye yuko Wizara hii, mwingine yuko Wizara hii kuhakikisha kwamba angalau kuna nusu ya ardhi ile inayohitajika na zaidi ukiangalia ni kwamba sasa hivi ana kiwanda pale Ruvu ambacho kitahitaji ng'ombe milioni tatu kila mwaka kwa hiyo, kwa miaka mitatu atakuwa amemaliza karibu ng'ombe wote kama hatutaweza kutenga sehemu ambayo tunaweza tukachunga na kuweza kuzalisha zaidi.

Lakini la pili, nataka kujua kwamba je, mfugaji mwenye shamba lake anahusika vipi na Ibara hii? Mwenye kihamba chake na ng'ombe wawili au kumi na mwenyewe itakuwa ni lazima afuate Sheria hii na isajiliwe kama *grazing area?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa John Cheyo kwamba hiki kifungu namba 16 kimewekwa kwa kuzingatia pia Sheria ambazo zilipitishwa na Bunge na kiliwekwa kwa kuzingatia Sheria ambayo tayari ilipitishwa na Bunge hili na hii ni Sheria namba 6 ya mwaka 2007 ambayo inazungumzia juu ya matumizi bora ya ardhi ya mwaka 2007.

Kuhusu hilo suala la kwamba maeneo ya malisho mengi yalikuwa hayajapimwa, huo ndiyo ukweli kwamba katika muda mrefu na kwa sababu hatukuwa na Sheria ambazo hata zinaweza zikaibana kwa upande mwingine Serikali kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ndiyo maana tumekuwa *flexible* kwa upande wa Serikali na ndiyo maana Sheria inapotungwa Sheria ni msumeno inauma kote kote hata kwa upande wa Serikali tunaumwa.

Kwa hiyo, kwa upande wa Sheria hii kwa sababu hadi sasa hivi tuna vijiji 14,000 katika nchi nzima lakini ambavyo vimeshapimwa ni vijiji 10,000. Kwa hiyo, kwa kupitia Sheria hii nina uhakika Serikali sasa itajipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba vile vijiji 4000 vilivyobaki vinapimwa, yale maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya malisho nayo yanapimwa na kutengwa kwa sababu Sheria hii ni Sheria ya nchi nzima.

Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo kwamba ndiyo maana ya Sheria hii, itawasaidia na hiki kifungu ndicho

kitawasaidia wafugaji kupata maeneo kwa ajili ya kulisha mifugo yao. Kwa hiyo, ninamshauri tu akubali kwa sababu ni kwa manufaa kwa wafugaji hata wale wa Bariadi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na maelezo yake, nashangaa tu utekelezaji wake ni wapi Serikali hii ndiyo yenyewe imeleta Muswada huu, hiyo hekta milioni 20 kwa mfano badala ya hekta 50 zipo na zinaweza kupatikana? Bunge hili liambiwe kwa sababu ukweli ni kwamba watu wengi wanaofuga wamebanana, wengine wanafukuzwa kila siku, watu wa Bariadi wanafukuzwa kule Mara, hatujui twende nao wapi. Kwa hiyo, kama kuna maeneo kuna hekta milioni 20 si yatengwe sasa tuwaambie wananchi kwamba nendeni huko?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina ukubwa wa kilometa za mraba 945,000, ukitafuta *square root* ya ile halafu u-*calculate* kwa kupata ni hekta ngapi zinatosha kwa ajili ya mifugo ndiyo maana nimeeleza katika *speech* yangu kwamba ukipiga *calculation* ya kawaida kuna maeneo karibu hekta milioni 50 ambayo yanaweza kufaa kwa ufugaji.

Katika maeneo ambayo yametengwa rasmi kwa ajili ya wafugaji ni hekta milioni 1.3 hiyo haina maana kwamba maeneo mengine ambayo wafugaji sasa hivi wanaishi hayafai kwa ajili ya ufugaji na izingatiwe na kueleweka kwamba kuna maeneo ambayo mtu anakuwa mfugaji lakini pia anakuwa mkulima. Kwa hiyo, maeneo haya ni katika kuelezea hali halisi kwamba tuna tatizo hili ni lazima tulikabili kwa Serikali nayo kwa upande mwingine kwa kupitisha Sheria namba 6 ya mwaka 2007 tuanze kutenga maeneo ya wafugaji.

Katika ile Sheria namba 6 ya mwaka 2007 inasisitiza wazi kwamba maeneo katika kile kijiji kitakuta kinatenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, wakulima, kujenga nyumba, vyanzo vya maji, misitu na kadhalika. Lakini kwa kusisitiza na hii Sheria sasa inaweka mambo mengine pia kwamba hata Serikali inaweza ikaamua kwamba eneo hili tunalikata linakuwa ni kwa ajili ya wafugaji kama ambavyo linaweza likakatwa eneo likawa kwa ajili ya wawekezaji labda kwa misitu au kwa ajili ya kilimo au hata kwa wanyamapori. Serikali itakuwa inaamua kufanya hivyo.

Lakini nataka kumueleza na kumhakikishia Mheshimiwa John Cheyo kwamba Serikali inafanya kazi kwa pamoja, Wizara ya Ardhi Mheshimiwa yuko hapa, Wizara ya Mifugo vilevile wote tunafanya kazi kama kitu kimoja chini ya *coordination* ya bosi wetu Mheshimiwa Mizengo Pinda ambaye ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba haya yatazingatiwa lakini kitu kikubwa ni kwamba Sheria iwepo ili tujue mahali pa kuanzia.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi Sheria hii inajielekeza kwenye sisi tujipange vizuri, tukijipanga vizuri ardhi iliyokuwa inaonekana kama vile haipo kutokana na fujo tu, itaonekana kwa sababu itakuwa imetengwa. Mimi ndiyo nimeelewa hivyo.

Mheshimiwa Dr. Slaa!

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inayoweza kuleta mgogoro mimi nafikiri ni vizuri kuiepuka. Mheshimiwa Waziri anazungumzia jumla ya ardhi ambayo kinadharia ipo lakini kihali halisi sidhani kama leo kuna mtu anaweza kutuambia kwenye vijiji tulivyonavyo iko mahali pale. Waziri wa Ardhi ni shahidi kwamba migogoro mingi katika nchi hii inatoka na ardhi, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba kwa kila eneo mgogoro ambao unaleta utata ni wa ardhi. Sasa tukizingumzia ardhi ambayo iko kwenye misitu, baharini na kwenye maeneo makavu wala haiko kwenye kijiji mimi nafikiri kuna tatizo, lakini tatizo la msingi katika kifungu hiki ni pale ambapo Sheria hii sasa inataka vijiji kutenga eneo la ardhi.

Mimi nafikiri Waziri atuhakikishie kwa kuwa ardhi ya jumla ambayo bado inaweza kutengwa iko chini ya Kamishna, Serikali ituhakikishie kwamba jukumu hilo lihamishwe kutoka kwa vijiji lipelekwe kwa Kamishna ili kusiwe na mgogoro kule chini, tutakapofika mgogoro uko chini watu wetu watauana, watakatana mapanga na mifano iko hai, jana kwenye vyombo vya habari wote tuliona kule Hanang, Karatu kule tumeona kila wakati, Mkoa mzima wa Manyara tuna mgogoro.

Kwa hiyo, mimi nafikiri suala hili Waziri atuhakikishie je, kwa mujibu wa Sheria namba 4 na 5 yeye pamoja na Kamishna wa Ardhi wako tayari kuchukua jukumu la kutenga ardhi hii badala ya kuiachia kwa Serikali ya Vijiji?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kutoa ufafanuzi kwamba hii migogoro ya ardhi ambayo tunaishuhudia maeneo mengi wakulima na wafugaji wanagombania ardhi ni kwa sababu hatujatekeleza ile Sheria namba 7 ya matumizi bora ya ardhi, hatujawekeza ardhi yetu tukaiwekea matumizi bora ya ardhi.

Kwa hiyo, moja ya majukumu ya Wizara yangu kuanzia mwaka ujao wa fedha ni kuingiza katika suala la kila kijiji kipangiwe matumizi ya ardhi, katika kila kijiji ijulikane kwamba hii ardhi imetengwa kwa kilimo, hii kwa ajili ya ufugaji, makazi, huduma mbalimbali, makaburi na kadhalika na tukifanya hivyo kwa nchi nzima yaani ardhi yetu tukiipanga namna hiyo matatizo haya yatapungua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha Serikali imekubali kutenga fedha kwa ajili ya kufanya kazi hii, tutaifanya kwa awamu baada ya miaka kadhaa nchi yetu itakuwa imeshapangiwa mipango mizuri ya ardhi na hapo matatizo yatakuwa yamepungua. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kwa sababu tunataka kuvutana tu. Mimi nafikiri nia yetu wote ni kutaka sheria nzuri inayotekelezeka. Katika Bunge hili hili wakati tunapitisha Sheria Na. 4 na Na. 5 mimi Serikali ilinihakikishia kwamba Waziri atahamia Wilaya ya Karatu. Kwa sababu kutokana na sheria ya awali nadhani ya *Village and Villagisation Act,* tukapata migogoro mikubwa sana. Karatu kwa mfano sasa hivi hatuna kipengele chochote cha ardhi kwenye kijiji chochote ambacho hakikugawiwa mtu. Sasa leo tukitunga sheria kwamba tutatumia

*Land Use Planning* na maneno mengine mazuri, lakini ardhi hiyo iko wapi na utamnyang'anya nani uende kugawa? Mimi ninapita kwenye maeneo mengi, kupitia Kamati yetu nakutana na migogoro hii kila kona tunapopita.

Mimi nafikiri tukubali pale ambapo kuna tatizo hebu nadharia tuiweke mahali, tutumie Serikali itusaidie kwanza ku-*identify* tufanye *mapping* ya nchi yetu tu-*identify* kwamba ardhi hii na mimi siku moja nimetoka Dar es Salaam kuja huku. Kila kipande cha ardhi unayokuta kutoka Dar es Salaam kuja huku kama sio msitu mkubwa tayari kuna mwananchi anakaa. Sasa leo ukisema tu kwamba ardhi ipo nadharia, mimi naogopa Bunge hili litatunga sheria kwa kitu ambacho ni nadharia, lakini na vijiji havitaweza kutekeleza na wafugaji kuanzia kesho wataanza kudai kwenye vijiji kwamba sisi tunataka ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kule nina tatizo lingine la ziada, Wahadzabe tayari wanadai. Kwa taarifa yako wamekwenda mpaka Austria sijui kwenye chombo gani na sijui ni nani aliwapeleka kudai Umoja wa Mataifa kwamba tunanyimwa. Wao wanasema tunataka ardhi kwa wakati wa kiangazi, tunataka ardhi kwa wakati wa masika, na sababu zinaelekeweka kwa sababu wenzetu wakati wa masika wanakaa kwenye mapango *(caves*), wakati wa kiangazi wanataka mahali ambapo kuna wanyama na mahali ambapo kuna miti yenye matunda kwa chakula chao kwa *background* yao. Sasa hapo tumeshindwa. Sisi kama Wilaya tumeshindwa kugawa na ni zaidi ya miaka mitano tunashughulikia. Waziri aliyenihakikishia atahamia Karatu kuja ku-*solve* hakuja Karatu. Sasa mimi naaogopa tutatunga sheria lakini tutaacha baadaye migogoro mikubwa. Tusipitishe sheria kwa sababu tu tunataka kupitisha, tuangalie sheria ina-*solve* nini na Serikali imejiandaa vipi katika tatizo hili ambalo liko mbele yetu kwa uwazi kabisa.

**MWENYEKITI:** Hebu nijaribu kuelewa, maana yake ikiwa msingi haueleweki, sasa tunaweza kubishana na sio tunazungumza ila tuna-*shout past each other*, kuna kitu kinaitwa namna hiyo. Mimi nadhani hapa ukichukua kifungu hiki ambacho tunakijadili hivi sasa cha 16, Serikali za Vijiji zinapewa uwezo wa kujipanga ndani ya eneo lile lile walilonalo kwa kuzingatia haki za wafugaji na wakulima. Hilo haliwezi kufanyika na Kamishna kutoka Dar es Salaam. *Infact* kwa maana tu ya demokrasia, bora wasikilizane wenyewe pale kwenye Kijiji kuliko utegemee mtu atoe amri kutoka mbali. Niseme tu kwamba kuna hatari ya kulinganisha tatizo mahsusi katika Wilaya fulani na kulifanya ndio la Tanzania nzima.

Kwa mfano, sisi Mikoa ya Magharibi, hilo linawezekana, kwa sababu hata sasa tuna wafugaji na wakulima, taabu yetu ni kwamba kijiji kinapoamua kwamba wafugaji mpaka wao ni huu, mamlaka hayo hawana na kweli tunafurahia kwamba hiki sasa kipo, tutawawezesha sasa Serikali ya Kijiji kuwapanga watu katika Kijiji. Sasa yale ya Karatu labda Waziri wa Ardhi atayashughulikia kwa hatua maalum, lakini isituzuie kuwezesha robo tatu ya nchi wajipange vizuri ndani ya eneo walilonalo kuliko tuachie sasa, maana yake ukiondoa hili unaondoa uwezo wa Serikali ya Kijiji kuwapanga wakulima, wafugaji, warina asali na watu mbalimbali katika eneo hilo. Lakini bado tunaelewa kwamba Kamishna wa Ardhi katika yale maeneo ambayo ni *public land* ambayo yatahitaji kugawiwa, atafanya hiyo kazi yake. Lakini huwezi kusema kama hilo

halifanyiki, basi vijiji pia tusijipange au Serikali za Vijiji visiwe na nguvu ya kurekebisha hii hali. Hiyo ndiyo hoja yenyewe.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli umetusaidia sana, umefafanua vizuri. Hapa kuna sheria tatu. Kuna Sheria Na. 4 ya Ardhi ya Mwaka 1999, Sheria ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya Mwaka 2007. Katika Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini, vijiji vinapewa mamlaka ya kupanga matumizi yao ya ardhi. Wanaweza hata wakatoa hati ambayo unaweza ukaenda kukopa hata Benki kupitia vikao vya *Village Assemblies* na kadhalika. Hayo madaraka wanayo.

Sasa kipengele hiki kinazungumza tuna *consider* yale mamlaka yaliyoko kwenye vijiji na tunapozungumza kwamba ardhi iko wapi, kwani sasa hivi wafugaji wako wapi? Hawakai kwenye ardhi? Si wanakaa kwenye ardhi? Sasa yale maeneo yatakuwa *demarcated* vizuri. Tunapozungumza tuna ng'ombe 19, kwani zinakaa ngapi? Zinakaa huko huko kwenye ardhi! Sasa maeneo hayo tuyafuate kwa kutumia sheria, tuyapange vizuri ili tumalize migogoro kati ya wakulima na wafugaji ili watu wote waweze kunufaika. Katika yale maeneo ambayo yamepimwa milioni 1.3 yamepimwa katika kipindi cha mwaka mmoja tu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mimi ningependa niwape pongezi sana Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa ambayo imeanza kuifanya ambapo katika kipindi cha mwaka mmoja imeshapima maeneo kwa ajili ya wafugaji hekta milioni 1.32. Kwa hiyo, ni mwanzo mzuri. Sasa kwa kupitisha sheria hii, wafugaji hawatadhulumika. Tutaanza kuyapanga maeneo vizuri kwa kutumia ile Sheria Na. 6 ya mwaka 2007. Lakini kwa kutumia hata ile Sheria Na. 4 ya Mwaka 1999 inayompa Kamishna kutenga maeneo mengine makubwa kwa ajili ya wafugaji na Serikali kwa ujumla katika kujipanga kuhakikisha kwamba hizi kero zinaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimweleweshe Mheshimiwa Wilbrod Slaa kutunga sheria, sio kwamba migogoro itakwisha. Hata Mungu alipoleta amri 10 bado watu tunazini, tunaiba na kadhalika. Lakini amri zipo na sheria zipo. Lakini tunataka tuwe na sheria ili kusudi watu waweze kufuata. Unaambiwa usizini bado mtu anakwenda kuzini; usitamani mwanamke ambaye sio mke wako, bado unamtamani. Sheria zipo na zipo kwa miaka mingi karne na karne. Kwa hiyo, kutungwa kwa sheria hii sio kwamba migogoro itakwisha. Watu wataendelea kuvunja sheria, lakini ni vyema basi tukawa na sheria ili watu tuwapeleke kwenye *direction* inayotakiwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani hii imeeleweka. Ndugu Blandes niliona umesimama, natoa nafasi kwa kila aliyekuwa na hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuuliza ufafanuzi tu kwamba kwa vile vijiji ambavyo pengine havina ardhi. Kwa sababu hapa sheria inazungumzia ardhi za vijiji lakini kuna vijiji ambavyo havina ardhi mpaka sasa hivi ardhi yote ni ya wananchi.

**MWENYEKITI**: Kijiji hakina ardhi, ama ardhi ya kijiji haijapimwa?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wanipe nafasi. Nilitaka kusema hivi, ardhi ya Kijiji hicho tayari ina wenyewe, tayari inamilikiwa na wananchi. Sasa katika Vijiji kama hivyo ambapo ardhi yote tayari imeshachukuliwa, ina wenyewe, sasa sheria hii ina-*consider* namna gani hayo maeneo ya malisho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sijui kama unaelewa vizuri. Sasa ardhi imechukuliwa yote, kwa hiyo, hawa ni kama wapangaji, au sijui *situations* za namna hiyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Blandes hasa anazungumzia katika masuala ya Kagera ambapo pamekuwepo na migogoro mingi ya ardhi kutokana na baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa ni ya wafugaji yamevamiwa na wakulima au yalikuwa ya wakulima yamevamiwa na wafugaji. Sasa kulingana na hilo suala ndipo sasa sheria ambayo inaelezea namna ya kufuga kulingana na uwezo wa ardhi inakuja na ndipo *notice* ya miaka mitatu inatolewa na *Inspector* na baada ya hiyo miaka mitatu anapewa tena *notice* nyingine ya miaka mitatu ili kusudi akatafute maeneo ambayo yanaweza yakahimili ule ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote ardhi yetu haikui, iko vile vile. Ni lazima tupange ni mahali gani patafaa kwa ufugaji, ni mahali gani patafaa kwa kilimo. Mimi nina uhakika tukipitisha sheria hii ndipo itakuwa ni rahisi sasa kuangalia ni mahali gani panakuwa na *overgrazing* kwamba mifugo hii sasa ihame iende mahali fulani na kuzingatia sheria ya Tanzania kwamba Mtanzania anaweza akaishi mahali popote. Basi hii sheria sasa anaweza akaruhusiwa kuhamia kwenye kijiji kingine au akapunguza mifugo yake wakati Serikali imeshajiwekea mazingira mazuri na ndiyo maana utekelezaji wa sheria hii *straight* tumejipa kama Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu ili ardhi kwa ajili ya wafugaji wakulima na kadhalika iweze kuwa imepangwa vizuri, migogoro hii midogo midogo ambayo imeanza kujitokeza tokeza tuanze kuishughulikia na kadhalika.

Kwa hiyo, ningependa nimweleze Mheshimiwa Blandes kutoka Kagera na Kagera ni *special case*, kwa sababu hata katika zile ranchi 51 ambazo zilibinafsishwa kwa wafugaji, sasa hivi zinatumika kukodisha watu kutoka Uganda na Rwanda. Kwa hiyo, mifugo kutoka nje inakuja kwa Mkoa wa Kagera kwa kulipa Sh. 50,000/= kwa kila mfugo wanaochunga. Kwa hiyo, wenyeji wa pale wamekosa maeneo na hili nalo Serikali inalifanyia kazi. Tumeshindwa kufanya hivyo kwa sababu hatuna sheria. Kwa hiyo, kwa sheria hii *Traceability* tutaweza ku-*trace* kujua huyu ni ng’ombe wa Rwanda au ni ng’ombe wa Uganda na kama ni wa Uganda kwa kuzingatia sheria hii tuweze kuchukua hatua. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Blandes atusaidie hii sheria ipite na tuweze kutatua matatizo yaliyoko katika Mkoa wa Kagera na eneo lake la Karagwe.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwamba pande zote mbili mimi ninahusika na kwa

hiyo, nina *interest* kama Waziri kwa upande wa Serikali na kama Mbunge ninayetoka Wilaya ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tatizo lipo na mimi naomba nitoe mifano halisi. *Masai Staple* kwa mfano ni eneo la wafugaji kama ilivyokuwa inajulikana zamani *Masai Staple*, hata ukiangalia historia, Wilaya ya Hanang kwa mfano ni Wilaya ya wafugaji, lakini utakuta leo kuna wakulima. Tatizo ambalo lipo ni kwamba kwa mfano leo unakwenda Wilaya ya Hanang kuna ng'ombe 300,000 na kuna wakulima labda 150,000. Sasa *practical problem* ni kwamba ukikuta Wilaya ya Hanang haitoshelezi wakulima wala haitoshelezi mifugo, kwa hiyo, kuna sababu ya kusimamia hii sheria kuona kwamba mifugo ile iliyopo wanapata eneo na wakulima waliopo wanapata eneo kwa sababu huwezi ukasema tu wafugaji wakatafute, bila shaka tutasema ni wakulima kama ni wengi kupita kiasi kwenye ile Wilaya nayo wakatafute nafasi.

Kwa hiyo, jambo lililo muhimu ni usimamizi wa sheria jambo ambalo kwa kweli kwa muda mrefu mimi nafikiri halikujikita vizuri kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, nasema hii sheria itasaidia sana wakulima na wafugaji pale ambapo usimamizi wa Serikali yetu utakuwa mzuri na ninaamini usimamizi huo utakuwepo. Bila kuwepo sheria kutakuwa na migogoro ambayo itakuwa inaendelea hasa sasa ambapo kuna sheria hii, kwa sababu kuna watu ambao watadai maeneo ambayo yanajulikana kihistoria, lakini kwa kutumia sheria hii sasa wafugaji na wakulima wa Tanzania watakuwa na hali nzuri zaidi hasa pale ambapo sheria hii itasimamiwa.

**MWENYEKITI:** Nadhani tumekaa pazuri.

*(Ibara iIliyotajwa Hapo Juu iIlipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru mwanzoni niliwasilisha mapendekezo tarehe 15 Aprili, kuhusiana na ibara hii ya 17 na leo baada ya majadiliano kwenye Kamati na mabadiliko ambayo yamefanywa na Serikali, nimebadilisha kiasi na pendekezo ninalolitoa ni kwamba katika ibara ya 17 kuna kifungu cha kwanza na cha pili lakini nilikuwa napendekeza kifungu cha tatu ambacho kitasoma: *"The Village Council shall prohibit, restrict, limit or control entry into grazing land for the purposes of cultivation, mining establishment of wildlife protected arears or any other use other than livestock keeping."*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwa lengo kuu la sheria hii ni kuboresha sekta ya mifugo, lakini ili iweze kuboresha sekta ya mifugo, ni lazima uendeleze malisho kwa maana ya *grazing lands*, lakini pia na *grazing resources*. Lakini tukitaka historia na hali halisi ilivyo sasa tatizo kubwa linalowakabili wafugaji ni kwamba maeneo mengi ya malisho yamechukuliwa na kutumiwa kwa matumizi mengine. Tunazo hifadhi za wanyama nyingi, maeneo mengi yamekwenda kwenye kilimo na mengine kwenye *infrastructural development.* Kwa hiyo, hoja hapa ninayoipendekeza ni baada ya kuwa

eneo limebainika kwamba ni la malisho, basi sheria hii badala ya kubaki kimya ama bubu itamke rasmi kwamba haitaruhusiwa na hili litakuwa ni jukumu la *Village Council* kuhakaikisha kwamba baada ya eneo kubainishwa kwamba ni malisho isiruhusiwe tena uvamizi wa aina nyingine uwe ni wa aina ya kilimo ama matumizi mengine ya wanyamapori kusudi kwa njia hii tuweze kuendeleza haya malisho na mwishoni tunufaike na sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hiyo na naomba niwasilishe hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Sheria Na. 6 ya Mwaka 2007 ambayo nimesema tutaanza kutekeleza mwaka ujao kwa kasi zaidi, inasema kijiji chenyewe ndicho kinachohusika katika kupanga matumizi ya ardhi yake. Kwanza kijiji chenyewe kitapata hati ya kumiliki eneo la kijiji chake; pili, kijiji chenyewe kupitia *Village Council*, Mkutano Mkuu wa Kijiji ndio watakaoshiriki kusema eneo hili hapa ni la malisho, hili hapa la kilimo, hili hapa la makazi. Wataalam wale wanawasaidia tu kuweka mipaka wao wenyewe ndio wanaojipangia hivyo. Wakishasema hili eneo la malisho, *(bye-law)* sheria ndogo inawekwa ili eneo hili la malisho liwe kweli la malisho. Kama hili wamesema la kilimo sheria ndogo inatungwa kwamba hili ni la kilimo ili wasiingiliane. Sasa kama hayo yakifanyika, hayo mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge yanakuwa sio ya lazima.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Tunachoongelea ni hali halisi kwamba sheria ndogo mara nyingi inashindikana kutekelezwa hasa shauri linapokuwa limetoka katika Baraza la Kata likaenda kwenye Mahakama. Maana tupende tusipende bado kumekuwepo na *tendency* ya sheria hizo ndogo ndogo kuonekana kwamba ni sheria za daraja la pili. Kwa hiyo, mimi ninalopendekeza hapa sana, kwa sababu ya hali halisi iliyopo kule katika maeneo yetu na Wilaya yangu ni mfano mmoja, nilikuwa napendekeza Serikali ikubali kuwepo pia na hili katika sheria hii, maana kwa njia hii itakuwa sheria inayolinda maeneo haya badala ya kutegemea sheria zile ndogo ndogo ambazo kwa kweli vijiji vingine vinashindwa kupitishwa kwa sababu ama ya kukosa *legal aid* na kushindwa kupata wataalam watakaoelekeza kutunga hizo sheria, lakini pia kuzifanya zifanye kazi inakuwa ni vigumu zaidi ku-*reinforce*, heri ziwepo katika sheria hii. Kwa hiyo, bado ningeliomba kwamba pamoja na sheria hizo nyingine ambazo zipo, Serikali ikubali hili nalo liingie kama kuweka msisitizo na mkazo katika sheria hii ili malisho yaweze kulindwa na hatimaye sekta ya mifugo nayo iweza kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuunga mkono haya ambayo Mheshimiwa wa Kiteto ameeleza. Ni kweli kwamba wakati tukiingia katika Vijiji hilo jambo la kutenga ardhi kwa ajili ya wakulima na kwa ajili ya wafugaji lilikuwepo. Kwa mfano, katika Wilaya ya Dodoma na sehemu nyingi, suala hili lilifanywa kwamba kulikuwa na sehemu za wafugaji ambazo ziliachiwa wafugaji. Lakini baadaye watu kwa jeuri wakaingia na wakapeleka majembe yao na mimi kila siku nataka niseme tatizo la wafugaji kwamba kila siku majembe yako nyuma yao. Kila

wanapokwenda majembe yako nyuma. Kwa hiyo, inawafanya wasonge mbele wakati ardhi yao inachakuliwa na majembe. Sasa hapa ndiyo Kijiji kitakuwa na sheria, lakini tunataka tuiweke hii katika sheria hii iwe kama sheria mama ili wanavijiji wakiweka *by laws* zao za ku-*protect* mahali pa wafugaji, basi angalau inatokana na sheria ambayo tumepitisha leo. Tunasema leo tunaingia katika Sheria ya kutuleta kwenye ufugaji bora. Sasa basi tuwe na Sheria mama ambako huko Bijijini ndiyo wataitengeneza kutokana na hii sheria mama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninasihi sana na ningemsihi Mheshimiwa Magufuli angalau kwa hili kwa sababu matatizo mengi tunayoyapata ni haya ambayo sheria ndogo ndogo ambazo haziwezi kuhimili mpaka ziwe na uzito wa sheria mama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tu tuwe na tabia ya kukumbuka. Ukurasa wa 35 wa Muswada huu unasema madhumuni ya Muswada huu ni kutunga Sheria ambayo itaweka mfumo wa kisheria wa kusimamia na kudhibiti maeneo ya malisho ya mifugo. “Kusimamia na kudhibiti maeneo ya malisho ya mifugo.” Haya ndiyo madhumuni ya Muswada huu.

Mheshimiwa Nangoro alipoleta mabadiliko haya, kimsingi yanalenga kusimamia na kudhibiti maeneo hayo yasiendelee kuvamiwa au kuweka utaratibu uliobora. Sasa eneo likishatengwa tayari kuwa eneo la mifugo kwa ajili ya malisho ya mifugo katika ardhi ambayo inakuwa *owned communally*, unategemea utaratibu uwekwe wa kulinda ardhi hii?

Muswada huu ukikataa kuingiza kifungu hiki, basi tuelezwe Muswada huu haukuwalenga wafugaji hao kwa kuwalindia ardhi yao ila imelenga kutengeneza ma-*tags* na kuwatengenezea mradi mwingine wa pembeni wa kuridhisha soko la huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi hii tunayozungumza kwamba Serikali ya Kijiji ipate mamlaka ya kusimamia maeneo haya yaliyotengwa ni kunusuru maeneo haya ya mifugo ambayo yamekuwa yakichukuliwa na uhifadhi wa wanyamapori kuchukuliwa na maeneo ya mashamba makubwa kama kule Basuto na Naberera katika Wilaya ya Simanjiro na kuchukua maeneo mengine kwa ajili ya wanyama kama ilivyokuwa Loliondo ambako leo wananchi wamezushiwa na kesi nyingine wanapo-*exercise rights* zao, kutetea na kueleza migogoro iliyopo katika eneo lililopo na wengine wamefunguliwa kesi juzi, eti kwa sababu tu wamejumuika pamoja kueleza matatizo yao. Ni kulinda ardhi hii kama ilivyo pale Naisinyai ambayo migodi mikubwa pale karibu na Mererani imechukua eneo lote la malisho la kijiji cha Naisinyai na Kijiji cha Langasiti na Mishiye na kuwafanya wananchi wale waondoke katika eneo lile na mifugo ikakosa malisho. Ni kuweka utaratibu wa kuweza kupata *concern* ambayo Sheria tu ina-*provide* kwamba unapotaka kuchukua eneo hili basi angalau upate idhini ya wale.

Sielewi ni kwanini Serikali inapata kigugumizi. Kama pale inapotaja *mining*, basi *procedure* zile zitafuatwa, haina maana kwamba itaondoa au itafuta Sheria ya Madini iliyokuweko au itakayoletwa kesho hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kulinda maeneo haya ili utaratibu uwekwe. Bado naisihi Serikali ikubali, vinginevyo msingi wa kusimamia malisho ya mifugo itakuwa haina maana katika Muswada huu na ni afadhali Serikali ikauelewa ukweli huu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kabisa *concerned* za Waheshimiwa Wabunge na ukweli hili pia ndiyo lengo halisi kwamba tunahakikisha tunalinda maeneo ya wafugaji ambayo siku nyingine yamekuwa yakitwaliwa, huo ndio ukweli kwa sababu tunaelewa hivyo. Lakini pia tunazingatia hii Sheria ambayo ni Sheria Na. 6 ya mwaka 2007. Lakini kwa ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na bahati nzuri nilizungumza na Mheshimiwa Nangoro nikamwambia pendekezo lake ni nzuri wala halina utata na basi niahidi kwamba mapendekezo haya ya kulinda maeneo ya wafugaji tutayaweka kwenye *regulations* ili kuhakikisha kwamba yale maeneo yatakayokuwa yametengwa kwa ajili ya wafugaji yasivamiwe tena na wakulima na wengine kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, tutaweka kwenye *regulation* na niliahidi wakati nikizungumza na Kamati kwamba wakati tutakapokuwa tunaandaa *regulations* tutawahusisha pia baadhi ya Wabunge na Kamati yenyewe ya Kilimo, Mifugo na Maji ili tuangalie ni kwa namna gani *those regulations* zitaweza kuwasaidia wafugaji. Kwa hiyo, pendekezo ni zuri na mimi nafikiri halina ubaya na mimi nafikiri tutaliweka kwenye *regulation* na ningemwomba Mheshimiwa Nangoro yale mapendekezo aliyoyatoa tuya-*include* akayaboreshe vizuri tuyaweke kwenye *regulation* ili tuweze kulinda maeneo ya malisho.

**MWENYEKITI:** Tatizo Mheshimiwa Waziri ni hivi, Waheshimiwa hawa wanasema *regulations* ndiyo haziheshimiwi. Wanataka liwemo kwenye Sheria hii. Sasa ukisema ni zuri unakubaliana naye lakini liende kwenye *category* (b), hawataki. Wanataka iwe *category* (a) iwe Sheria. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu tusaidie. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa shule tulikuwa tunafanya michezo ya kuigiza na mimi niliipenda sana michezo miwili. Ule wa *three witches* na mchezo mmoja wa *Caucasian Chock Cycle* wa kuweka mtoto katikati kwa wanawake wanaogombea mtoto, atakayevuta mkono ule akashinda basi ndiye mwenye mtoto wake. Yule mwenye haki ya mtoto anaona huruma ya kumvuta mtoto, kwa hiyo, anamwachia yule ambaye anastahili. Huo ndiyo mfumo wa haki ambao unaweza kuupata kama hatutaweza kufanya tafakuri na tafakari nzuri katika utaratibu wa kutunga Sheria. Sheria mama inaruhusu kutungwa kwa Sheria ndogo na Sheria ndogo ukiziambia kwamba ziko kwenye daraja (b) kwa wataalam wanaotunga Sheria itakuwa siyo sahihi. Kwa sababu mapendekezo haya yana nia nzuri hiyo hiyo yaku-*protect,* yatahitaji pia urudie kwa kusema kwamba hata haya wafugaji wasiende kwenye maeneo ya wakulima utakuwa tayari unacheza mchezo wa *Caucasian Chock Cycle* na utaleta matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba kama anavyosema Mheshimiwa Waziri na kama mapendekezo ya Serikali yalivyo, zile *regulations* sio *second class* kwa

sababu yako mambo ambayo Vijiji vikishatunga zile Sheria lazima ziheshimiwe. Kwa hiyo, ninashauri kwamba kwa kweli mahali ambapo tutavipa Vijiji mamlaka ya kuamua matumizi ya ardhi ni kuvipa Vijiji hivyo kutumia mamlaka yake chini ya sheria ndogo ambayo Sheria hii inaruhusu Sheria hizo zitungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Waziri kwamba hili ni eneo ambalo linatakiwa kwa kweli liende kwenye Sheria ndogo yaani *by-laws*. Ninasema hivyo nikitambua hofu ya wachungaji na mimi ni mchungaji, lakini pia ni mkulima. Kwa hiyo, nafikiri sioni kwamba ukiweka kwenye Sheria hii ambayo utapata yale ambayo tunataka tuyapate na utayakosa kama utaweka kwenye sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishia hapo.

**MWENYEKITI:** Lakini, jamani Serikali mtusaidie. Hii ya kutuambia Sheria ndogo ziko sawa kabisa na Sheria mama halikai vizuri. Tuseme ukweli tu, kama ingekuwa ni hivyo, basi Sheria ndogo nazo tungezipitisha hapa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nadhani sijui kama inaweza ikasaidia tukisema *subject to other laws* halafu tuendelee na lile la Mheshimiwa Nangoro ili isionekane kwamba tunazuia mtu kuja kuchimba dhahabu ikipatikana na vitu kama hivyo. *Subject to other laws,* basi hii ardhi ya wafugaji ilindwe. Tunapoteza nini hapo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba unaweza ukaona kwamba hatupotezi kitu. Lakini mimi nazungumzia taaluma ya uandishi wa Sheria na mimi kazi yangu ni kushauri na kushawishi. Katika taaluma ya uandishi wa Sheria hatusemi kwamba Sheria ndogo zinafanana kabisa na Sheria kubwa. Lakini tunasema kwamba Mamlaka ya Sheria ndogo yanatokana na Sheria kubwa na ndivyo utaratibu ulivyo na inawezekana naonakana ni msumbufu, lakini jamani ndiyo *professional* yenyewe. Sasa kama itaonekana utafanya hivyo, sasa zile *by-laws* ni za kazi gani? Kwa sababu *by-laws* zina-*binding nature* ambayo inatokana na Sheria Kuu. Nafikiri hili ni la kitaalam na ni vizuri twende kwenye *professional* ya utungaji na uandaaji wa Sheria.

**MWENYEKITI:** Mimi nadhani itatubidi tupige kura. Mheshimiwa Ole Nangoro umesema mara mbili, kwa hiyo, huruhusiwi sasa. Mheshimiwa Ole Sendeka na Mzee Malecela ndiyo bado. Wote wamesema sio kwa hoja hii. Kwa kifupi sana mnapewa dakika zisizozidi tatu. Tuanze na Mheshimiwa Malecele, atafuatiwa na Mheshimiwa Mlingwa na Mheshimiwa Mongela.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza Bunge hili linaingia katika tatizo kubwa ambalo katika miezi michache iliyopita au mwaka jana tumekuwa na matatizo mengi ya wafugaji na wakulima na hakuna wakati wowote ambapo mfugaji ataingiza ng’ombe zake kwa wakulima na isitokee matatizo. Lakini mkulima akiingiza jembe lake kwenye ardhi ya mfugaji mara nyingi sana hakuna kinachofanywa. *(Makofi)*

Kwa kweli mimi naisihi Serikali, ukisema kwamba iende kwenye *regulations,* hivi kuna wakati hapa tumepata kumwuliza Waziri yeyote alituahidi *regulation* na asiiweke halafu tuje tumwulize hapa mbona haujaiweka? Kwa hiyo, mara nyingi tunaahidiwa *regulations,* lakini hatuzioni. Sasa tunataka hii iwe kwenye Sheria na tuipitishe hapa wote tunaiona. Mimi nasema kama wanaona hakuna utata wowote, sasa tatizo liko wapi? Sheria ni Sheria na *regulation* ni *regulation* na kikubwa katika hivi ni Sheria, *otherwise* kama *regulation* ingekuwa sawa na Sheria basi ungeweka kwenye Sheria.

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuingia kwenye mgogoro wa Kanuni, Sheria ndogo na Sheria mama, lakini ninajua tu kwamba mkitunga Sheria ndogo lazima isalimu amri kwa Sheria kubwa ya Bunge. Lakini Kanuni anazokwenda kutunga Waziri haziletwi wala hazitushirikishi sisi, anaweka yeye kwa jinsi anavyoona yeye inafaa. Tulichokuwa tunaomba hapa ni kutumia mamlaka yetu kama Bunge kuhakikisha kwamba huko tulikotoka ni vizuri wenzetu walioko kwenye *front bench* wakajua. Muswada tuliopitisha sasa hivi unawazuia wafugaji na hii tunayoijadili sasa unasajili makazi ya wafugaji kwa nia ya kupunguza na dhamira kuhakikisha kwamba wafugaji wasiondoke kuingia katika maeneo mengine.

Hapa tunachokusudia ni madhumuni yale ya kuhakikisha kwamba ardhi ile iliyokwishatengwa kwa ajili ya wafugaji kwa ajili ya mifugo isiingiliwe hivyo na jembe na shughuli nyingine bila *consents* sio kwamba tunasema ikigundulika kwamba hapa kuna rubi, hapa kuna almasi kwamba Sheria nyingine hazitafuatwa. Tunachotaka na ndiyo maana hata ushauri wa Spika, kwa kutambua Sheria nyingine zinazotawala, bado ninasema kwamba ni vizuri Waziri na Mwanasheria Mkuu wakakubali kifungu hiki, vinginevyo maana ya Sheria nzima kuzungumza kwamba mnataka kulinda wafugaji itakuwa haipo. Kimsingi hatujashindwa kuuza nyama au maziwa kwa sababu hatuna Sheria hii. Tulipitisha Sheria ya ngozi, tumepitisha ya nyama, maziwa na zote hatuuzi kwa sababu ya mambo mengine, lakini sio kwa sababu ya alama hizi tunazokuja kuweka na sio kwa sababu ya Muswada huu. Ni mpaka muamue kuwekeza kama wenzetu wa Botswana, kama wenzetu wa Australia ndipo tutakapoweza kushindana na wenzetu kwenye Soko la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado napendekeza hapa kwamba pendekezo la Mheshimiwa Nangoro liheshimiwe, liingizwe kwenye Muswada huu, ikishindikana tupige kura, ikishindikana tutumie Kanuni yaku-*withdraw* Muswada huu tukaelewane huko nje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa usielekeze kazi za Mwenyekiti hapa. Mwenyekiti ndiyo ataamua yote hayo. Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa.

**MHE. DR. CHARLES MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niseme naunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Nangoro kwa sababu pamoja na kuheshimu sana taaluma nyingine na jinsi inavyopaswa kuzingatiwa, lakini hapa tunatunga Sheria ambayo ni lazima iweze kuwa na manufaa kwa wananchi. Kwa hiyo,

sio suala la kusema hivi ndivyo uandishi wa Sheria, hapana. Ni lazima tuangalie mantiki ya Sheria yenyewe tunayoitunga ili isilete migogoro kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilichopendekezwa na Mheshimiwa Nangoro hakivunji malengo na madhumuni ya Muswada, mimi nashauri Bunge hili likubali mapendekezo hayo kwa sababu nia yake ni kuwalinda wafugaji ambao tunafahamu ni kundi moja ambalo ipo mifano ya kutosha ya jinsi wanavyoteseka kwa kutokuwepo na Sheria zinazowalinda katika maeneo waliyonayo. Mifano iko mingi na sihitaji kuirudia hapa, lakini Mheshimiwa Nangoro amezingatia haja ya Sheria hii kujielekeza katika kuleta ufanisi katika ufugaji na kuondoa migogoro ambayo imepelekea wafugaji kupoteza mifugo yao kwa sababu tu ya kutokuwepo na Sheria kama hiyo. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nizungumzie ufugaji. Kwanza nataka nijitambulishe kwamba mimi natoka eneo la wafugaji, wakulima na wavuvi. Nimesikiliza sana maneno haya. Watu wangekuwa wanafanya *cross reference* katika kutunga Sheria. Kituo cha kwanza cha kujifunza namna ya matumizi ya ardhi ingekuwa ni Ukerewe, kwa sababu tuna ardhi ndogo sana na finyu, lakini tunafanya vyote hivyo kwa uwiano na kwa taratibu na wanaovuruga ni *Administration* ya Serikali.

Wakati mwingine hata maeneo tuliyoyatenga kwa ajili ya mifugo anakuja kwenye Tarafa ya Mumbuga anapanda miti ambayo haikuwepo hata siku moja. Lakini sisi tulitenga na maeneo ya visiwa *specific* kwa uvuvi tu, anika samaki unavyotaka. Msimu wa samaki ukiisha viache visiwa vilivyo. Sasa watu wanaanza kufanya na makazi na vyote hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *observation* iliyonifanya nisimame baada ya mazungumzo haya, nadhani tuna tatizo la utungaji wa sheria, hatuhusianishi sheria ya ardhi na shughuli za watu juu ya ardhi aliyotupa Mungu. Kwa hiyo, pamoja na kuitunga hii, tunaanza kuona matatizo wafugaji wanayoyaelekeza. Lakini tutakuja kesho tutakuwa na matatizo na wavuvi. Hatuwezi kuvua tumesimama hewani tu majini, tunapaswa kurudi nchi kavu. Hilo eneo halijatengwa, sasa unalinda wakulima, unalinda wafugaji, hujamlinda huyu mvuvi na shughuli zake.

Kwa hiyo, mimi *observation* niliyotaka nisimame niseme, hii sheria tutaipitisha. Lakini hebu tukae tena tutafute watu waliobobea katika kuandaa sheria na wafanye *cross reference,* sheria zetu nyingi zinagongana ndiyo maana zinashindikana utekelezaji. Naomba hii *observation* tuifanye, lakini ningewaomba wafugaji hako kakitu kakiingizwa mle, tunaingiza hasara gani kubwa! Tukaweke na kesho Waziri yule yule wa Uvuvi alete sheria ya kulinda maeneo ya wavuvi. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naona jambo limetuchukulia muda mrefu kidogo hili. Lakini, wafugaji ni Watanzania, wakulima ni Watanzania na wavuvi ni Watanzania. Tunachojaribu kufanya ni kuona namna ya kusaidia makundi yote yaweze kuishi kwa salama. Suala hapa kwanza tuweke kwenye *regulations* au tuweke kwenye sheria, kwangu mimi halinipi tatizo hata kidogo. Mimi nadhani kimsingi tungekubali tu

tuweke kwenye sheria mama, isipokuwa tutafute tu namna ambayo haitatoa picha kwamba mfugaji yeye hapeleki mifugo kwa mkulima, maana picha unayoipata hapa ni kama vile ni wakulima tu ndio wanakwenda ku-*encroach* kwenye *grazing land*, lakini *the vise versa is equally true*.

Mimi natoka Rukwa na *we are having that problem night and day*. Kwa hiyo, cha msingi ambacho tunaweza kufanya tu ni kwamba tukubali ama tuchukue *version* yako Mwenyekiti kwamba *subject to other laws* na nini na nini, basi Halmashauri au Serikali ya Kijiji itakuwa na mamlaka fulani fulani. Lakini kwa sababu tumekwenda mle ndani, tumejaribu ku-*categorize* na tukasema *specifically* kwamba usi-*encroach* katika eneo hili au *the other way round*, tukaweza tu kuwa na lugha ambayo inaonyesha kwamba tuko pale kulinda makundi yote mawili. Mimi nadhani halina tatizo, tuikubali na tuweke kwenye sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuamua hili, nadhani limekaa vizuri. Ninaomba tu lile eneo la wengine nao kwenda kwenye ardhi ya mkulima na kuharibu mazao na kadhalika nalo labda litafutiwe majibu. Sijui Waziri yuko wapi! Maana tukiruhusu Mwanasheria Mkuu akienda kuweka anaambiwa ameingia kinyemela. Pengine litengenezwe hivi sasa ili kabla hatujamaliza kupitisha Muswada, haki ya Serikali ya Kijiji isiwe tu ni kulinda eneo la wafugaji ila ni kulinda pia eneo la wakulima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameliweka vizuri na nafikiri halitaleta madhara yoyote kwa kutambua kwamba wanaoonewa sio wafugaji tu. Napenda nitoe mfano kule Kilosa, kuanzia mwaka 1990 mpaka sasa hivi watu waliokufa kule ni karibu 40 na waliouawa wengi ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri kama alivyoliweka Mheshimiwa Waziri Mkuu, yale maeneo uliyoyaweka wewe yale, sijayashika vizuri, lakini najua wewe ni mtalaam mzuri, basi…

**MWENYEKITI:** *Subject to other written laws!*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Ndiyo, kwa hiyo, wakulima walindwe, wavuvi walindwe na wafugaji walindwe ili pasitokee *group* la mtu mwingine mkulima kwenda kuvamia la mfugaji na mfugaji kwenda kuvamia la mkulima ambalo limetengwa kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2007.

**MWENYEKITI:** Sasa, napendekeza basi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kabla hatujakipitisha hiki, tuendelee, mtupe *version* na *CPD* ambayo itajibu hilo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kwamba kwa vile hii sheria ni sheria ya *strategic grazing*,

ingetosha tu kusema kwamba *subject to other laws* kwa sababu kuna *laws* nyingine ambazo zinalinda matumizi ya ardhi kwa ajili ya wakulima.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ibaki hiyo, *Nangoro's amendment* linapita likitanguliwa na maneno hayo! Ndivyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana! Nilikuwa nafikiri kwamba, sijui kama atakubaliana na mimi, nilikuwa nafikiri kwamba tungeanza tu kwamba: *"subject to other laws, the Village Council shall set out aside part of the communion village land to be strategic grazing land in accordance with the provisions of the Land Use Plan Act"*, ambalo ndilo liko kwenye Muswada.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, lakini tunazungumza badiliko lililoletwa na Mheshimiwa Nangoro, tulifanyeje hili? Tulikatae, tulikubali? Nadhani Serikali imekwishalikubali.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Nangoro, ulipendekeza marekebisho kwenye Ibara ya 18.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko niliyopendekeza baada ya mengine kufanywa na Serikali, naondoa haya ya kwangu sasa.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki *basically* kinazungumzia *grazing land management* na hapa kuna *principles* za ku-*manage grazing land* iwe kwa ajili ya *wildlife*, iwe kwa ajili ya *livestock*. *Principle* inayotumiwa, kama alivyoeleza Waziri, ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na namba inayokubalika katika *a piece of land*. Kitalaam tunatumia *principle* ya *carrying capacity* ambayo ni kigezo cha kitalaam, kinafanywa kisayansi, kiutafiti ili kupata kiwango hicho kwamba eneo hili la ardhi lina uwezo wa kubeba mifugo kadhaa yenye uzito kadhaa.

Lakini kwa sababu hicho ni kigumu, mara nyingi huwa wanatumia *limits of acceptable use* ambayo wanakubaliana watalaam waliokaa, jopo la watalaam lile au wadau waliokaa kuamua matumizi ya ardhi waseme kunaruhusiwa watu wangapi au mifugo kiasi gani kwenye eneo hili. Sasa *principle* hii, watalaam wa mifugo wanajua na watalaam wapo na nina amini Waziri anajua vile vile, lakini wamekuwa hawafanyi,

hawatumii na ndiyo maana tumekuwa na matatizo ya watu kuhamahama na mambo ya ku-*over stock*. Sasa nimeona hapa maneno yanayotumika ni kubadilisha badala ya kuondoa, tunasema tuta-harvest, sawa, *it means the same thing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilichotaka ufafanuzi ni kwamba: Je, sheria hii sasa ni kweli itawezesha kutumia hizo *basic principles* za ku-*manage grazing land* kwa ku-*determine carrying capacity* au *limit of acceptable use* na ku-*adhere to* hizo *principles*. Kama haitakiwi, haitakiwi, *otherwise* kama siyo hivi, nataka Mheshimiwa Waziri anieleze, tutatumia maajabu gani kuhakikisha kwamba *land* itakuwa *properly managed* ili iwe endelevu kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa *concern* ya Mheshimiwa Profesa pale na ni ukweli usiopingika kwamba *carrying capacity* ya ng'ombe ina-*depend* na mahali. Kuna mahali ng'ombe wanaweza wakakaa wengi kuliko mahali pengine, ina-*depend* na hali halisi, *climatic condition* na kadhalika na ndiyo maana tumeona Namibia ambao sehemu kubwa ni jangwa, lakini *contribution* ya sekta ya mifugo ni kubwa zaidi kuliko Tanzania ambayo ni *fertile* na ina majani mazuri.

Sasa haya yote ambayo anayazungumza Profesa ndiyo tutayaweka kwenye *regulations* kwa sababu inayotunga sheria kwamba wapi pawe na kilimo, wapi pawe na mifugo, wapi pawe na misitu ni ile Sheria Na. 6 ya mwaka 2003. Kwa hiyo, tumeyaacha kwa sababu kwenye *regulations*, tusingeweza kuyaandika hapa, *carrying capacity* ya Mwanza ni tofauti na *carrying capacity* ya Chato, ni tofauti na *carrying capacity* ya Mtwara, ni tofauti na *carrying capacity* ya Lindi, ni tofauti na *carrying capacity* ya Wagogo akina Malecela na sehemu nyingine pia. Kwa hiyo, ndiyo maana tumeiacha ili kusudi wakati watakapokuwa wanapanga yale maeneo waweze kuangalia *carrying capacity* ya kila eneo.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 20

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Gosbert, hebu tusikie hoja zako!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta marekebisho kwenye kifungu cha 20 ambacho kinazungumzia *stocking rate* and *measures in case of excess livestock units*. Marekebisho yangu hapa yanahusiana na neno *"removal"* ambayo ndiyo *concern* yangu kubwa sana katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno ambalo limetumika hapa ni *removal of the excess livestock unit*. Sasa kwenye mapendekezo yangu nilikuwa napendekeza hili neno

*removal,* liondoke na badala yake liingie neno *harvesting or any other appropriate measures*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Ukiangalia hili neno *removal*, linatumika kama vile hii *excess*, yaani hawa mifugo ambao watakuwa wanaonekana wamezidi kwenye hilo eneo, kama vile ni kitu ambacho hakina thamani kwamba inatakiwa kiondolewe tu.

Sasa, kwa sababu tunatunga sheria kwa manufaa ya wananchi wetu wafugaji na tungetaka sheria hii iwe sheria rafiki *(very friendly)* kwa wafugaji, ndiyo maana nikapendekeza kwamba huyu *Inspector* akishagundua kwamba kuna *excess* ya mifugo, basi iwe ni kazi yake ya kwanza ya kuwashauri wafugaji wavune ile mifugo kama tunavyoshauri wakulima wengine wanavyovuna pamba, wanavyovuna kahawa, wavune mifugo yao katika kipindi cha miaka mitatu. Kama mtu pengine hatapenda kuvuna mifugo yake hii katika kipindi cha miaka mitatu, ndiyo maana nikapendekeza kwamba badala ya kutumia neno *harvest*, tuongezee *or any other appropriate measures*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini hapa? Ni kwamba, kwa yule ambaye hatapenda pengine kuuza, anaweza akahamisha mifugo yake kutoka eneo hilo, pengine akapeleka kwenye *ranch*, pengine anaweza akawa amepata ardhi nyingine au anaweza akawa amepeleka nyumbani kwake kufuga katika ile *zero grazing* au hata akaweza kuwagawia ndugu, jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa neno sahihi hapa ndiyo hilo ambalo nimependekeza kwamba tuweke *harvesting or any other appropriate measures* ambalo naamini kabisa likifanyiwa mabadiliko hata Mheshimiwa Waziri kaka yangu Magufuli halitampa shida hata kidogo. Lakini tukibakiza neno *removal*, ni kama vile unaingia kwenye shamba unasema una *remove* au unaondoa yale majani ambayo hayatakiwi kwenye shamba lako labda la mahindi, unayatupa. Lakini sasa hapa tunazungumzia mifugo kama zao lingine kwamba ni vizuri tutumie neno *proper* ambalo kwa kweli '*harvest'* ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu nimeyatoa kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lakini nadhani sasa tukiingia hasa kwenye *drafting* kabisa tutapata shida. Ukiambiwa punguza mifugo, siyo maana yake uwaue hapo hapo. Mimi nilikuwa nadhani tafsiri hiyo inakuwa ni tafisiri tu kwa sababu *harvest* ni sehemu ya ku-*remove*, kuwagawia marafiki ni sehemu ya ku-*remove*, vyovyote vile. Nadhani hata Mheshimiwa *AG* atakubaliana nami kwamba *removal in a legal sense* siyo maana yake ufanye uharibifu, ni kwamba upunguze mifugo kwa sababu imethibitika kuzidi ule uwezo wa kuweza kupata malisho pale na badala yake inakuwa ni uharibifu tu. Kwa hiyo, *removal by any other means.* Ukiwa na hasira ukawapiga risasi, sasa hiyo, basi

wewe ni mtu wa ajabu kidogo. Lakini, bado u-*de-stock* kufikia kiwango ambacho kimeruhusiwa na *Inspector*, ndiyo lengo hilo.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa maelekezo yako na hatimaye tutakubaliana *grazing* kwenye kifungu hiki iweje. Lakini mimi ningependa kusaidia kidogo kwa uzoefu. Wafugaji ukiwaambia punguza mifugo, kwanza unawarejesha kwenye ukoloni ambako hii lugha ndiyo ilianza na kumewahi kuwepo na mpango huo punguza mifugo. Kwa hiyo, lina *colonial history*. Lakini cha pili, mimi katika utumishi wangu katika nafasi ya Naibu Waziri wakati fulani nilisafiri na aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, alitumia lugha hii ya kusema punguza, wafugaji walikuwa wanajisikia vibaya sana na wanasikitika vibaya sana.

Mwishoni, lugha hiyo ilibadilika ikawa vuna mifugo, kwa sababu wafugaji wanaelewa sana tofauti ya punguza na kuvuna mifugo. Kuvuna mifugo wanakubali zaidi kwa sababu wanaelewa kuwa mali ile ina thamani, ni zao.

Kwa hiyo, naunga mkono mapendekezo ya Mheshimiwa Blandes na hasa kwa sababu Muswada huu utakapokuwa sheria utatuweka kwenye mfumo utakaobadilisha aina ya ufugaji hapa nchini ambapo ningeweza kusema kwa Kiingereza: *"this will be a transformation system in the livestock sector"*. Kwa sababu wafugaji wetu wakishaelewa maana ya kufuga ili hatimaye wavune, watapenda kuvuna mifugo bora na siyo mingi kama ambavyo ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo ya Mheshimiwa Blandes ni katika kujenga taswira chanya ya Muswada kuliko neno *removal* ina taswira hasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, una *objection* kwa hiyo *harvesting? It is just*…sijui!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vifungu ambavyo sisi Serikali tulivifanyia kazi sana ni pamoja na kifungu hiki cha 20, na ndiyo maana ukikiangalia katika hali halisi, kwanza ile *power* ya *Inspector* ni kama tumeipunguza na kama tumeimaliza. Ndiyo maana tumeeleza kwamba huyu *Inspector* atatoa *notice* ya miaka mitatu. Wakati huo wa miaka mitatu, huyu mfugaji atakuwa ana-*harvest* hiyo mifugo yake, anaweza akauza, anaweza akaihamishia mahali pengine, anaweza akafanya nini, ikishapita miaka mitatu, bado tena panaweza pakawa na *extension* ya *notice* sasa nyingine ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka sita yote, mimi nilifikiri kwa sababu tumeamua kutunga sheria, sheria siyo lazima iwe na maneno matamu tu, lazima ifike mahali mtu ambaye atakataa kwa miaka sita yote pawepo na *removal*, *otherwise* hii haitakuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba, kwa sababu tumekubali mengi na mabadiliko mengi, miaka mitatu imepita, huyo yeye hataki tu, hata ku-*harvest* hataki,

hata kumpa mdogo wake hataki, anapewa tena miaka mingine mitatu, bado hasikilizi tu, kwa nini tusi-*remove*? Hii ndiyo maana ya sheria! Sheria lazima kwa upande mwingine uwe mkali ili kusudi tuweze kwenda mbele. *Otherwise* tutazungumza maneno matamu matamu tu, watu hawataweza kutekeleza. Mimi naona hili neno *remove* ndilo *appropriate word* kusudi litumike na hii *remove* itatumika baada ya miaka sita. Ni mtu gani ambaye hasikilizi miaka sita yote?

**MWENYEKITI:** Mkorofi sana huyo! *(Kicheko)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubali maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwamba angalau Serikali imekubali kutoa dhana ya kwamba tunakupa muda huu mpaka imefika miaka sita. Lakini pia ninakubaliana na dhana iliyoletwa na Mheshimiwa Blandes na kuungwa mkono na Mheshimiwa Mlingwa, tuko katika siasa tena mimi ninaishangaa CCM kwa kutunga Sheria kwa kutumia neno “Punguza”, hili neno!

**MWENYEKITI:** Wewe unaihurumia CCM?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kabisa, *yes I agree because you are harming us for nothing. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujawaomba mtupe vitu vya kuwashambulia, lakini kwa dhana hii mnatupa waziwazi kuwa Sheria hii ilikataliwa wakati wa ukoloni Mwalimu alipokuwa anaomba wananchi wamuunge mkono. Marehemu Bomani aliulizwa Kisukuma *akopunguja e ng’ombe* kwamba atapunguza ng’ombe? Naye akaambiwa kwa Kiswahili akasema: “Mimi mkinipa madaraka katika TANU na baadaye imekuwa CCM sitatunga Sheria ya kupunguza ng’ombe.” Leo Chama kilichozaliwa na Marehemu ndiyo kinatunga Sheria ya kupunguza ng’ombe, jambo hili halieleweki! Hii ni siasa na *some of us* tunashangaa mnayemtungia hii Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo Rais atakayekuwa anatembea kule anauza hii Sheria tutamwuliza maswali, wewe utapunguza ng’ombe zetu au hapana? *That is the issue* na *after all* watu wa kawaida hawaelewi. Wewe Mheshimiwa hatujakuuliza kwenye benki *account* yako una hela ngapi? Kwanini hatukwambii wewe punguza, zimezidi sana? Haya ndiyo maelezo ambayo lazima tutoe kwa wananchi. Lakini tukieleza wananchi kwamba sasa tumejenga kiwanda cha labda Ruvu kinahitaji ng’ombe 3,000,000 kwa mwaka na kingine tunajenga Bariadi kinahitaji ng’ombe 3,000,000 na kingine Longido na wapi wananchi watajua kuwa sasa tumepata soko zuri la kuweza kuuza mifugo yetu na kwamba zao hili la mifugo linathaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *removal* ni Sheria toa na hii tunazungumza hapa keshokutwa hatuko hapa na wengine na wengine watatuletea vitu vya ajabu *already,* sasa hivi ninavyokuambia, Mara watu wanakuwa *removed* wanaondolewa kwa lazima. Mpaka inaleta sasa hisia za ukabila! Nyinyi leo mnatunga Sheria *removed*, tumieni maneno ya

busara yaliyoletwa na Blandes. Hii ni kwa ajili yenu pia, lakini mkituachia tutawatengeneza mbele ya safari. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, inaonekana ni suala la lugha tu kuvuna au kuondoa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kazi ya Bunge ni pamoja na kutunga Sheria na Sheria ni lazima iwasaidie hawa wanaotungiwa Sheria. Mimi pamoja na kwamba siyo mtaalamu sana wa Sheria kama neno *removal* ndiyo linaleta maana mbaya, basi mimi naona sina tatizo, badala ya *removal* tunaweza tukaweka *harvest* na ninafikiri halina ubaya kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante na wale wanaosema Serikali ya CCM siyo sikivu ninawashangaa maana yake mnaona jinsi mambo yanavyobadilika, tunatunga kwa pamoja. Hadi Mheshimiwa John Cheyo anaihurumia CCM!

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 21

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara 22
Ibara 23
Ibara 24
Ibara 25
Ibara 26
Ibara 27
Ibara 28
Ibara 29
Ibara 30
Ibara 31
Ibara 32
Ibara 33
Ibara 34
Ibara 35
Ibara 36
Ibara 37

Ibara 38
Ibara 39
Ibara 40
Ibara 41
Ibara 42
Ibara 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara 44

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2
Jedwali la 3

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri atoe taarifa ya kazi ya Kamati ya Bunge Zima, nimepata ufumbuzi na maelekezo mazuri sana ya Kiswahili kutoka kwa mtaalamu aliyebobea Mheshimiwa Mudhihir. Yanasema hivi, kwa mwanadamu kile ambacho anazaa kinaitwa mtoto, kwa wanyama wote ni ndama, siyo mtoto; kwa kuku ni vifaranga na kwa ndege ni kinda au makinda ya ndege.

Kwa hiyo, nitaangalia kuwa mnafuata Kiswahili sahihi, msiseme mtoto wa kondoo hapana, ni ndama wa kondoo, au mtoto wa kuku, hapana ni kifaranga. Mtoto ni wa binadamu tu.

Sasa namwita Mheshimiwa Waziri kwa taarifa ya kazi ya Kamati**.**

**Muswada ya Sheria ya Maeneo ya Malishona Rasilimali za Vyakula vya Mifugo ya mwaka 2010 (*The Grazing Land and Animal Feeding Resources Act of 2010)***

*(Kusomwa mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati imeupitia Muswada ya Sheria ya Maeneo ya Malishona Rasilimali za Vyakula vya Mifugo ya mwaka 2010, yaani *The Grazing Land and Animal Feeding Resources Act of 2010* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo ya Mwaka 2010, yaani *The grazing Land and Animal Feed Resources Act of 2010,* kama ulivyorekebishwa na Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MABO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kufikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huo sasa umesomwa kwa mara ya tatu na kwa mujibu wa Kanuni ya 91, sasa ni Sheria iliyopitishwa na Bunge ikisubiri tu ridhaa au kibali cha Mheshimiwa Rais. Ninawapongeza sana Serikali walioshirikiana kwa pamoja kutoa ufafanuzi, Muswada ulikuwa mgumu, unagusa mambo mengi sana tuliyoyazoea mengine ya kimila na mambo ya kimila ni vigumu sana kuyaondoka hata pale yanapokuwa na hasara kwa uchumi, lakini hatimaye kwa jinsi ambavyo tunaendelea kujadili kwa dhati, tumefikia mwisho mzuri na Muswada huu sasa ni bora zaidi kwa jitihada za Waheshimiwa Wabunge kuliko ambavyo ungekuwa kama ulivyofika hapa Bungeni na hii ndiyo kazi ya Bunge. Ninawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli ya kesho itakuwa ni Sheria ya Madini. Tunaingia katika Sheria ya Madini na imebidi niwaambie hivyo ili watu wajiandae msije mkaenda kupumzika bila kujua kesho tunaanza na shughuli gani. Baada ya kusema hivyo. Sasa naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.30 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 21 Aprili, 2010, Saa Tatu Asubuhi)*